

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI  
MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA  
WA FEDHA 2009/2010

---

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Sanduku la Posta 9080,  
Simu : 255 (022) 2115157/8  
Nukishi: 255 (022) 2117527  
Barua pepe: [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz)  
Tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)  
DAR ES SALAAM,  
Tanzania.

31 Machi, 2011

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Simu ya Upepo: "Ukaguzi"  
D'Salaam  
simu: 255(022)2115157/8  
Nukishi: 255(022)2117527  
Barua pepe: [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz)  
Tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)  
Unapojibu tafadhali taja  
Kumb. Na.CA.4/37/01/2009/10



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa  
Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Barabara ya Samora /Ohio,  
S.L.P. 9080,  
DAR ES SALAAM.  
31 Machi 2011

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
S.L.P. 9120,  
Ikulu,  
DAR ES SALAAM.

**YAH : KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA  
MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU  
UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA  
WA FEDHA 2009/2010**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebisha 2005), ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya 3 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008, nawasilisha kwako ripoti yangu ya nne ya mwaka ya ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi Nyinginezo.

Ripoti hii inajumuisha taarifa za ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kwa vipindi vilivyoishia tarehe 30 Septemba 2009, 31 Disemba 2009 na tarehe 30 Juni 2010.

Nawasilisha,

Ludovick S.L. Utouh  
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

**Ofisi ya Mdhiditi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

*(Imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)*

Kazi na wajibu wa Mdhiditi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeainishwa katika Ibara 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebisha 2005) na kufafanuliwa na Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka, 2008.

**Dira ya Ofisi**

Kuwa kituo cha ubora kwenye ukaguzi wa hesabu katika sekta ya ukaguzi wa umma.

**Lengo la Ofisi**

Kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia raslimali za umma.

Katika kutoa huduma zenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya misingi ifuatayo:

Kutopendelea	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma kwa wateja wake kwa haki.
Ubora	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.
Uadilifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.
Kujali Watu	Tunajali mahitaji ya wadau kwa kujenga utamaduni mzuri wa kujali wateja na kuwa na watumishi wenye uwezo na tija.
Ubunifu	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya Taasisi.
Matumizi bora ya raslimali za umma	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi inayozingatia matumizi bora ya raslimali zilizokabidhiwa kwake.

# YALIYOMO

## Ukurasa

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali .....	iii
Dira ya Ofisi .....	iii
Lengo la Ofisi.....	iii
Shukrani.....	xi
Dibaji .....	xiii
Muhtasari .....	xv
SURA YA KWANZA .....	1
Utangulizi na Taarifa za Jumla.....	1
SURA YA PILI.....	9
Aina za Hati za Ukaguzi Zilizotolewa .....	9
SURA YA TATU .....	15
Muhtasari wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Mwaka Uliopita Ambayo Hayajatekelezwa .....	15
SURA YA NNE .....	25
Masuala Muhimu Ambayo Hayakutolewa Taarifa Katika Ripoti ya Mwaka Uliotangulia .....	25
SURA YA TANO .....	33
Usimamizi wa Mapato na Matumizi.....	33
SURA YA SITA.....	53
Usimamizi wa Sheria ya Manunuzi na Mikataba .....	53
SURA YA SABA.....	63
Usimamizi wa Raslimali .....	63
SURA YA NANE .....	69
Usimamizi wa Raslimali Watu .....	69
SURA YA TISA.....	79
Utawala Bora.....	79
SURA YA KUMI .....	91

Utendaji wa Mashirika Yaliyopo na Yaliyobinafsishwa .....	91
SURA YA KUMI NA MOJA .....	105
Teknolojia ya Habari na Mawasiliano .....	105
SURA YA KUMI NA MBILI .....	113
Matokeo ya Kaguzi Maalumu.....	113
SURA YA KUMI NA TATU.....	117
Hitimisho na Mapendekezo .....	117
VIAMBATANISHO .....	Error! Bookmark not defined.

## MAJEDWALI

### Ukurasa

Jedwali 1: Mgawanyo wa Kaguzi za Mashirika ya Umma .....	7
Jedwali 2: Kuwasilisha Hesabu .....	12
Jedwali 3: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi.....	13
Jedwali 4: Mapendekezo Ambayo Hayakutelezwa 2007/2008....	16
Jedwali 5: Muhtasari wa Mapendekezo Ambayo Hayajatekelezwa.....	Error! Bookmark not defined.
Jedwali 6: Mapendekezo Ambayo Hayajatekelezwa 2008/2009 ..	18
Jedwali 7: Mikopo ya Wanafunzi Ambayo Haijarejeshwa .....	30
Jedwali 8: Madeni Ambayo Hayajakusanywa .....	34
Jedwali 9: Masurufu ambayo Hayajarejeshwa .....	42
Jedwali 10: Matumizi Yasiyo na Viambatanisho Timilifu.....	44
Jedwali 11: Matumizi Yaliyozidi Kiasi cha Bajeti.....	45
Jedwali 12: Malipo Yanayotia Shaka .....	47
Jedwali 13: Mapato ya Serikali.....	98



## VIELELEZO

### Ukurasa

Kielelezo 1: Mgawanyo wa Kaguzi za Mashirika ya Umma .....	7
Kielelezo 2: Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma ....	13
Kielelezo 3: Mapendekezo Ambayo Hayajatekelezwa .....	18
Kielelezo 4: Mapato ya Serikali.....	99





## SHUKRANI

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za mara kwa mara za kutilia msisitizo kwenye ripoti zangu za jumla za mwaka za ukaguzi.

Shukrani zangu za dhati ziende kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wenyeviti na waheshimiwa wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge na kwa wabunge wote kwa kujitolea kwao kujadili mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti zangu.

Napenda, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi za Wakurugenzi, Watendaji Wakuu na Wafanyakazi wote wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zilizokaguliwa kwa ushirikiano walioutoa kwa wakaguzi wakati wa zoezi zima la ukaguzi.

Vilevile, ninapenda kutoa shukrani zangu kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuhakikisha kazi ya uchapaji wa ripoti hii inakamilika na hivyo kuifanya itoke na kuweza kupelekwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge kwa muda uliowekwa kisheria.

Zaidi, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wabia wa maendeleo ambao wamekuwa wakitoa misaada kwa Ofisi yangu na hususani Mpango wa Maboresho wa Menejimenti ya Fedha za Umma (PFMRP) chini ya uratibu wa Benki ya Dunia, na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (SNAO), Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Sweden (SIDA) na wadau wote wanaoitakia mema Ofisi yangu na waliochangia kwa sehemu kubwa kuifanya kuwa ya kisasa.

Zaidi ya hayo, napenda kuyashukuru Makampuni Binafsi ya Ukaguzi ambayo yamekuwa yakifanya kazi za ukaguzi na Ofisi yangu katika ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru sana wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kujitolea kwao na uvumilivu waliouonyesha umekuwa wa manufaa sana na faraja sana kwangu. Nawasihi wafanyakazi wa ofisi ya Taifa ya Ukaguzi waendeleo kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa bidii na umoja kwa siku zijazo ili kuendelea kudumisha heshima ya Ofisi yetu katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora katika kuhimiza uwajibikaji na kuzingatia thamani ya fedha katika makusanyo na matumizi ya raslimali za Umma.

## DIBAJI


Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya nne ya mwaka kuhusu Taarifa ya ukaguzi wa Mashirika na Taasisi za Umma kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2010. Ripoti hii ni mkusanyiko wa ripoti za kaguzi mbalimbali za Mashirika ya Umma zilizofanyika kwa kipindi husika. Ripoti hii inaelezea kwa kifupi mambo ambayo yamekuwa ni kikwazo cha ufanisi katika kutekeleza malengo ya kuanzishwa kwa Mashirika na Taasisi za Umma husika.

Ripoti hii, imelenga kuwapa wadau kama vile Serikali, Bunge, Mahakama, Wabia wa Maendeleo, Asasi za Kijamii, na Umma wa Watanzania kwa ujumla muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa hesabu pamoja na kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha ufanisi wa utendaji kazi wa Mashirika na Taasisi za Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010. Kwa kipindi hiki ambapo kumekuwa na ongezeko kubwa la uwajibikaji kwa umma, limekuwa ni jambo muhimu kwa watendaji kutoa taarifa zao za utendaji ikiwa ni pamoja na taarifa za fedha na usimamiaji wa mali za umma ndani ya Mashirika na Taasisi za Umma. Nimeadaa ripoti hii katika kuhakikisha kuwa watoa maamuzi katika nchi yetu wanapata taarifa muhimu na ambazo hazijapitwa na wakati zenye mapendekezo ya kitaalamu juu ya taarifa za fedha na usimamizi wa raslimali za umma katika Mashirika na Taasisi za Umma. Nimeandaa ripoti hii kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sehemu ya 34 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008.

Ili kuhakikisha kuwa kazi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inachangia katika maendeleo ya Taifa, Ofisi yangu mara kwa mara imekuwa ikiboresha mbinu za ukaguzi ili kuona kuwa matokeo ya kaguzi yanakidhi haja za wadau wetu. Kujenga uwezo wa wakaguzi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni jambo linalopewa kipaumbele ili kuhakikisha wanapata uelewa wa Sheria, Miongozo, Kanuni na matoleo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na mabadiliko yanayofanywa na Taasisi za Taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi za Kimataifa kama vile "IFAC", "INTOSAI" na nyiginezo ambazo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama.

Ni vyema ikafahamika kwamba, wakati vyombo vyenye dhamana ya uangalizi (Oversight Organs) vina jukumu la kuhakikisha kuwa Sheria na taratibu zinafuatwa katika Mashirika na Taasisi za Umma, Bodi za Wakurugenzi na Maafisa Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi hizo kwa upande wao wana jukumu la kuweka mifumo imara ya udhibiti wa ndani na miongozo ili kuhakikisha kwamba sheria na taratibu hizo zinafuatwa.

Juu ya yote, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake kwa ujumla, Kamati za Bunge za usimamizi wa utendaji, Bunge kwa ujumla, Wabia wa Maendeleo na Benki ya Dunia kwa michango yao katika kuweka msisitizo wa uwepo kwa uwajibikaji katika nchi yetu.



Ludovick S. L. Utouh

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

---

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
S.L.P. 9080,  
Dar es Salaam,

31 Machi 2011

## MUHTASARI

### i Utangulizi

Ripoti hii ya ukaguzi inatolewa kulingana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa mwaka 2005) na kufafanuliwa katika Sehemu ya 34 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Ripoti hii inahusu kaguzi za vipindi vinavyoishia tarehe 30 Septemba, 2009; tarehe 31 Disemba, 2009 na tarehe 30 Juni, 2010. Muhtasari huu unaelezea kwa kifupi mambo ambayo yameelezwa kwa kina katika ripoti hii ambayo yanahitaji kushughulikiwa na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika na Taasisi za Umma husika.

Mambo yaliyoainishwa ni pamoja na: Hati za ukaguzi, utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita, usimamizi wa mapato na matumizi, usimamizi wa manunuzi na mikataba, usimamizi wa raslimali, usimamizi wa raslimali watu, utawala bora, utendaji wa Mashirika yaliyopo na yaliyobinafsishwa, teknolojia ya habari na mawasiliano, matokeo ya ukaguzi maalum na mapendekezo ya ukaguzi.

### ii Hati za Ukaguzi

Kufikia tarehe 25 Februari, 2011, nilifanikiwa kuhitimisha kaguzi 122 (71.7%) za Mashirika ya Umma kati ya kaguzi 170 zinazotakiwa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika kaguzi zilizokamilika, kaguzi za Mashirika ya Umma 92 (75.4%) zilipata hati safi, kaguzi 12 (9.8%) zilipata hati safi yenye masuala ya msisitizo, kaguzi 10 (8.2%) zilipata hati yenye shaka, kaguzi 7 (5.8%) zilipata hati zenye shaka zenye masuala ya msisitizo ambapo sikuweza kutoa maoni ya ukaguzi kwa shirika 1 (0.8%) na hakuna shirika lililopata hati mbaya.

### iii Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa juhudi alizozifanya kuifahamisha Ofisi yangu kuhusu utekelezaji wa mapendekezo niliyoyatoa katika taarifa zangu za miaka iliyopita. Hata hivyo, mengi ya mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi zilizopita hayajatekelezwa, juhudi kidogo zimechukuliwa na Serikali, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika kuhusiana na utekelezaji wa mapendekezo hayo. Mengi ya mapendekezo hayo bado hayajatekelezwa kabisa au yametatekelezwa kwa kiwango kidogo. Ni imani yangu kuwa Serikali, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma watachukua hatua madhubuti za kuhakikisha kuwa mapendekezo ya ripoti za miaka iliyopita yanatekelezwa kwa ajili ya kuboresha utendaji mzuri wa Mashirika na Taasisi za Umma.

**iv Usimamizi wa Mapato na Matumizi**

Upembuzi wa usimamizi wa mapato katika Mashirika ya Umma ulibaini mapungufu mbalimbali yakiwemo mianya katika ukusanyaji wa madeni ambao umekuwa na udhaifu mkubwa katika Mashirika ya Umma, kuvuja kwa maji, uandaaji wa ankara zisizo sahihi kwa wateja na upotevu wa nishati ya umeme iliyozalishwa ambacho kimekuwa ni chanzo kikubwa cha upotevu wa mapato katika Mamlaka za Maji na Shirika la Umeme na Ugavi Tanzania. Tulibaini pia kutoweka bayana mapato na matumizi kama inavyotakiwa na matakwa ya viwango vya kihasibu hali ambayo inaweza kusababisha vitendo vya ubadhirifu. Kwa upande wa matumizi, tumegundua udhaifu katika mifumo ya ndani ya udhibiti wa malipo, kutokuwepo kwa nyaraka za kuthibitisha malipo, kutorejeshwa kwa masurufu na udhaifu katika udhibiti wa bajeti. Haya yote yameelezwa zaidi katika sura ya tano ya taarifa hii.

**v Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba**

Katika usimamizi wa manunuzi na mikataba, tunapenda kutambua juhudi zilizochukuliwa na Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) katika mpango wa kujenga uwezo ambao umewezesha Mashirika kufikia kiwango kikubwa cha

kutekeleza Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Hata hivyo, baadhi ya Mashirika ya Umma bado hayafuati kikamilifu matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma katika kupitisha zabuni, uundaji na utendaji kazi wa vitengo vya manunuzi, uteuzi wa kamati za kufanya tathmini na kamati za uhakiki na kukubali mali. Migongano ya kimaslahi katika taratibu za manunuzi na pia udhaifu katika usimamizi wa mikataba bado ni tatizo kubwa.

**vi Kuchelewa kwa Utekelezaji wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa**

Baraza la Mawaziri liliidhinisha mpango wa kutekeleza mradi mwaka 2007, ambapo mradi ulipangwa kuanza mwezi Julai 2008 hadi Disemba 2009. Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Mambo ya Ndani iliidhinisha zabuni kwa ajili ya kazi hii tarehe 20 Septemba, 2008 baada ya hapo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilisaini mkataba na Mshauri Gotham International Limited tarehe 13 Januari, 2010 kutoa huduma ya Ushauri wa menejimenti kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa vitambulisho vya Taifa kwa kutumia tekinolojia ya SMART CARD. Jumla ya gharama za mkataba ni dola za kimarekani milioni 9 na muda wa mkataba ni miaka mitano (5) kuanzia tarehe 14 Januari, 2010.

Mradi umechukua muda wa mwaka mmoja tangu tarehe ambayo Bodi ya Zabuni ya Wizara itoe idhini kwa ajili ya kazi ya ushauri na kusainiwa kwa mkataba. Ucheleweshwaji huu una athari katika kufikia na kutimiza malengo ya shughuli za mradi. Ninashauri kwamba menejimenti ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iongeze juhudi katika kuongeza kasi ya Mradi wa Vitambulisho vya Taifa kwa manufaa ya Taifa.

**vii Usimamizi wa Raslimali**

Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yanakopesha baadhi ya makampuni ambayo yanashindwa kurejesha fedha zilizokopa. Aina hizi za ukopeshaji umeonekana kuwa ni matumizi mabaya ya pesa za umma



ambazo zingeweza kutumika kwa shughuli nyingine za maendeleo. Tatizo kubwa ni kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa mali zisizohamishika. Tatizo lingine ni lile la kutoweza kutafsiri na utekelezaji wa Viwango vya Kihasiibu vya Kimataifa kuhusu sera za kutoza uchakavu wa Mali zisizohamishika katika baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma. Aya ya 33 ya Kiwango cha Kimataifa Na. 8 kinataka kufanya makadirio ambayo ni ya uhakika na yanayoaminika. Tunashauri Msajili wa Hazina kufanya utafiti kuhusu viwango vya kutoza uchakavu ili kutoa mwongozo unaostahili. Masuala haya yameainishwa zaidi katika sura ya saba.

**viii Usimamizi wa Raslimali Watu**

Raslimali watu ni injini ya raslimali nyingine na hivyo inahitaji uangalizi wa kipekee. Katika Usimamizi wa Raslimali watu tulibaini udhaifu wa kutorekebishwa kwa taarifa za wafanyakazi, kukosekana kwa mikataba ya ajira kwa baadhi ya wafanyakazi, kuajiri bila kufuata taratibu za ajira katika utumishi wa umma, kutokuwepo mafunzo kwa wafanyakazi, udhaifu katika upimaji kazi watumishi, ucheleweshwaji wa michango ya pensheni kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Maelezo zaidi juu ya usimamizi wa raslimali watu yanapatikana katika sura ya nane ya taarifa hii.

**ix Utawala Bora**

Utawala bora ni changamoto inayoathiri ufanisi wa utendaji kazi katika Mashirika na Taasisi za Umma. Ukosefu wa Bodi za Wakurugenzi zenye mamlaka thabiti na ukosefu wa mgawanyo wa madaraka ulio wazi kati ya Serikali, Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mashirika ya Umma umeathiri kwa kiasi kikubwa katika kufikia malengo ya Mashirika na Taasisi za Umma. Pamoja na matukio ya hivi karibuni yaliyoyakumba mashirika ya umma kama vile NCAA na CTB ambayo yameshindwa kutekeleza kanuni za utawala bora, serikali imewekeza juhudi ndogo katika utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi tuliyoyatoa juu ya mifumo ya utawala bora. Ni wakati muafaka sasa kwa Bunge, Serikali,

Bodi za Wakurugenzi, Menejimenti za Mashirika na Taasisi za Umma kuhakikisha mapendekezo hayo yanatekelezwa. Bunge linashauriwa kutunga sheria na kanuni ambazo zitayabana Mashirika na Taasisi za Umma kufuata kanuni za utawala bora. Haya yameelezwa zaidi katika sura ya tisa ya taarifa hii.

- x Mgongano wa Kimaslahi kwa Wabunge kuwa Wajumbe Katika Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma  
Kama ilivyopendekezwa katika ripoti zilizopita na kwa kuwa Bunge ni chombo cha juu cha uwakilishi wa watu chenye majukumu ya kuangalia utendaji wa Mashirika ya Umma kupitia POAC na ili kuondoa migongano ya kimaslahi, wabunge hawapaswi kuwa wajumbe katika Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma. Waheshimiwa Wabunge kuwa kwenye Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi za Serikali, ni kinyume na desturi nzuri na ni kinyume na kanuni za utawala bora. Utaratibu huu hautumiki katika nchi yoyote ambayo ni mwanachama wa Mashirikisho kama vile EAC, SADCOPAC, SADC, AFROSAI-E na AU.
- xi Bodi za Wakurugenzi Kuingilia Kazi za Menejimenti  
Bodi za Wakurugenzi kuingilia kazi za menejimenti katika mashirika ni kinyume na utaratibu wa utawala bora unaoitaka Bodi kuwa kama jicho la kuangalia shughuli na utendaji wa menejimenti. Kazi za Bodi; ni kutunga sera zitakazoongoza Shirika, kuandaa mipango, kutengeneza Muundo wa Shirika na kuhakikisha kuwa Shirika lipo imara kifedha. Mgongano wa kimaslahi kati ya Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma kwa kiasi kikubwa hupunguza motisha kwa menejimenti katika kutimiza malengo yaliyojiwekea na majukumu ya kiutendaji. Hali hii inaweza kupelekea kutofikiwa kwa malengo ya mashirika.
- xii Kutokufuata Waraka na Taratibu za Serikali ya Kulipa Ada na Marupurupu Mengine ya Wakurugenzi wa Bodi

Chini ya utawala bora, ada za Wakurugenzi wa Bodi ya Shirika hupangwa na wadau kwa upande wa Mashirika ya Umma mdau ni Msajili wa Hazina kwa niaba ya Serikali. Zaidi ya hayo, ada za wakurugenzi hazitakiwi kupangwa kutokana na uzalishaji wa mashirika kwa sababu inaweza kupelekea utengenezaji wa hesabu kwa mbinu ili zionyeshe uwepo wa faida usio sahihi. Kudhibiti ada za Wakurugenzi kutaleta uhalali, uhalisia na usawa katika menejimenti za Mashirika ya Umma. Upangaji wa ada za Wakurugenzi na mafao yao isiachwe moja kwa moja kwenye mikono ya Bodi za Wakurugenzi wenyewe kama ilivyoonekana kwenye baadhi ya Mashirika ya Umma. Bodi za Wakurugenzi ni chombo ambacho kinatakiwa kuwa na mtizamo wa kuongeza mapato na kupunguza matumizi ya Shirika na siyo vinginevyo.

#### xiii Kutokufuata Waraka wa Msajili wa Hazina

Wizara ya Fedha ilitoa waraka wa Msajili wa Hazina Na.8 unaoyataka Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kuchangia asilimia 10 ya mapato kabla ya matumizi yatokanayo na shughuli za uzalishaji wa shirika kwenda Hazina. Baadhi ya Mashirika hayakufuata waraka huu. Hali hii ilionekana katika mashirika mawili ambapo shirika moja kupitia kikao chake cha Bodi ya Wakurugenzi kiliamua kuwa mchango wa Hazina uwe asilimia 10 ya faida iliyopatikana baada ya matumizi na si mapato kabla ya matumizi ambapo ni kinyume na waraka uliotolewa na Msajili wa Hazina.

#### xiv Utendaji wa Mashirika Yaliyobinafsishwa

Kulingana na taarifa ya Msajili wa Hazina ya tarehe 30 Juni, 2010, madeni yaliyopo kama dhamana zilizotolewa na Serikali zilikuwa za jumla ya shilingi bilioni 451, Mapato yaliyokusanywa na Msajili wa Hazina kama gawiwo, malipo ya mikopo na mapato mengineyo yalipungua kwa shilingi bilioni 42.5 kutoka shilingi bilioni 84.1 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2009 mpaka kufikia shilingi bilioni 40.6 katika mwaka huu wa ukaguzi. Salio la mikopo iliyobaki lilipungua kwa billion 21 kutoka shilingi bilioni 478 mwaka 2009 hadi kufikia shilingi bilioni 456.8 mwaka 2010. Vitega

uchumi vya ndani vya Serikali viliongezeka kwa shilingi trilioni 1.6 ikiwa ni ongezeko kutoka shilingi trilioni 6.1 kutoka tarehe 30 Juni, 2009 hadi kufikia shilingi trilioni 7.7 katika mwaka huu wa ukaguzi. Uwekezaji wa kigeni ulipungua kwa shilingi bilioni 27 kutoka shilingi bilioni 140.5 tarehe 30 Juni, 2009 hadi kufikia shilingi bilioni 113.6 mwishoni mwa mwaka huu wa ukaguzi. Maelezo zaidi kuhusu utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma yanayomilikiwa na Serikali na yaliyobinafsishwa yameelezwa katika sura ya kumi ya taarifa hii.

**xv Mitaji Midogo katika Mashirika ya Umma**

Mitaji midogo katika Mashirika na Taasisi za Umma, imekuwa ni tatizo sugu katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, ambayo ina idadi kubwa ya Mashirika ambayo hayafanyi kazi kwa ufanisi na faida kutokana na kukosa mtaji. Kuna haja ya Serikali kuingilia kati na kutatua tatizo hili linaloyakumba Mashirika na Taasisi za Umma kwa kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ili kuongeza mtaji kwenye Mashirika na Taasisi hizi za Umma ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi ili yaweze kujiendesha kwa ufanisi na kwa hali hiyo yataboresha utoaji wa huduma kwa umma.

**xvi Mashirika Yaliyotengwa kwa Ajili ya Kubinafsishwa**

Mashirika ya umma 34 yaliyotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa na Serikali na yalichukuliwa kutoka Tume ya Rais ya Ubinafsishaji wa Sekta za Umma (PSRC) na kuwekwa chini ya Shirika Hodhi la Mali za Makampuni Yaliyobinafsishwa (CHC), bado yametengwa kwa ajili ya mpango wa ubinafsishwaji mpaka wakati huu tunaandika ripoti hii. Itambulike kwamba, Mashirika yanayotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa, yanakuwa hayawezi kukopa wala kutekeleza mipango ya muda mrefu ya maendeleo. Pia, wafanyakazi wa mashirika haya wanakuwa hawana motisha wa kufanya kazi au kutimiza wajibu wao kwa kujituma kwa sababu ya kutokujua hatima ya ajira zao na ya mwajiri wao. Uchakavu wa mali na raslimali za mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa ni wa hali ya juu

kutokana na kwamba ukarabati au ubadilishaji wa mali zilizoharibika unakuwa mgumu kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Serikali inapaswa kuongeza kasi ya taratibu za ubinafsishaji wa mashirika haya 34 yaliyotengwa kwa ajili ya ubinafsishaji katika kuhakikisha kuwa raslimali za mashirika hayo haziendelei kuchakaa au kufuta mpango wa ubinafsishaji wa mashirika hayo na kuyapatia mtaji wa kutosha ili yaweze kujiendesha kama ilivyokuwa hapo awali.

#### xvii Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Mashirika na Taasisi za Umma zimekuwa zikiwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye teknolojia ya mawasiliano na habari katika kuhakikisha yanakwenda na wakati na kuongeza kiwango cha ufanisi. Upembuzi wa mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano umebaini mashirika mengi ya umma hayana kamati za uendeshaji wa TEKNOHAMA, mikakati ya TEKNOHAMA, uwekaji kumbukumbu wa taratibu za TEKNOHAMA, Sera za TEKNOHAMA na Mifumo na taratibu za kurudisha taarifa zilizopotea. Pia, baadhi ya Mashirika ya Umma bado hayajawekeza kwenye mifumo ya kompyuta ya kijasibu. Hali hii huyaweka Mashirika hayo katika hatari ya kushindwa kurejesha taarifa muhimu panapotokea maafa. Maelekezo zaidi yapo katika sura ya kumi na moja ya ripoti hii.

#### xviii Ukaguzi Maalumu

Katika mwaka huu wa ukaguzi tulifanya ukaguzi maalum mmoja juu ya vitendo vya ubadhirifu katika Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC). Tulibaini kuwa hapakuwa na hati ya mabadiliko iliyotolewa inayoelezea kazi za nyongeza au mabadiliko ya bei katika kuthibitisha malipo ya ziada ya shilingi milioni 24 kwa ajili ya kutambua na kurekodi mali za NDC kutoka kwa mzabuni. Zaidi ya hayo hundi zenye namba 806118 na 806113 zenye kiasi cha shilingi milioni 12 na shilingi milioni 23 kwa mpangilio huo zililipwa kama

fedha taslimu na afisa mwandamizi wa NDC tarehe 26.02.2010.

Tunapenda kuripoti pia kuwa vitendo hivi vya ubadhirifu viliripotiwa kwa menejimenti ya shirika na baadae kuripotiwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi ambapo hatua zimechukuliwa dhidi ya wafanyakazi waliohusika ikiwa ni pamoja na kufungua mashtaka mahakamani.

**xix Hitimisho**

Ili ukaguzi uweze kuonekana umeongeza tija katika ufanisi wa utendaji kazi katika Mashirika na Taasisi za Umma, utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ni wa muhimu sana. Bunge, Serikali, Bodi za Wakurugenzi, Maafisa Wakuu Watendaji na Menejimenti za Mashirika na Taasisi za Umma kwa ujumla wanapaswa kuhakikisha utekelezaji wa mapendekezo haya bila kuchelewa zaidi. Kwa hiyo, ni muhimu kwa kila anayehusika akachukua hatua madhubuti katika kushughulikia kasoro zilizoonekana. Kwa kufanya hivyo ufanisi katika utendaji kazi wa Mashirika na Taasisi za Umma utaongezeka.

## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI NA TAARIFA ZA JUMLA

- 1.0 Uanzishwaji wa Kazi ya Ukaguzi Kisheria  
Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ofisi iliyopo Kikatiba iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (ilivyorekebishwa mwaka 2005) kama ilivyofafanuliwa kwenye Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 na Sehemu 44 (2) ya Sheria ya Manunuzi Na.21 ya 2004.

Ibara 143 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Mashirika ya Umma angalau mara moja kwa kila mwaka wa fedha. Vilevile, sehemu ya 33 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 inampa Mamlaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kumruhusu mtu yeyote ambaye anaweza kuchaguliwa kuwa Mkaguzi wa Shirika ama Afisa yeyote kukagua kwa niaba yake vitabu vya hesabu vya Shirika la Umma au Taasisi za Serikali yeyote ambaye Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu anapaswa kukagua kwa mujibu wa Sheria.

Katika kuelewa miongozo ya kisheria inayoongoza kaguzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Umma, ni vizuri kuelewa pia Mashirika mengi yanafuata viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu au Viwango vya Kimataifa vya Kuandaa Taarifa za Hesabu za Umma. Kwa hali hiyo, miongozo ya kisheria inayotumika kuandaa mahesabu na kaguzi ni ama Sheria ya Makampuni Na. 12 ya mwaka 2002 ama sheria yeyote iliyopitishwa na Bunge inayohusu shirika husika.

## 1.1 Mamlaka ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu ya Ukaguzi na Kutoa Taarifa

1.1.1 Mamlaka ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu ya Kutoa Taarifa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) inamtaka Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwasilisha taarifa ya mwaka ya Ukaguzi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ifikapo tarehe 31 Machi ya kila Mwaka. Baada ya kupokea taarifa atawaelekeza maofisa wanaohusika kuwasilisha taarifa hizo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge ambacho kitafanyika baada ya Rais kupokea taarifa hizo na lazima taarifa hii iwasilishwe ndani ya siku saba tangu kikao hicho cha Bunge kilipoanza. Kama Rais hatachukua hatua zozote za kuwasilisha taarifa hizo bungeni, Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha nakala ya taarifa kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (au Naibu Spika ikiwa kiti cha Spika kiko wazi wakati huo au ikiwa kwa sababu yoyote Spika hawezi kutekeleza majukumu yake) ambaye atawasilisha taarifa hizo Bungeni. Kimsingi taarifa ya Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali hujadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma.

### 1.1.2 Mamlaka ya Kufanya Ukaguzi

Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa mamlaka ya kufanya ukaguzi wa hesabu na ukaguzi wa thamani ya fedha wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kulingana na Sehemu ya 30 na 32 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008. Sehemu ya 12 ya Sheria hiyo inampa mamlaka Mdhibili na Mkaguzi Mkuu kutoa mapendekezo kwa nia ya:-

- Kuzuia na kupunguza matumizi ya fedha za Umma yasiyokuwa na tija,
- Kuongeza makusanyo ya maduhuli ya umma,



- Kuzuia hasara inayoweza kutokea kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu udanganyifu au rushwa kuhusiana na fedha na raslimali za umma.

## 1.2 Wigo na Matumizi ya Viwango Katika Kuandaa Hesabu

### 1.2.1 Wigo wa Ukaguzi

Tunapozungumzia wigo wa ukaguzi tunamaana maeneo ambayo yatakaguliwa. Wigo wa ukaguzi unajumuisha, nia ya ukaguzi, aina ya ukaguzi na mbinu za kukagua zilizotumika na muda uliotumika kwenye ukaguzi. Nia na madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kutimiza jukumu la kutoa maoni huru kwenye mahesabu ya Mashirika ya Umma yanayoishia tarehe 30 Septemba 2009, tarehe 31 Disemba 2009 na tarehe 30 Juni 2010. Pia inajumuisha hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa kaguzi za miaka iliyopita ambayo hayajafanyiwa kazi.

Ukaguzi unahusu pia tathmini ya ufanisi wa mifumo ya kiuhasibu na ubora wa vidhibiti vya ndani vinavyodhibiti shughuli, ukaguzi na uhakiki wa ubora wa hesabu, taarifa za utendaji kazi na mbinu nyingine za kiukaguzi zinazoonekana ni muhimu katika kutoa maoni ya ukaguzi. Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia athari na ukubwa wa athari, kwa hiyo, hoja za ukaguzi zilitokana na kumbumkumbu, nyaraka na taarifa zilizokuwa zimeombwa na kupatiwa wakaguzi.

### 1.2.2 Viwango vya Kimataifa Vilivyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni mwanachama katika Shirikisho la Kimataifa la Ukaguzi (INTOSAI), (AFROSAI-E) na Jumua nyingine za Kimataifa katika taaluma ya ukaguzi. Hivyo, tunatumia viwango vilivyotolewa na INTOSAI, Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC). Hivyo, wakati wa kufanya kaguzi zetu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina jukumu la pekee la kuhakikisha kunakuwepo na nidhamu katika matumizi ya raslimali za Umma, uwajibikaji na uwazi katika Jamhuri ya

Muungano ya Tanzania. Pia, ofisi kwa mujibu wa sheria ina jukumu la kutoa ripoti iliyo bora na kwa wakati inayoelezea namna raslimali za Taifa zilivyotumika.

- 1.3 **Majukumu ya Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu**  
Jukumu la kutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu kwa madhumuni ya ukaguzi ni la Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi husika. Tunapenda ieleweke kuwa uandaaji wa hesabu unatakiwa ufanywe kiasi ambacho suala la mgongano wa kimaslahi halitakuwepo kwani mtu hawezi kusimamia na kukosoa barabara hesabu ambazo yeye mwenyewe anahusika kuziandaa. Vilevile kuhusu suala la mgongano wa kimaslahi pia ni muhimu ikaeleweka kuwa linajitokeza pale ambapo Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma wanapokuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika na Taasisi za Umma ambazo watapaswa kusimamia shughuli zake.

Kiwango Na. 1 cha Kimataifa cha Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu na Kiwango Na.1 cha Kimataifa cha Uhasibu vinaelezea aina za taarifa za fedha zinazotakiwa kutayarishwa. Mashirika na Taasisi za Umma hapa nchini zinatakiwa kutayarisha hesabu zao kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS) au viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) kulingana na muundo wa majukumu ya Mashirika ya Umma na Taasisi husika. Hii ni kutokana na uamuzi uliofanywa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) na kuungwa mkono na Serikali kuwa kuanzia Julai 2004 Mashirika ya Umma na Taasisi za Umma Tanzania yalitakiwa kutengeneza hesabu zake kulingana na viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IFRS) na ukaguzi utafuata viwango vya ukaguzi vya kimataifa (ISA), na Sheria zinazotolewa mara kwa mara na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Uandaaji na uwasilishaji wa hesabu za Mashirika na Taasisi za Umma ni jukumu la kisheria lililoainishwa kwenye Sheria zilizoanzisha Mashirika na Taasisi za Umma husika, Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002 na Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Ripoti za mwaka za Mashirika na Taasisi za Umma zinawapatia wananchi taarifa ambazo zinawawezesha kupima ufanisi wa utendaji kazi wa Mashirika hayo na kuona yanawajibika ipasavyo katika kutumia raslimali za Umma. Hesabu zinazowasilishwa kwa wakati zinawezesha uandaaji wa ripoti hii kwa wakati.

#### 1.4 Mifumo ya Udhibiti ya Ndani

Mifumo ya udhibiti ya ndani maana yake ni namna ambayo Mashirika ya Umma yanapangilia mifumo yake katika kuhakikisha kuwa raslimali za Umma zinatumiwa ipasavyo. Mifumo wa ndani unatumika kama chombo muhimu katika kudhibiti ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali za umma. Katika ngazi ya Taasisi, udhibiti wa ndani unahakikisha uwepo wa taarifa za fedha za kuaminika, kupata taarifa kwa wakati kuhusu mafanikio ya malengo iliyojiwekea, na kuhakikisha sheria na kanuni zinafuatwa. Katika ngazi fulani ya utekelezaji wa shughuli za Taasisi, vidhibiti vya ndani ni hatua inayochukuliwa katika kuhakikisha lengo husika kwa mfano kuhakikisha malipo yanafanywa kwa wazabuni na watoa huduma wa mali na kulingana na huduma halisi iliyotolewa.

Jukumu la kuangalia kama vidhibiti vya ndani vinafuatwa ni la Mkaguzi wa Ndani wa shirika husika. Udhaifu katika utendaji kazi wa vitengo vya ukaguzi vya ndani, ni sawa na udhaifu katika kuhakikisha vidhibiti vya ndani vinafanya kazi ipasavyo.

#### 1.5 Majukumu ya Msajili wa Hazina

Kulingana na Sheria ya Msajili wa Hazina kifungu Na. 6 cha Sheria ya Mashirika ya Umma Na.16 ya mwaka 1992, kuhusu shughuli za Mashirika ya Umma, inaeleza kwamba Msajili

wa Hazina ana kazi na majukumu ya kusimamia vyema uendeshaji wa shughuli za Mashirika na Taasisi za Umma kwa kushirikiana na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika husika.

#### **1.6 Mpangilio wa Ripoti Hii**

Ripoti hii inaelekeza kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi uliofanywa katika Mashirika na Taasisi za Serikali kwa kipindi husika. Ili kutimiza malengo na kazi zangu kikatiba, niliamua kushirikiana na makampuni binafsi ya ukaguzi katika kufanya kazi ya ukaguzi. Katika kutekeleza wajibu huu, tulifanya kazi hizo kwa kushirikiana, au kwa kuziachia kampuni binafsi zenyewe kufanya ukaguzi chini ya usimamizi wa ofisi yangu. Kazi za ukaguzi zilizofanywa na makampuni binafsi kwa niaba yangu ziliwasilishwa kwenye ofisi yangu ili kuhakikiwa ubora wake kabla ya kusainiwa kwa hati ya ukaguzi.

Katika mwaka husika, ofisi yangu ilifanya kazi kwa pamoja na kampuni binafsi za ukaguzi 47 ambazo ziliomba kufanya kazi na ofisi yangu kwa mwaka husika na ambazo zimesajiliwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) kama CPA-PP. Majina ya Kampuni binafsi zilizofanya kazi kwa niaba yangu ni kama inavyoonyeshwa kwenye Kiambatanisho 1 cha ripoti hii.

#### **1.7 Kuwasilisha Hesabu kwa Ajili ya Ukaguzi**

Kifungu 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya Mwaka 2008, kinawataka Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma kutayarisha hesabu katika kipindi cha miezi mitatu baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha na kuziwasilisha kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

#### **1.8 Uteuzi wa Makampuni Binafsi ya Ukaguzi**

Kifungu Na.33 (5) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka, 2008 inampa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mamlaka ya kumruhusu mtu au kampuni yoyote iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Wakaguzi wa Hesabu na Wahasibu Na.33 ya mwaka 1972 (iliyorekebisha mwaka


1995) kufanya ukaguzi kwa niaba yake na kumuwezesha kupeleka ripoti kwa wakati Bungeni. Wakaguzi watakaoteuliwa watafuata Sheria kama inavyotakiwa na hawatakuwa na mgongano wa kimaslahi katika kutekeleza wajibu wao. Wajibu wa kutoa hati ya ukaguzi ni wa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwenyewe. Katika mwaka husika ukaguzi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali 122 ulikamilika na kaguzi zake zilifanyika kama ifuatavyo:

#### Jedwali 1: Mgawanyo wa Kaguzi za Mashirika ya Umma

Na	Maelezo	Mashirika	Asilimia
1.	Mashirika yalivyokaguliwa na Ofisi yangu	11	9.0
2.	Mashirika yaliyokaguliwa kwa kushirikiana na Makampuni Binasfi ya Ukaguzi	13	10.7
3.	Mashirika yaliyokaguliwa na kampuni binafsi kwa niaba yangu chini ya usimamizi wa Ofisi yangu	98	80.3
	<b>Jumla</b>	<b>122</b>	<b>100</b>

Taarifa hiyo hapo juu inaonyeshwa kwenye kielelezo Kifuatacho:-

#### Kielelezo 1: Mgawanyo wa Kaguzi za Mashirika ya Umma



Idadi ndogo ya Mashirika ya Umma yaani asilimia 9 yaliyokaguliwa na ofisi yangu ni ishara ya upungufu mkubwa wa wafanyakazi wa kutosha na wenye sifa stahili katika ofisi yangu. Ofisi yangu inahitaji wafanyakazi wengi na wenye ujuzi ili iweze kupambana na changamoto mbalimbali inazokumbana nazo.

Majina ya makampuni binafsi ya ukaguzi yaliyotumiwa na ofisi yangu yameorodheshwa kwenye kiambatanisho Na.1 cha taarifa hii.

## SURA YA PILI

### AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

#### 2.0 Utangulizi

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi kuhusu hesabu zilizokaguliwa kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango vinavyokubalika vya uhasibu kwa kuzingatia sera za uhasibu na kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazokubalika.

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi, dhumuni la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumuwezesha mkaguzi kutoa maoni huru ya ukaguzi yanayoeleza iwapo hesabu zimeandaliwa kwa usahihi na kwa kufuata viwango vinavyokubalika. Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea mtumiaji wa taarifa za hesabu na taarifa zinazoambatana nazo kuziamini taarifa hizo. Lengo la kufanya ukaguzi ni kupata sababu za uhakika ya kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa makubwa yanayotokana na wizi ama makosa ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

Ukaguzi wa taarifa za hesabu za sekta ya umma hapa nchini ni kwa mujibu wa matakwa ya sheria ambayo yameelezwa na Ibara 143 (2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyofafanuliwa na sehemu ya 34 (1) ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008 ambayo inaeleza kuwa “baada ya kupokea taarifa za hesabu kwa mujibu wa sheria, Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu atakagua hesabu hizo ndani ya miezi tisa baaada ya tarehe ya mwisho ya mwaka wa hesabu husika na kutoa maoni ya ukaguzi kwa kila hesabu na matokeo ya ukaguzi.”

#### 2.1 Aina za Hati za Kaguzi

##### 2.1.1 Hati Inayoridhisha

Hati inayoridhisha inajulikana pia kama hati safi. Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu

zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika vya kuandaa hesabu na zinaonyesha hali halisi ya shirika.

#### 2.1.2 Hati Inayoridhisha Yenye Masuala ya Msisitizo

Hati inayoridhisha yenye masuala ya Msisitizo inatolewa pale ambapo mkaguzi anapoona hati inayoridhisha haiwezi ikatolewa. Taarifa ya Mkaguzi inaweza kurekebisha kwa kuongeza aya ya masuala ya msisitizo inayoelezea kwa kifupi mambo yanayoathiri taarifa za fedha ambayo yemelezewa kwa kina kwenye hesabu. Kuongeza aya ya masuala ya msisitizo haibadilishi hati ya ukaguzi. Mkaguzi anaweza kurekebisha hati ya ukaguzi kwa kutumia masuala ya msisitizo kutoa taarifa ya mambo mengine zaidi ya yale yanayoathiri taarifa za hesabu.

#### 2.1.3 Hati yenye Kasoro

Hati yenye kasoro hutolewa pale ambapo mkaguzi anabaini makosa ambayo yana athari kwenye taarifa za hesabu na mkaguzi anaona kuwa hati inayoridhisha haiwezi ikatolewa lakini kutokukubaliana na menejimenti au kushindwa kufanya ukaguzi sio kwa hali ya juu ambako kungepelekea kutolewa kwa hati mbaya au kutokutolewa kwa hati ya ukaguzi.

#### 2.1.4 Hati Yenye Kasoro na Yenye Masuala ya Msisitizo

Hati yenye kasoro na yenye masuala ya msisitizo hutolewa pale ambapo mkaguzi anaona hati inayoridhisha haiwezi ikatolewa lakini athari zozote za kutokukubaliana na menejimenti au kukwamishwa kufanya ukaguzi sio kwa athari kubwa ambako kungepelekea hati mbaya au mkaguzi kushindwa kutoa hati ya ukaguzi. Aya ya masuala ya msisitizo haibadilishi hati ya ukaguzi kwa kutoa taarifa ya mambo mengine zaidi ya yale yanayoathiri taarifa za hesabu.

#### 2.1.5 Mkaguzi Kushindwa Kutoa Maoni

Hati hii ya ukaguzi hutolewa pale ambapo athari ya mkaguzi kushindwa kufanya ukaguzi ni kubwa na kwamba



mkaguzi alishindwa kupata ushahidi wa kutosha na hali hiyo kumpelekea kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kwenye taarifa za hesabu.

#### 2.1.6 Hati Mbaya

Hati mbaya hutolewa pale ambapo athari za kutokukubaliana na menejimenti ni kubwa na kwamba taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zina makosa makubwa na mkaguzi kuona kuwa kutoa hati yenye kasoro haitoshi kuonyesha hali halisi ya kutokukamilika kwa taarifa za hesabu.

#### 2.2 Hali Halisi ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma

Ripoti hii ya jumla itajadili ripoti 170 za Mashirika ya Umma ikilinganishwa na ripoti 166 zilizoripotiwa kwenye ripoti ya jumla ya mwaka 2008/2009.

Hii inatokana na kujumuishwa kwa mashirika manne ambayo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Usafiri Majini na Nchi Kavu (SUMATRA ccc), Chuo Cha Teknologia cha Arusha (AIT) na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama kwenye orodha ya Mashirika yanayokaguliwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2010, Maafisa Watendaji Wakuu wa mashirika 167 waliwasilisha hesabu zao kwenye ofisi yangu kwa ajili ya kukaguliwa. Kaguzi 122 zilihitimishwa ambapo kaguzi 103 zilipitishwa na Bodi za Wakurugenzi, kaguzi 19 zilikuwa zinasubiri kupitishwa na bodi za wakurugenzi, kaguzi 15 zipo katika hatua ya uhakiki wa ubora, kaguzi 30 zinaendelea na ukaguzi wa mashirika 3 hayajafanywa kabisa kwa kuwa ofisi yangu haijapokea hesabu za Mashirika haya kwa ajili ya ukaguzi. Mashirika matatu (3) ambayo hayajawasilisha hesabu zao kwa ajili ya ukaguzi ni Kampuni ya Maendeleo ya Uwanja wa Ndehe Kilimanjaro, Kiwanda cha Matairi cha Afrika Mashariki, na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Korogwe

Kwa kifupi,taarifa hii inaonyeshwa kwenye jedwali kama ifuatavyo:

## Jedwali 2: Kuwasilisha Hesabu

Na	Kundi la Shirika	Idadi ya Mashirika Niliyo Paswa Kukagua	Ripoti Zilizokamilika		Kaguzi Zilizochini ya Uhakiki wa Ubora	Kaguzi Zinazoe-ndelea	Hesabu Ambazo Hazijawasilishwa
			Repoti Zilizopitishwa na Bodi	Ripoti Zinazo-subiri Kupitishwa Na Bodi			
1.	Taasisi za Fedha, Mifuko ya Pensheni na Kampuni za Bima.	16	14	1	-	1	-
2.	Taasisi za Uzalishaji.	18	9	4	3	-	2
3.	Bodi za Udhibiti, Mabaraza, Kamisheni Na Mamlaka	56	33	10	5	8	-
4.	Vyuo vya Elimu ya Juu, Tafiti, Mafunzo.	36	20	1	3	12	-
5.	Mashirika ya Kutoa Huduma.	44	27	3	4	9	1
Jumla		170	103	19	15	30	3
			122				

Hali halisi ya ukaguzi wa Mashirika ya Umma kufikia tarehe 25 Februari 2011 imeonyeshwa kwenye Kiambatanisho namba III cha ripoti hii.

- 2.3 **Hati zilizotolewa kwa Mashirika ya Umma**  
Kufikia tarehe 25 Februari, 2011 nimefanikiwa kuhitimisha kaguzi 122 (71.7%) kati ya kaguzi 170 zinazotakiwa kukakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika kaguzi zilizokamilika, kaguzi 92 (75.4%) za Mashirika ya Umma zilipata hati inayoridhisha, kaguzi 12 (9.8%) zilipata hati safi zenye masuala ya msisitizo, kaguzi 10 (8.2%) zilipata hati zenye kasoro na kaguzi 7 (5.8%) zilipata hati zenye kasoro zenye masuala ya msisitizo wakati nilishindwa kutoa maoni ya ukaguzi kwa shirika 1


(0.8%). Katika mwaka huu wa ukaguzi hakuna shirika lililopata hati mbaya. Maelezo ya kina ya hati za ukaguzi yameonyeshwa katika kiambatisho II cha ripoti hii.

**Jedwali 3: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi**

Mashirika	Hati Safi	Hati safi Yenye Masuala Msisitizo	Hati Zenye Kasoro	Hati Yenye Kasoro Zenye Msisitizo	Kushindwa Kutoa Hati
122	92	12	10	7	1
100%	75.4%	9.8%	8.2%	5.8%	0.8%

Mchanganuo huo hapo juu unaweza ukaonyeshwa kwenye pai chati kama ilivyoonyeshwa hapo chini:

**Kielelezo 2: Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mashirika**





## SURA YA TATU

### MUHTASARI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI WA MWAKA ULIOPITA AMBAYO HAYAJATEKELEZWA

#### 3.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza kwa muhtasari mapendekezo ambayo hayajatekelezwa yaliyotolewa katika ripoti za jumla za kaguzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali za miaka iliyopita. Mpaka namaliza kuandika ripoti ya jumla ya mwaka huu mapendekezo mengi yalikuwa hayajatekelezwa kikamilifu huku mengine yakiwa hayajatekelezwa kabisa au yametekelezwa kwa kiasi fulani tu. Mapendekezo haya yanahitaji angalizo na kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma.

#### 3.1 Majibu ya Ripoti ya Mwaka Uliopita

Nimepokea majibu ya Serikali juu ya ripoti zangu za miaka iliyopita kupitia kwa Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa barua yenye Kumbukumbu Na.EB/AG/392/04/11/VOL.VII/13 ya tarehe 27 Julai, 2010. Hata hivyo, kuna mapendekezo ambayo hayajatekelezwa, ambayo yanahitaji angalizo zaidi na kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma kwa miaka iliyoishia tarehe 30 Juni, 2008 na 30 June, 2009.

Katika ripoti ya mwaka ulioishia tarehe 30 June, 2008 jumla ya mapendekezo 15 yalikuwa yametolewa. Hadi kufikia tarehe ya kuandika ripoti hii mapendekezo yote 15 yalikuwa hayajatekelezwa ipasavyo.

Mapendekezo ambayo yanasubiri utekelezaji wa Serikali, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika husika ni kama ifuatavyo:-

## Jedwali 4: Mapendekezo Ambayo Hayakutekelezwa 2007/2008

Na.	Mapendekezo
1.	Menejimenti ya Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania linapaswa kutoa maelezo ya uhalali wa malipo ya Dola za Kimarekani 4,865,000 zilizolipwa kwa M/s Dowans kwa ajili ya kukodisha ndege maalumu.
2.	Mhajili wa Hazina anapaswa kuhakikisha kuwa Mashirika ambayo hayana mtaji wa kutosha, yanapatiwa fedha kwa ajili ya kujiendesha.
3.	Serikali inatakiwa kuanzisha Mamlaka itakayokuwa na majukumu ya kudhibiti utendaji na shughuli za Mashirika ya Umma
4.	Mhajili wa Hazina anapaswa kuchukua majukumu zaidi ya kusimamia uendeshaji wa shughuli za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali.
5.	Utawala Bora: Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapaswa kufikiria kupanua majukumu ya Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma (POAC) katika kuhakikisha kuwa Kamati ina utaratibu wa kusimamia hesabu za Mashirika na makampuni yote ambayo Serikali ina hisa.
6.	Menejimenti ya Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO) linapaswa kuhakikisha kuwa linafua umeme kulingana na mpango nyongeza wa shirika.
7.	Serikali inapaswa kuingia mikataba ya kiutendaji na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na kuandaa malengo ambayo yatatakiwa kutekelezwa katika kipindi husika ambacho Bodi itakuwa madarakani. Kwa hali hiyo Bodi za Wakurugenzi nazo zitapaswa kuingia mikataba ya kiutendaji na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma ambayo pia watatakiwa kuingia mikataba ya kiutendaji na wasaidizi wao.
8.	Serikali inapaswa kuangalia uwezekano wa kuligawa mara mbili Shirika la Maendeleo ya Petroli la Tanzania (TPDC); ambapo shirika moja litashughulika na shughuli za kibiashara na la pili lishughulike na utoaji wa leseni, kufanya ukaguzi na kufanya kazi zaidi za udhibiti.
9.	Menejimenti ya Shirika la Maji Dar es Salaam (DAWASCO) inapaswa kuwekeza kwenye uchimbaji wa maji ardhini ili yatumike kwa eneo kubwa la Jiji la Dar es Salaam ambalo halina maji. Pia, Shirika lipitie upya viwango vya ankara za maji ili kuiwezesha DAWASCO kulipa gharama zake za uendeshaji.
10.	Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma zinapaswa kuhakikisha kuwa, watendaji wakuu wa Mashirika ya Umma wanawajibika zaidi kwa matokeo ya utendaji kazi zao. Bodi za Wakurugenzi zipewe mamlaka zaidi ya kuingia mikataba ya kiutendaji (performance contract) na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma baada ya kuainisha malengo ya mwaka ambayo watatakiwa kuyatekeleza. Kwa hali hiyo, kuna haja kuangalia uwezekano wa watendaji wakuu wa Mashirika ya Umma kuteuliwa na Bodi za wakurugenzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na wajibu wa kuteua wenye viti wa Bodi za Wakurugenzi hizo.
11.	Kwa vile Bunge ni chombo cha juu kinachowawakilisha wananchi na kinachosimamia utendaji wa kazi za Mashirika ya Umma kupitia Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC), na ili kuepuka mgongano wa kimaslahi, napendekeza kuwa wabunge wasiwe wajumbe wa bodi za wakurugenzi za Mashirika ya Umma kama ilivyoazimiwa kwenye mkutano wa uwajibikaji wa Mashirika ya Umma "Parastatals Accountability Conference" uliofanyika tarehe 23-24 Januari, 2009.

12.	Serikali inatakiwa kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali, kuziba mianya ya ukwepaji kulipa kodi hususani kwenye mafuta ya magari na mitambo, kupunguza misamaha ya kodi na kupanua wigo wa kodi.
13.	Serikali inapaswa kupunguza matumizi yasiyokuwa ya lazima kama vile ilivyoamua kupunguza manunuzi ya magari ya kifahari na kupunguza gharama za semina. Pia, matumizi ya kawaida yanaweza kusimamiwa vizuri zaidi ili mapato yanayokusanywa yatumike kwenye shughuli za maendeleo.
14.	Maliasili zetu zinatakiwa zisimamiwe vizuri ili kuhakikisha watanzania wananufaika na maliasili zao.
15.	Shirika la ndege la Tanzania (ATCL) linapaswa kuhakikisha kuwa uamuzi wowote utakaofanywa kutokana na mazungumzo yanayoendelea kuhusu ushirikiano wa pamoja (joint venture) uzingatie matakwa ya watumiaji wa ndege. Pia, Tanzania, bila kuchelewa inapaswa kuthibitisha kuridhia maamuzi ya YAMAUSSOUKRO kama ilivyopendekezwa na mkutano wa uwajibikaji uliofanyika tarehe 23-24 Januari 2009.

### 3.2 Majibu ya Mapendekezo ya Mwaka 2008/2009

Katika ripoti ya Ukaguzi wa Mashirika na Taasisi za Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2009 nilitoa mapendekezo 17 kwa ajili ya utekelezaji. Hata hivyo hadi wakati tunaandaa ripoti hii, mapendekezo 5 tu ndiyo yaliyopata majibu kutoka kwa Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali na mengine yapo kwenye hatua za utekelezaji.


Kwa muhtasari yafuatayo ni mapendekezo yaliyotolewa kwa kipindi cha miaka iliyoishia tarehe 30 Juni 2009 ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma ili kuwepo ufanisi zaidi katika mashirika husika.

#### Jedwali 5: Muhtasari wa Mapendekezo Ambayo Hayajatekelezwa

Na.	Hali Ilivyo	Idadi ya Mapendekezo	Asilimia %
1.	Yaliyotekelezwa	0	0
2.	Yaliyopo kwenye utekelezaji	5	29%
3.	Ambayo hayajatekelezwa	12	71%
Jumla		17	100%

Utekelezaji wa mapendekezo ya mwaka ulioishia 2008/2009 yanaweza kuonyeshwa katika chati kama ifuatavyo:-

### Kielelezo 3: Mapendekezo Yasiyotekelezwa



### Jedwali 6: Mapendekezo Ambayo Hayajatekelezwa 2008/2009

Na.	Mapendekezo	Maoni ya Ukaguzi
1.	<p>Haja ya Kuanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina Kuendana na Tamko la Sheria ya Msajili wa Hazina Cap.418</p> <p>Endapo utekelezaji wa tamko hilo halitawezekana, Serikali inapaswa kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi itakayokuwa na jukumu la kudhibiti, na kusimamia uendeshaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali 166 zenye hisa/mtaji ambao una jumla ya shilingi trilioni 6.1 katika kukuza uwajibikaji na uwazi katika kutoa huduma nzuri kwa Umma. Vinginevyo Serikali iwasilishe muswada Bungeni wa kuifuta Sheria ya Msajili wa Hazina - Cap 418.</p>	<p>Pendekezo lipo kwenye utekelezaji.</p>



2.	<p>Mgongano wa Maslahi ya Wabunge kutokana na kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Za Serikali</p> <p>Katika taarifa yangu ya mwaka uliopita na kutokana na Bunge kuwa ndicho chombo kikuu kinachowakilisha wananchi na chenye majukumu ya kutathmini utendaji kazi (oversight role) wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kupitia kwa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Mashirika ya Umma (POAC) si sahihi kwa Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma. Ili kuondoa mgongano wa kimaslahi, Wabunge hawapaswi kuwa wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali. Mwenendo huu ni wa kipekee kwa Tanzania na hautumiki mahali popote katika Jumuiya ambayo Tanzania ni mwanachama, kwa mfano EAC, SADCOPAC, SADC, AFROSAI-E, AU n.k</p>	Pendekezo halijatekelezwa.
3.	<p>Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu</p> <p>Mwenendo mzuri ungelikuwa kwa Watendaji Wakuu kuteuliwa na Bodi za Wakurugenzi badala ya kuteuliwa na mamlaka moja. Rais angeachiwa jukumu la kuteuwa Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi wakati uteuzi wa Maafisa Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali lingekuwa ni jukumu la Bodi za Wakurugenzi.</p>	Pendekezo lipo kwenye utekelezaji.
4.	<p>Bodi za Wakurugenzi na Uwajibikaji</p> <p>Kama ilivyopendekezwa kwenye ripoti yangu ya mwaka uliopita kuwa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinapaswa kuwajibika kwa Serikali kwa matokeo ya utendaji kazi, vilevile Menejimenti za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zitawajibika pia kwa Bodi za Wakurugenzi kwa matokeo ya utendaji kazi.</p>	Pendekezo halijatekelezwa.

5.	<p>Haja ya Kuanzishwa Mfuko wa Umma wa Uwekezaji          Siyo siri kwamba Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali za Umma zimegubikwa na matatizo mengi, kubwa ikiwa la ukosefu wa mitaji, ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali. Fedha hizo zitatumika pia kuinua uwekezaji katika Sekta ya Umma. Kuna haja kubwa ya kuanzisha mfuko huu ukizingatia mapato hasa yanayopatikana kutokana na uwekezaji kwenye baadhi ya Mashirika.</p> <p>Serikali inapaswa kuanzisha Mfuko wa Umma wa Uwekezaji ili kuweza kukabiliana na changamoto hizi. Gawio na misaada ya wahisani inayopatikana katika nyanja hii zinaweza kuwekwa katika mfuko huu. Fedha hizo hazipaswi kutumiwa katika shughuli za matumizi ya kawaida bali zinaweza kutumika kwenye miradi ya maendeleo kama vile miradi mipya, kuongeza mitaji na kutoa mikopo nafuu kwa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinazohitajika</p>	Pendekezo halijatekelezwa.
6.	<p>Ajira za Kudumu za Pensheni Vis-a-Vis Ajira za Mkataba kwa Wafanyakazi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali          Kuna haja ya Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi na Ofisi ya Rais ya Menejimenti za Huduma kwa Umma (POPSM) kuhusishwa katika kupitisha miundo ya ajira wa aina hii kwa wafanyakazi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kutoka kwenye ajira za kudumu na pensheni kwenda kwenye ajira za utendaji na mikataba.</p>	Pendekezo halijatekelezwa.
7.	<p>Kuchelewa Kuteua Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi Za Serikali          Serikali na Mamlaka husika za uteuzi zinapaswa kuhakikisha kuwa Bodi za Wakurugenzi zinateuliwa mapema pale muda wa Bodi unapokwisha kutokana na ukweli kwamba kuna</p>	Pendekezo lipo kwenye utekelezaji.

	madhara makubwa kuchelewa kuteua Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali	
8.	<p>Kutokuwepo kwa Usawa Katika Matumizi ya Mali za Umma</p> <p>Kuna haja ya Serikali kuhakikisha kuwa kuna uwiano katika marupurupu wanayopata Menejimenti na Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kutokana na ukweli kwamba raslimali wanayotumia ni raslimali ya umma kama ilivyokuwa kabla ya kuvunjwa kwa Kamati ya Kudumu ya Mashirika ya Umma (SCOPO).</p>	Pendekezo halijatekelezwa.
9.	<p>Ukaguzi Maalumu Uliofanyika TRL</p> <p>(a) Malipo ya Nyongeza ya Mishahara</p> <p>Kiasi kilichotakiwa kudaiwa na TRL na kulipwa na Serikali kama nyongeza ya mishahara kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Julai 2008 kingelikuwa sahihi kama kingelipwa ni shilingi bilioni 1.4 na sio shilingi bilioni 9.8 zilizodaiwa.</p> <p>Kwa hiyo, TRL ilidai zaidi shilingi bilioni 8.4 kutoka Serikalini.</p> <p>Serikali inapaswa kuangalia upya uamuzi wake wa awali wa kulipa nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi wa TRL na kuchukua hatua madhubiti za kuhakikisha Serikali haiendelei kulipa mishahara hiyo.</p> <p>(b) Ada ya Makubaliano ya Maridhiano Kati ya Serikali na TRL Isiyolipwa Shilingi Bilioni 16.1</p> <p>Serikali inapaswa kufanya tathmini ya ubia wake na RITES, hali ya sasa ya ubia wao, kutokufuata vipengele vya mkataba wa makubaliano, matatizo ya sasa yanayokumba uendeshaji na endapo TRL itaendelea huendesha shughuli zake “going concern” na kutafuta suluhu ya kumaliza</p>	<p>Pendekezo limetekelezwa kiasi.</p> <p>Pendekezo limetekelezwa kiasi.</p>

	matatizo hayo.	
10.	<p>Mkopo wa PSPF Shilingi Bilioni 58 na Marejesho ya Mikopo ya Wanafunzi Shilingi Bilioni 51.1 Serikali inapaswa kuhakikisha kwamba bakaa ya deni lote la mkopo (ikiwa ni kiasi cha mkopo na tozo) lililokopwa kutoka PSPF linalipwa bila kuchekelewa ili kuepuka gharama zaidi za tozo na adhabu. Bodi inapaswa kuanza kutekeleza hatua za kisheria kwa waajiri na wakopaji binafsi ambao hawatoi ushirikiano kama ilivyoelezwa na sehemu ya 19A-23 ya Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya 2004.</p>	Pendekezo lipo kwenye utekelezaji.
11.	<p>Usimamizi wa Mapato na Matumizi Kutokuandaliwa mapema kwa hati za madai ya wateja, kuchelewa kukusanya mapato, kutokuwa na taarifa sahihi na zilizokamilika za mapato na kutokuwa na ulinzi wa kutosha wa fedha za makusanyo. Kwa upande mwingine, ukaguzi wa matumizi kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali ulibaini kwamba baadhi ya Mashirika ya Umma yana mifumo dhaifu ya matumizi ya fedha iliyopelekea baadhi ya malipo kufanywa bila kuzingatia uidhinishwaji unaokubalika na baadhi ya malipo kulipwa bila ya kuwa na nyaraka pungufu.</p> <p>Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinapaswa kuhakikisha kwamba mifumo thabiti ya menejimenti ya mapato na matumizi ipo na inafanya kazi vizuri ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za Umma.</p>	Pendekezo halijatekelezwa.
12.	<p>Usimamizi wa Sheria za Manunuzi na Mikataba Bodi ya Wagavi "Procurement Supplies Professionals and Technician Board" inapaswa kuongeza kasi zaidi ya kufanya kazi ya manunuzi kuwa ya kitaalamu, kuimarisha mawasiliano na Taasisi za Mafunzo katika kuhakikisha mitaala yao inakidhi soko na kusimamia</p>	Pendekezo halijatekelezwa.

	<p>uzingatiaji wa Sheria za Manunuzi za Umma.</p> <p>Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinapaswa kuzingatia vipengele vya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005.</p>	
13.	<p>Usimamizi wa Raslimali Serikali, Bodi za Wakurugenzi Maafisa Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali wanapaswa kuhakikisha kwamba wanawekeza kwenye makampuni yanayojiendesha kwa tija. Zaidi ya hayo, Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinapaswa kuhakikisha zinapata umiliki halali wa nyumba, mitambo, magari na pikipiki zinazomiliki</p>	Pendekezo halijatekelezwa.
14.	<p>Usimamizi wa Raslimali Watu Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali yanashauriwa kuwapatia fedha taslimu waajiriwa wake na kuwaacha waajiriwa kulipia huduma ya umeme kama wateja wengine badala ya kutoa hati za madai zenye punguzo au huduma ya maji n.k kama motisha kwa waajiriwa ambayo kwa kiasi zinatumiwa vibaya. Pia michango na makato yote ya kisheria yanapaswa kutumwa kwa wakati kwa Taasisi zinazohusika kama ilivyotajwa kwenye Sheria husika</p>	Pendekezo halijatekelezwa.
15.	<p>Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Menejimenti za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinapaswa kuanzisha Kitengo cha Teknolojia cha Habari na Mawasiliano kitakachokuwa na jukumu la kuendeleza na kutunza mifumo ya taarifa za Kompyuta na kuhakikisha Sera madhubuti za Teknolojia za Habari na Mawasiliano zinaandaliwa na zinatumiwa kwa kuendeshea ya mifumo hiyo ndani ya Shirika husika. Pia, Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinapaswa kuwa na mpango madhubuti wa kupata kumbukumbu wakati wa kipindi cha majanga.</p>	Pendekezo halijatekelezwa.

16.	<p>Matokeo ya Ukaguzi Maalum Yaliyofanyika TANESCO</p> <p>Bodi ya Wakurugenzi ya TANESCO inapaswa kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya 2004 na Kanuni zake za 2005 na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana wakati wa kusimamia shughuli za kila siku za Shirika hilo.</p>	Pendekezo halijatekelezwa.
17.	<p>Kupima Utendaji Kazi wa Mashirika Yaliyopo na Yale Yaliyobinafsishwa Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa madeni ya Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali ambazo marejesho yake yalikuwa yameiva lakini yalikuwa hayajarejeshwa, yanarejeshwa ili kuepuka Serikali kulipa mikopo hiyo na bakaa ya mapato ya kipindi cha nyuma yanakusanywa bila kuchelewa zaidi.</p> <p>Shirika Hodhi la Mali za Makampuni yaliyobinafsishwa (CHC) linapaswa kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kampuni zilizobinafsishwa zinazijiendesha kulingana na makubaliano ya mikataba ya mauzo na kuchukua hatua madhubuti kwa kampuni zote zinazojiendesha bila kuzingatia makubaliano ya mikataba ya mauzo.</p>	Pendekezo lipo kwenye utekelezaji.

### 3.3 Hitimisho

Napenda kutoa Shukrani zangu za dhati kwa majibu niliyopokea kutoka Serikalini kupitia kwa Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali yanayojibu mapendekezo ya mwaka uliopita. Kwa ujumla majibu niliyopata hayajitoshelezi, mapendekezo hayajapewa kipaumbele na uzito unaostahili. Majibu yaliyotolewa yanajibu tu mapendekezo machache, hivyo Serikali bado haijaonyesha juhudi za kutosha za kusimamia utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na kuyapatia ufumbuzi wa kutosha. Mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa na machache yapo kwenye hatua za utekelezaji. Bado naishauri Serikali kutilia mkazo mapendekezo ya ukaguzi na kuyapatia ufumbuzi wa kudumu ili kufanya Mashirika na Taasisi za Umma ziendeshe kwa ufanisi zaidi.

## SURA YA NNE

### MASUALA MUHIMU AMBAYO HAYAKURIPOTIWA KATIKA RIPOTI YA MWAKA ULIOITANGULIA

#### 4.0 Utangulizi

Kwa mujibu wa Sehemu ya 31 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ni wajibu wa kila Shirika la Umma kuwasilisha hesabu kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kufunga mwaka wa fedha. Kwa vile kumekuwa na kiasi kikubwa cha kutokuzingatia kwa matakwa haya ya sheria katika baadhi ya Mashirika ya Umma, ukaguzi katika baadhi ya Mashirika ya Umma umekuwa unachelewa kuanza na hivyo kumsababisha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kushindwa kuripoti kuhusu kaguzi hizo katika mwaka husika. Ni muhimu ikaeleweka kuwa Mashirika ya Umma ambayo kaguzi zake zitashindwa kukamilika katika kipindi kinachotakiwa na hivyo kutoripotiwa katika ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka husika, kaguzi hizo zitaripotiwa katika mwaka unaofuata.

Hadi kufikia kipindi cha kuandaa ripoti ya mwaka jana iliyowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais mwishoni mwa mwezi Machi, 2010, ni kaguzi za mashirika 51 tu zilikuwa zimekamilika na kuingizwa katika ripoti na kaguzi za Mashirika yaliyobaki yapatayo 115 hazikuwa zimekamilika kutokana na masuala mbalimbali ikiwemo kuchelewa kuwasilisha hesabu, kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi baada ya zile za awali kumaliza muda wake, menejimenti za mashirika husika kushindwa kujibu kwa wakati hoja za ukaguzi na masuala mengine.

Kutokana na hali hiyo, sura hii inaelezea kwa kifupi masuala muhimu ambayo yapo katika ripoti za baadhi ya mashirika zilizokuwa hazikukamilika mwaka jana na hivyo kutoingia katika ripoti ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2009 iliyotolewa tarehe 26 Machi 2010.

**4.1 Madeni ambayo Hayajakusanywa na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) Shilingi bilion 2.3**

Kampuni ya TSN inayo sera ya madeni ambayo inaelekeza kuwa madeni yote yakusanywe katika muda wa siku 30 toka siku ambayo hati ya madai inatolewa, vinginevyo madeni yote yatakayovuka muda huo yatatakiwa kutozwa riba ya asilimia 1 kila mwezi, kusitishwa huduma ya mkopo na ikilazimu hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya wadaiwa wa muda mrefu. Hata hivyo, tulibaini kuwepo kwa madeni yasiyokusanywa ya shilingi bilion 2.3 hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2008 yakiwa ni madeni ya muda mrefu zaidi ya siku 30 na hakukuwa na hatua yoyote iliyochukuliwa na menejimenti ya kampuni kwa mujibu wa sera husika.

**4.2 Fedha Zilizo Katika Hatari ya Kutorejeshwa Katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

Katika kupitia uwekezaji wa fedha za wanachama wa NSSF katika mikopo mbalimbali tulibaini kutokuwepo kwa uzingativu wa mikataba baina ya wale waliokopa hivyo kupelekea kuwa na hofu juu ya urejeshwaji wa fedha hizo walizokopeshwa. Ilibainika kuwa mikopo mingi ilitolewa ambapo hadi wakati wa ukaguzi haikuwa imerejeshwa hali inayoashiria kuwa menejimenti ya NSSF haikufanya upembuzi wa kina kabla ya kutoa mikopo hiyo. Kutokana na kutolipika kwa mikopo hiyo, menejimenti ya NSSF imeanza kujiandaa kufuta baadhi ya mikopo kutokana na dalili kuwa huenda isirejeshwe. Mikopo hiyo ni pamoja na hii ifuatayo:-

**a) Kiwira Coal and Power Ltd**

Mkopo kabla ya riba wa kiasi cha shilingi bilioni 9.009 uliotolewa na NSSF kwenda kwa Kiwira Coal Power Ltd ambapo muda wa kurejesha mkopo huo ulikwisha tarehe 8 Januari, 2008 na Mfuko ulitoa notisi ya madai. Mdaiwa aliomba nyongeza ya muda kutokana na kutokukamilika kwa taratibu za urejeshaji. Katika kikao chake cha 44 kilichofanyika tarehe 17 Novemba, 2008, Bodi ya Wadhamini ya NSSF iliridhia nyongeza ya muda hadi tarehe 31 Disemba 2008. Hadi namaliza ukaguzi wa hesabu za



shirika hilo kwa mwaka husika hapakuwepo marejesho ya mkopo yoyote yaliyokuwa yamefanywa. Kwa hiyo, riba ya mkopo huo imefikia shilingi bilioni 2.689. Jumla ya mkopo pamoja na riba kwa sasa ni shilingi bilioni 11.698.

b) General Tyre East Africa

Mkopo wa dola za kimarekani milioni 10 ulitolewa kwa kampuni ya General Tye East Africa mnamo mwaka 2005. Riba ya kwanza ilitakiwa kulipwa mwezi Disemba 2005, na mkopo wenyewe kulipwa Novemba, 2007. Mkopo huu ulidhaminiwa na Serikali kwa asilimia 85. Mnamo tarehe 4/7/2008 NSSF iliiandikia Serikali kuitaka ilipe mkopo baada ya mdeni kushindwa kulipa na kuwa kiasi kinachobaki kipatikane kutokana na mauzo ya dhamana iliyowekwa. Hadi tarehe 30 Juni 2009 mkopo huu ulikuwa umefikia shilingi bilioni 16.576. Barua ya kukumbushia deni ilitumwa kwa Wizara ya Fedha tarehe 15 Disemba 2008. Tarehe 24 Aprili 2009, Wizara iliiandikia NSSF ikiitaka kuwa na subira wakati Serikali inakamilisha taratibu za kufilisi kampuni hii. Ili kufahamu thamani ya dhamana iliyowekwa, NSSF kupitia barua yenye kumbukumbu N.NSSF/LA/F.507/08/2004/VOL.II/164 ya tarehe 10/07/09 walimuomba mthamini mali wa Manispaa ya Arusha kuthaminisha mali iliyowekwa kama dhamana dhidi ya mkopo. NSSF imeanza taratibu za kufuta riba ya shilingi bilioni 3.461 kama deni lisilolipika.

c) MediTech Industrial Co

NSSF ilitoa mkopo wa dola za kimarekani shilingi milioni 1.45 mwaka 2004. Kampuni ilishindwa kutimiza masharti kwa kushindwa kulipa mkopo huo. Ili kutatua tatizo, kampuni iliingia ubia na muwekezaji kutoka nchini Denmark M/s Emunio Tanzania limited ambaye alikubali kuwekeza Yuro milioni 1.8 tarehe 29 Januari 2007, mkopaji aliuomba Mfuko kusitisha madai ya riba katika mkopo na kisha kusogeza mbele muda wa kulipa kwa miaka mingine miwili. Ombi hili lilikubaliwa na Bodi ya Wadhamini wa NSSF katika kikao chake cha 44 ambapo riba ya USD 74,645 ilishalipwa. Baadae muda wa kurejesha mkopo ulibadilishwa na badala

ya kurejeshwa 2009 ulitakiwa kurejeshwa mwaka 2011. Kutokana na kukosekana kwa mtaji wa uendeshaji (working capital), kampuni hii haijaanza uzalishaji. Kwa hiyo kampuni hii ilishindwa kwa mara nyingine kutimiza wajibu wake. Mnamo tarehe 8 Mei 2009, Mfuko ulitoa notisi ya kushindwa kulipa ambayo iliisha muda wake 8 Agosti 2009. Jumla ya deni lote ni shilingi bilioni 2.653.

**d) Killimanjaro Bazaar Loan**

Mkopo huu ulitolewa katika awamu tatu kati ya mwaka 1990 na mwaka 1992. Hadi kufikia Februari 1999, jumla ya mkopo ulikuwa shilingi milioni 788.7. Kwa kuwa mkopaji alikuwa ameshindwa kutimiza wajibu wake, mwezi Februari 1999, NSSF ilimpeleka mahakamani ikitaka kukamatwa kwa dhamana ya mkopo. Hata hivyo mkopaji alishinda kesi na NSSF iliamriwa kulipa gharama za kesi shilingi milioni 600. NSSF ilikata rufaa kuhusu maamuzi ya Mahakama Kuu-Moshi na uamuzi wa awali ulitolewa kuhusu pingamizi la Kilimanjaro ambapo NSSF ilikubaliwa kusikilizwa. Rufaa ilisikilizwa tarehe 27 Mei 2009 ambapo siku ya kutolewa hukumu bado inasubiriwa. Jumla ya deni lote ni shilingi milioni 850 ambapo menejimenti imeanza maandalizi ya kufuta deni hili toka vitabuni.

**e) Mbowe Hotels**

Mkopo wa shilingi milioni 15 ulitolewa mwaka 1990. Mkopaji ameshindwa kurejesha mkopo na hivyo kupelekea ongezeko kubwa la riba hadi kufikia shilingi milioni 229.898 hadi kufikia mwezi Juni 2001. NSSF ilichukua hatua za kisheria dhidi ya mkopaji ambapo ilishinda. Ingawa NSSF ilishinda mkopaji alishindwa kulipa mkopo kama ilivyoamriwa na Mahakama. Baadae mwezi Disemba 2006 na Januari 2007 Mkopaji alilipa jumla ya shilingi milioni 55. Kwa hiyo, jumla ya deni lote ni shilingi milioni 174.898. Katika kikao cha bodi kilichofanyika tarehe 21/07/2001, Bodi iliidhinisha kusitisha kukua kwa riba katika mkopo huu kuanzia tarehe 30 Juni 2001. Kiasi cha riba hadi tarehe 30 Juni 2009 kilikuwa shilingi milioni 174,898 ambapo menejimenti inafanya utaratibu wa kufuta deni hilo.

f) Continental Ventures

Mkopo wa dola za kimarekani milioni 3.5 ulitolewa mwaka 2005 ambapo ulitakiwa kuwa na dhamana ya Serikali kwa asilimia 85 kwa mkopo bila riba. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe ya kuandika taarifa hii, hakuna marejesho ya mkopo yaliyofanyika licha ya ahadi kutoka kwa Waziri wa Fedha. Mkopaji amefunga uzalishaji. Licha ya jitihada nyingi mkopaji ameshindwa kulipa mkopo na riba na hivyo kupelekea NSSF kutaka kulipwa kupitia dhamana ya Serikali. Tayari Mfuko umeshatoa taarifa ya kushindwa masharti ambayo iliisha tarehe 26/6/2008 na sasa Mfuko uko katika hatua za kuuza mali za Kampuni. Hata hivyo menejimenti ya NSSF inaandaa utaratibu wa kufuta deni hilo.

4.3 Mikopo ya Wanafunzi Iliyoibiwa Nchini Algeria (€ 9,154.05)

Tulibaini kuwa kiasi cha dola za kimarekani 12,539.32 (€ 9,154.05) kilipelekwa kwa wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma nchini Algeria kupitia Ubalizi wa Tanzania nchini Ufaransa mnamo mwezi wa Aprili 2009 ikiwa ni fedha za kujikimu kwa wanafunzi watano. Hata hivyo; tulibaini kuwa fedha hizo hazikuwa zimelipwa kwa wanafunzi hao kama ilivyokusudiwa.

Kiasi hicho kililipwa na Ubalizi wa Ufaransa kwenda akaunti Na. 0163300019/68 ya ndugu Rweikiza Rugeyamba Erasto ambaye alikuwa kiongozi wa chama cha wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma nchini Algeria kwa lengo la kuwapatia wenzake waliokusudiwa. Rweikiza Rugeyamba Erasto alipunguza kiasi cha fedha katika fedha alizotakiwa kuwapatia wanafunzi wenzake na kuwaacha wakiishi maisha magumu.

Pia, Rweikiza alitumia fursa ya kuaminiwa na wenzake kwa kutayarisha orodha ya malipo bandia na kuacha kiasi cha zile fedha zilizotumwa kwake kutoka ubalizi wa nchini Ufaransa kwa kupunguza viwango vilivyotayarishwa na bodi

ya mikopo. Mwezi Februari 2009 Bodi ya Mikopo ilituma dola za kimarekani 35,644.11 (€27,897.36) ambayo ni sawa na shilingi milioni 46.9 lakini Mr. Rweikiza Erasto alitayarisha orodha nyingine iliyopunguzwa €70.25 ambayo ni fedha aliyojipatia visivyo halali. Hata hivyo Rweikiza alishasimamishwa masomo huko Algeria na alisharudishwa nchini na uchunguzi wa polisi unaendelea. hA

#### 4.4 Utoaji wa Mikopo kwa Wanafunzi Wanaoendelea na Masomo Nje ya Nchi Bila Kupata Taarifa ya Maendeleo ya Kitaaluma

Ukaguzi nchini India, Russia na China ulibaini kuwa wanafunzi wanaoendelea na masomo wamekuwa wakilipwa na Bodi ya Mikopo ada na posho za malazi bila ya kupata na kupitia taarifa za maendeleo ya kitaaluma. Haikuweza kufahamika ni kwa namna gani na ni kwa vigezo vipi ambavyo Bodi ya mikopo inaweza kutoa mikopo katika mazingira haya wakati kunakuwa na wanafunzi wengine wanaofeli mitihani yao na wengine kufukuzwa vyo. Nchini China mwanafunzi anayejulikana kama Magimila Shamoro Ahmad wa Chuo Kikuu cha Afya cha Tianjian alifeli masomo na kuondoka chuoni baada ya kupokea kiasi cha shilingi milioni 12.5 kama mkopo wa masomo kutoka Bodi ya Mikopo.

#### 4.5 Mikopo ya Wanafunzi Ambayo Haijarejeshwa Shilingi Milioni 80.9

Kutoka mwaka 1994 hadi mwezi Juni 2009, Bodi ya Mikopo ilikuwa imetoa jumla ya mikopo inayofikia shilingi bilioni 433.3 kwa wanafunzi katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi ambapo kati ya mikopo hiyo shilingi bilioni 80.9 ni mikopo inayotakiwa kurejeshwa Bodi ya Mikopo kwa kuzingatia kuwa wanafunzi wahasika walikwisha maliza masomo yao kama inavyoonekana hapa chini:-

**Jedwali 7: Mikopo ya Wanafunzi Ambayo Haijarejeshwa**

Maelezo	Juni 2008		Juni 2009	
	Idadi ya	Kiasi	Idadi ya	Kiasi

	Wanafunzi	Sh.	Wanafunzi	Sh.
Jumla ya Mikopo yote	55,687	294,160,780,167.00	58,798	433,254,461,262.00
Mikopo ambayo iko tayari kurejeshwa	48,378	51,103,685,914.00	56,801	80,957,774,609.00
Awamu za malipo	48,378	5,110,368,591.40	48,378	15,331,105,774.20

Hadi kufikia Juni 2009 Bodi ya mikopo ilitakiwa kuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 15.3 ikiwa ni awamu za malipo kutoka kwa wanafunzi lakini hadi kufikia tarehe 30 Juni 2009 Bodi hiyo ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 2.2 tu. Hata hivyo ukusanyaji wa mikopo yote iliyostahili kurejeshwa imekuwa ikisuasua.

#### 4.6 Udhaifu Katika Usimamizi wa Mali za TANAPA

Kumekuwepo na udhaifu katika kusimamia mali na mitambo ya TANAPA inayofikia thamani ya shilingi bilioni 62.2 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2009. Baadhi ya mapungufu yaliyobainika ni pamoja na:-

- i. Ingawaje mali za TANAPA zenye thamani ya shilingi bilioni 16.4 (bila majengo, barabara na ardhi) zilihakikiwa mnamo tarehe 30/6/2009 lakini matokeo ya uhakiki huo hayakuoanishwa na daftari la mali.
- ii. Hakukuwa na nyaraka za umiliki wa ardhi katika eneo la - Fort Ikoma katika Mbuga ya Taifa ya Serengeti.
- iii. Kulikuwa na mali ambazo zilitolewa na Idara ya Wanyama Pori na kupelekwa katika Mbuga ya Taifa ya Mkomazi bila ya kuthaminiwa na kuingizwa vitabuni.

#### 4.7 Makosa Katika Taarifa ya Thamani ya Mali iliyo Katika Ghala la Bohari ya Madawa (MSD) Shilingi Bilioni 98.4

Tumebaini kuwa katika thamani ya mali zilizo katika ghala zenye thamani ya shilingi bilioni 39.093 kuna mali zenye thamani ya shilingi milioni 98.4 kutoka katika akaunti inayojulikana kama “Inters Zone Transfers” ambayo inatokana na malimbikizo ya muda mrefu. Hata hivyo thamani hii haiwakilishi thamani ya mali yoyote iliyo katika ghala na kwa hiyo kufanya thamani ya mali iliyo ghalani kuwa imezidishwa thamani yake.

#### 4.8 Hitimisho

Masuala ambayo yameripotiwa katika sura hii ni sehemu tu ya masuala ambayo hayakuripotiwa mwaka jana kutokana na kutokukamilika kwa kaguzi za Mashirika na Taasisi za Serikali zilizoripotiwa. Tunapenda kusisitiza kuwa kuchelewa kwa Mashirika na Taasisi za Umma kuandaa na kuwasilisha hesabu kwa ajili ya ukaguzi hupelekea kuchelewa kumaliza na kuripoti matokeo ya ukaguzi wake. Kuchelewa kuwasilisha hesabu na kupelekea huchelewa kuripoti kwa wakati muafaka kunaondoa umuhimu na maana ya taarifa zinazotolewa. Tunaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kuchukua hatua kali za kisheria kwa Mashirika na Taasisi za Serikali zote zitakazoshindwa kuwasilisha hesabu kwa wakati.

## SURA YA TANO

### USIMAMIZI WA MAPATO NA MATUMIZI

#### 5.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea usimamizi wa mapato na matumizi katika Mashirika ya Umma ambayo yametolewa taarifa kwenye ripoti za ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2010. Wakati wa ukaguzi wa Mashirika ya Umma, mambo mbalimbali yalijitokeza kuhusu mapato na matumizi. Hata hivyo, kwa madhumuni ya utoaji wa taarifa katika ripoti hii ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tumeamua kuigawa sura hii katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inahusu usimamizi wa mapato na sehemu ya pili inahusu usimamizi wa matumizi kama ifuatavyo:

#### 5.1 Usimamizi wa Mapato

Mapato yanayotokana na shughuli za msingi za Taasisi au Shirika, yanajulikana pia kwa majina mengine kama vile mauzo, ada, riba, gawio au mrahaba. Mapato yanatambulika tu baada ya kuonekana kuwa manufaa ya kiuchumi yatapatikana. Mapato yanarekodiwa tu pale ambapo huduma imetolewa. Kwa hiyo ni jukumu la menejimenti katika Mashirika na Taasisi za Umma kuhakikisha mapato yanayopatikana yanaingizwa katika vitabu vya hesabu kama ilivyoainishwa kwenye viwango vya kijasibu vya kimataifa.

Zifuatazo ni hoja zilizotokana na tathmini iliyofanyika juu ya usimamizi wa mapato katika baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010.

##### 5.1.1. Kutokuwepo kwa Ufanisi Katika Ukusanyaji wa Madeni

Ukusanyaji wa madeni katika Mashirika na Taasisi za Umma umekuwa ni tatizo linalosababisha ukwasi katika Mashirika mengi. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa madeni kiasi cha shilingi bilioni 52.2 katika Mashirika na Taasisi za Serikali 17 ambazo hazijakusanywa kutoka kwa wateja kwa muda

mrefu. Kutokusanywa kwa madeni hayo kunakwamisha shughuli nyingi katika Mashirika na Taasisi za Umma. Madeni ambayo hayajakusanywa kwa zaidi ya kipindi kinachostahili yameainishwa katika jedwali lifuatalo:-

**Jedwali 8: Madeni Ambayo Hayajakusanywa:-**

Na.	Jina La Shirika	Kiasi (Sh)	Maelezo
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tabora (TUWASA)	1,156,446,994	Ankara ambazo hazijalipwa kutoka kwa Wateja.
2.	Bodi ya Korosho Tanzania	281,963,000	Madeni ambayo hayajakusanywa kutoka kwa wateja.
3.	Bodi ya Usajili ya Wakandarasi (CRB)	1,158,922,000	Ada za Wakandarasi ambazo hazijalipwa kwa zaidi ya mwaka mmoja.
4.	Kampuni ya Kusimamia Rastimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO)	36,645,021,073	Madeni ambayo hayajakusanywa kwa muda mrefu.
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga (SHUWASA)	260,826,959	Ankara za maji ambazo hazijakusanywa kutoka kwa wateja.
6.	Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO)	176,315,435  111,860,000	<ul style="list-style-type: none"> <li>● Madeni ya mikopo ambayo hayajakusanywa.</li> <li>● Kodi za majengo kutoka kwa wapangaji wanaokaa nyumba za SIDO bila mikataba.</li> </ul>
7.	Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)	362,995,415	Deni la muda mrefu toka Serikalini litokanalo na kiwanja cha Bandari kilichogawiwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.
8.	Shirika la Magazeti Tanzania (TSN)	2,048,861,365	Deni la muda mrefu.
9.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)	315,992,145	Deni ambalo halijakusanywa kwa muda mrefu.
10.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)	1,238,713,648	Mapato ambayo hayajakusanywa



			kutokana na kodi za majengo, na kutokumalizika kwa miradi kwa muda unaotakiwa.
11.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA)	161,000,000	Madeni yasiyokusanywa zaidi ya miaka mitatu.
12.	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)	44,073,650	Shirika limeshindwa kukusanya kodi za nyumba za Mwanza kiasi cha Sh.8,623,650 na kutoka kampuni iliyokodi majengo ya TAMKO Kibaha kiasi cha Sh.35,450,000
13.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga (TUWASA)	661,492,503 37,069,000	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Ankara ambazo hazijalipwa na wateja wa maji.</li> <li>• Madeni mengine yaliyokaa zaidi ya miaka miwili.</li> </ul>
14.	Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania.	6,037,252	Kodi ya pango ambayo haijalipwa na mpangaji ambaye mkataba wake wake haukupatikana.
15.	Shirika la Posta la Tanzania (TPC)	5,805,930,427	Madeni ya muda mrefu ambayo hayajakusanywa na Shirika.
16.	Ubungo Plaza Ltd.	396,698,849	Kodi ya pango ambayo haijalipwa zaidi ya miezi sita.
17.	Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC)	1,329,910,817.22	Madeni ambayo hayajalipwa na wateja.
Jumla		52,200,130,532.10	

### 5.1.2. Usimamizi wa Mabomba Yanayovuja Maji na Kuandika Ankara kwa Makosa

Uvujaji maji katika mabomba na utoaji wa ankara zisizo sahihi limekuwa ni tatizo kubwa na linalozidi kuongezeka katika Mamlaka za Maji, hali inayopelekea kupungua kwa mapato. Kupotea kwa mapato hayo kumesababisha kutopanuka kwa huduma za maji na hatimaye kukidhi mahitaji yanayozidi kuongezeka siku hadi siku. Kupotea kwa maji na utoaji wa ankara ambazo ni chini ya gharama sahihi kumesababisha mamlaka za maji kuwa tegemezi kwenye mikopo na misaada kutoka nje. Hali hii ilibainika wakati wa kaguzi za mamlaka za maji ambapo viwango vya mapato hupotea kutokana na uvujaji wa maji, utoaji wa ankara zenye makosa, uunganishwaji wa maji nje ya taratibu, wizi wa maji na ubovu wa mita za maji. Hata hivyo kuna kiwango kilichowekwa na Mamlaka ya Udhubiti wa Nishati na Maji (EWURA) kwamba kiwango cha upotevu wa maji kisizidi asilimia 27 ya uzalishaji. Mamlaka zilizobainika na mapungufu hayo ni pamoja na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza (MWAUWASA) iliyopoteza shilingi milioni 23.017 kwa kuandika ankara pungufu ya gharama sahihi. Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma ilipoteza jumla ya mita za ujazo 4,273,467 kutoka jumla ya uzalishaji wa mita za ujazo 9,916,911 wakati Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga (SHUWASA) ilipoteza mita za ujazo 856,687 na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida (SUWASA) mita za ujazo 549,731. Hali hii ya kupotea kwa mapato si nzuri, inahitaji kushughulikiwa mapema na Serikali na Mashirika husika.

### 5.1.3. Ucheleweshwaji wa Fedha za Mashirika Kutoka Hazina

Mahitaji ya fedha zilizopitishwa kwenye bajeti ya Mashirika na Taasisi za Umma ni suala la msingi na la kupewa kipaumbele, ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizopangwa ndani ya Mashirika na Taasisi za Umma. Ukaguzi wa Mapato ndani ya mwaka husika ulibaini kuwepo kwa ucheleweshwaji wa upatikanaji fedha kutoka Hazina kulingana na bajeti. Ucheleweshwaji huo

umekwamisha shughuli nyingi za Mashirika na Taasisi za Umma kutekelezwa kwa wakati kutokana na ukosefu fedha. Hili suala limekuwa ni moja ya changamoto zinazoikabili Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB). Bodi imekuwa ikishindwa kulipa fedha za mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa wakati kutokana na Hazina kutoa fedha za mikopo ya wanafunzi kwa kuchelewa na kwa mafungu madogo chini ya mahitaji. Hali hii imepelekea kuwepo kwa migomo ya wanafunzi mara kwa mara wakilalamika kuwa Bodi imeshindwa kulipa fedha za mikopo kwa wakati.

Jedwali hapa chini linaloonyesha ucheleweshwaji wa fedha ikilinganishwa na matarajio ya mtiririko wa fedha na mahitaji ya wanafunzi na jinsi fedha zilivyokuwa zikipokelewa na Bodi kila robo mwaka kutoka Hazina katika miaka mitatu kuanzia 2008/2009, 2009/2010 hadi Januari 2011.

#### Mwaka 2008/2009

Na.	Robo Mwaka /Mwezi	Kiasi Kilichopokelewa Sh.	Matarajio Kulingana na Mahitaji Sh.	Tofauti Zaidi/(Pungufu)	Maoni
1.	Julai-Sept. 2008	28,741,975,047	54,071,593,911	(25,329,618,864)	Pungufu
2.	Okt - Dis 2008	31,883,024,953	31,644,634,649	238,390,304	Zaidi
3.	Januari - Machi 2009	37,100,000,000	20,803,968,591	16,296,031,409	Zaidi
4.	Aprili - Juni 2009	41,375,000,000	10,479,802,848	30,895,197,152	Zaidi
Jumla		139,100,000,000	116,999,999,999	22,100,000,001	Zaidi

#### Mwaka 2009/2010

Na.	Robo Mwaka/Mwezi	Kiasi Kilichopokelewa Sh.	Matarajio Kulingana na Mahitaji Sh.	Tofauti Zaidi/(Pungufu)	Maoni
1.	Julai-Sept. 2009	67,543,758,418	46,452,711,486	21,091,046,932	Zaidi
2.	Oct - Dis 2009	11,000,000,000	55,141,046,995	(44,141,046,995)	Pungufu
3.	Januari - Machi 2010	47,000,000,000	95,755,180,394	(48,755,180,394)	Pungufu
4.	Aprili - Juni 2010	-	70,805,200,000	(70,805,200,000)	Pungufu
Jumla		125,543,758,418	268,154,138,875	(142,610,380,457)	Pungufu

Mwaka 2010/2011

Na.	Robo Mwaka/Mwezi	Kiasi Kilichopokelewa Sh.	Matarajio Kulingana na Mahitaji Sh.	Tofauti Zaidi/(Pungufu)	Maoni
1.	Julai-Sept 2010	2,000,000,000	96,819,570,224	(94,819,570,224)	Pungufu
2.	Oct - Dis 2009	86,096,000,000	24,362,836,750	61,733,163,250	Zaidi
3.	Januari 2011	30,000,000,000	63,831,988,031	(33,831,988,031)	Pungufu
4.	-	0	0	-	
Jumla		118,096,000,000	185,014,395,005	(66,918,395,005)	Pungufu

Kwa hiyo, katika vipindi ambavyo kuna upungufu na ucheleweshwaji wa fedha za wanafunzi kutoka Hazina ndipo yanatokea matatizo kati ya wanafunzi na Bodi ya Mikopo. Ili kupunguza migomo na maandamano ya wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu ambayo inaweza kuathiri wanafunzi kimasoma na maendeleo ya Taifa kwa ujumla, Hazina itafute utaratibu mzuri wa kutatua tatizo hili ikiwa ni pamoja na kutoa fedha za wanafunzi zinazotosha kwa wakati.

#### 5.1.4 Kutokuonyesha Mapato Kama Inavyotakiwa Katika Vitabu vya Hesabu

Mapato ni maingizo vitabuni ambayo hutokana na shughuli za shirika kabla ya kutoa matumizi na ambayo hupatikana katika shughuli za kawaida au biashara za Taasisi. Mapato yanatambulika tu pale ambapo manufaa yatokanayo na shughuli za biashara yanayoingia katika Taasisi. Mapato na matumizi ya biashara moja huwa yanatambulika kwa pamoja. Mapato hayawezi kupatikana na kutambulika kama matumizi yake hayafahamiki.

Ilibainika kuwa baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma hazikuonyesha mapato yake kama inavyotakiwa na Viwango vya Kihisibu vya Kimataifa. Pia, kuna baadhi ya Mashirika hayakuweza kuonyesha Mapato yaliyopatikana kwa mwaka. Kwa mfano Bodi ya Biashara ya Nje (BET) haikuweza kuonyesha mapato yaliyotokana na ukodishwaji wa kumbi za sherehe na hakukuwa na ripoti zilizoandaliwa kuonyesha siku ambazo kumbi zilikodishwa, jina la mteja, kiasi kilichopatikana, kiasi ambacho bado kinadaiwa na kiasi kilicholipwa kabla ya huduma.

Ilibainika pia, Mamlaka ya Maendeleo ya Mji wa Dodoma (CDA) kuwa minara 23 ya simu iliyowekwa katika Manispaa ya mji wa Dodoma haikusajiliwa wala kuwekwa kwa mikataba kulikopelekea kutokukusanywa kwa jumla ya shilingi milioni 212.862. Kwa upande mwingine Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) lilirekodi katika vitabu vya hesabu kiasi cha shilingi milioni 22 kama malipo tangulizi na kuyarekodi kama mapato ya mwaka kinyume na matakwa ya Viwango vya Kihisibu vya Kimataifa.

Pia, katika Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC) kulibainika kuwepo kwenye hesabu shilingi milioni 149.8 kama faida au hasara iliyotokana na tofauti ya sarafu ambazo hazikuwa na maelezo.

Ukaguzi wa Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC) uligundua kutokurekodiwa mapato ya ubia kati ya TBC na Kampuni ya Star Media ambayo ilitangaza matangazo yenye thamani ya shilingi milioni 36. Matangazo hayo hayakuwahi kuandikiwa ankara wala kulipwa. Pia kulikuwa na malipo yaliyoandikiwa ankara pungufu ya jumla ya dola za kimarekani 34,338.9 kwa SIBUKA FM na Clouds FM.

#### 5.1.5 Kutokuwepo Usuluhishi wa Mapato kati ya Vitabu vya Hesabu na Ripoti Nyingine za Mapato kwenye Mashirika ya Umma

Kutokufanya usuluhishi/uoanishi wa mapato katika vitabu vya hesabu na ripoti nyingine zinazorekodi mapato imeonekana ni tatizo katika Mashirika ya Umma. Katika Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Tanzania (TTCL) iligundulika kutokufanyika usuluhishi wa mapato ya vocha za malipo ya kabla kati ya leja na mtandao wa "Intelligence Network (IN)". Leja ilirekodi mapato jumla ya shilingi milioni 15.1 wakati IN ilirekodi jumla ya shilingi milioni 783.124 hivyo kusababisha tofauti ya shilingi milioni 767.997. Pia ilibainika TTCL kuwa na tofauti ya mapato kati ya leja na mfumo wa ankara ya kuhudumia wateja (Customer Care Billing Systems) (CCBS), ambapo CCBS ilirekodi jumla ya shilingi milioni 14,730,451,665 wakati

leja ilirekodi jumla ya Sh.14,761,033,248 hivyo kusababisha tofauti ya Sh.30,581,583 ambayo haikuweza kusuluhishwa ili kuwa na ulinganisho.

Katika Kampuni ya Usambazaji Maji ya Dar es Salaam (DAWASCO) ilionekana kuwepo tofauti ya Sh.220,943,143 iliyotokana na kutosuluhishwa kwa mapato yaliyorekodiwa na EDAMS ya Sh.836,993,737 na mapato ya kwenye leja ya Sh.616,050,594.

Katika Shirika la Ugavi wa Umeme la Tanzania (TANESCO) kumekuwa hakufanyiki usuluhishi wa mapato yanayotokana na mauzo kwenye matawi yake na mapato yaliyopo kwenye leja.

Shirika la Matangazo la Tanzania (TBC) limekuwa na tofauti ya Sh.10,888,214 kati ya leja na ripoti ya mauzo ya tawi la TBC Arusha.

#### **5.1.6 Kushuka kwa Makusanyo ya Faini za Kuingiza Magari Ambayo Hayajakaguliwa Nchini**

Mapato katika Mashirika yakilinganishwa na miaka iliyopita yameonekana kushuka kutokana na Menejimenti za Mashirika kukosa ubunifu wa kutafuta vyanzo vya mapato. Kwa mfano katika Shirika la Viwango la Tanzania (TBS) faini za kuingiza magari ambayo hayajakaguliwa kutoka nje zimeshuka kutoka Sh.134,600,156 mwaka uliopita hadi Sh.104,870,162 katika mwaka wa ukaguzi. Pungufu hiyo imetokana na waagizaji magari kugushi ankara za gharama ya uagizaji ili faini kuwa ndogo na TBS ikashindwa kudhibiti mwenendo huo katika vituo vya forodha vya bandari ya Dar es Salaam, Holili, Namanga na Tanga.

#### **5.1.7 Upotevu wa Umeme Wakati wa Uzalishaji na Usambazaji kwa Wateja**

Tathmini iliyofanyika katika Shirika la Ugavi wa Umeme la Tanzania (TANESCO) ilibainika kuwa shirika limeendelea kupata hasara ambayo imeongezeka kufikia asilimia 25 inayotokana na shirika kupoteza Mw 1,188 za umeme kati

ya Mw 4,831 zilizozalishwa. Hii inaonyesha kuwa bado kuna ongezeko kubwa la wateja wasio waaminifu, uandikaji wa ankara usio sahihi na uunganishaji umeme usio halali. Pia imeendelea kufahamika kuwa wateja waliokatiwa umeme wameendelea kupata huduma ya umeme iwapokuwa wana madeni ya jumla ya Sh.70,001,940.

## 5.2 Usimamizi wa Matumizi

Usimamizi wa matumizi ya umma ni suala ambalo hutokea kila penye mjadala kati ya Serikali, sekta ya umma na masuala ya maendeleo. Kwa miaka mingi Benki ya Dunia imewekeza raslimali nyingi katika kufanya tathmini ya matumizi ya umma na athari zake katika kudumisha maendeleo, yote hayo yanafanyika ili kuimarisha usimamizi wa matumizi ya umma.

Zifuatazo ni hoja zinazotokana na tathmini iliyofanyika juu ya usimamizi wa matumizi katika Mashirika na Taasisi za Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Septemba, 2009, 31 Disemba 2009 na tarehe 30 Juni, 2010.

### 5.2.1. Mapungufu Yaliyoonekana Katika Udhibiti wa Ndani

Usimamizi wa udhibiti wa ndani umekuwa haupewi kipaumbele katika baadhi ya Mashirika ya Umma, hali hii imepelekea matumizi kufanyika kinyume na taratibu. Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa manunuzi yaliyofanyika bila ya kuwepo hati za manunuzi (LPO) na manunuzi mengine kufanyika bila kujaza fomu za kuomba malipo kama ilivyoainishwa kwenye sheria za fedha za Mashirika ya Umma. Katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma (DUWASA) matumizi yenye jumla ya Sh.1,630,000 yalilipwa bila nyaraka za manunuzi (LPO) kupitishwa. Matumizi mengine yenye jumla ya Sh.9,498,000 yalilipwa bila kujaza fomu za matumizi.

### 5.2.2. Kutorejeshwa kwa Masurufu na Mikopo ya Mishahara ya Jumla ya Sh.3,153,386,768

Kanuni za fedha za Mashirika na Taasisi za Umma zinaainisha kurejeshwa kwa masurufu baada ya kukamilika

kwa safari husika. Masurufu mapya hayawezi kutolewa kama ya zamani hayajarejeshwa baada ya kuisha kwa kazi au safari iliyokusudiwa. Pia, kanuni za fedha huainisha masurufu yasiyorejeshwa yarejeshwe kwa kukata kwenye mishahara ya miezi inayofuata ya ofisa mhusika. Kaguzi zilizofanyika zilibaini kuwepo kwa mapungufu katika urejeshwaji wa masurufu. Masurufu mengi hayarejeshwi kwa wakati na masurufu hayo hayarejeshwi kupitia makato ya mishahara ya Maafisa wanaohusika kama taratibu zinavyotaka. Mapungufu yameonekana kwenye mashirika mengi na yameainishwa katika jedwali lifuatalo hapo chini:-

#### Jedwali 9: Masurufu Ambayo Hayajarejeshwa

Na.	Jina La Shirika	Kiasi (Sh)	Maelezo
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi (MUWASA)	9,335,000	Masurufu ambayo hayajarejeshwa.
2.	Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)	9,668,500	Masurufu ambayo hayajarejeshwa na wafanyakazi.
3.	Bodi ya Korosho ya Tanzania.	68,555,000	Masurufu ambayo hayajarejeshwa.
4.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza (MWAUWASA)	155,938,558	Masurufu ambayo hayajarejeshwa na wafanyakazi.
5.	Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)	671,578,801	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Sh. 66,122,922.90 Masurufu yaliyocheleweshwa kwa zaidi ya miezi 6 na 7.</li> <li>• Sh. 117,870,218.60 Masurufu mapya yaliyolipwa kwa watumishi ambao bado hawajarejesha masurufu ya zamani ya jumla ya Sh.487,565,660.12</li> </ul>
6.	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF)	9,390,000	Masurufu ambayo hayajarejeshwa.
7.	Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo	172,907,637	Masurufu ambayo hayajarejeshwa.



	Vidogo (SIDO)		
8.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Bima Tanzania (TIRA)	5,125,415	Masurufu ambayo hayajarejeshwa.
9.	Kituo cha Mikutano ya Kimataifa Arusha (AICC)	81,822,838	Masurufu ambayo hayajarejeshwa na watumishi, watumishi hao wakapewa tena masurufu mapya ya Sh.40,177,757 kabla ya kurejesha ya nyuma.
10.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma (MUWASA)	1,112,400	Masurufu ambayo hayajarejeshwa.
11.	Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)	1,572,935,455	Masurufu na malipo ya awali ambayo hayajarejeshwa.
12.	Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA)	40,775,255	Masurufu ya watumishi, ambayo hayajarejeshwa.
13.	Bodi ya Huduma za Maktaba	19,710,128	Masurufu ya watumishi, ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu.
14.	Kampuni ya Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL)	231,531,779	Masurufu ya muda mrefu ambao hayajarejeshwa kwenye hesabu za TCRA.
15.	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF)	9,390,000	Masurufu ya watumishi ambayo hayajarejeshwa.
16.	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania(TANESCO)	103,000,000	Malipo ya awali ambayo hayajarejeshwa.
Jumla		3,153,386,768	

### 5.2.3 Matumizi Yasiyo na Viambatanishi Timilifu

Kanuni za fedha katika kila shirika la Umma hutoa miongozo ya kuhakikisha kuwa malipo yote yanakuwa na viambatanisho vyote kikamilifu. Kaguzi zilizofanyika ziligundua jumla ya matumizi ya Sh.183,644,693 kutoka katika sampuli ndogo ya mashirika iliyochukuliwa ambayo hayakuwa na viambatanisho ipasavyo kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo.

#### Jedwali 10: Matumizi Yasiyo na Viambatanisho Timilifu

Na.	Jina la Shirika	Kiasi (Sh)	Maelezo
1.	Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)	11,646,800	Malipo mbalimbali yasiyo na risiti na malipo yasiyo na idhini.
2.	Shirika la Masoko Kariakoo	1,340,000	Malipo yaliyofanyika bila viambatanishi.
3.	Shirika la Hifadhi ya Mfuko wa Jamii (NSSF)	160,628,393	Malipo ambayo hayakuwa na viambatanisho vya ankara.
4.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano (TCRA)	10,029,500	Malipo ambayo hayakuwa na viambatanisho.
Jumla		183,644,693	

### 5.2.4 Udhhibiti wa Bajeti

- (i) Udhhibiti wa matumizi kulingana na bajeti umeonekana ni tatizo katika Mashirika na Taasisi za Umma kulikopelekea kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha za umma. Tofauti kubwa kati ya matumizi halisi na yaliyobajetiwa ilionekana baada ya matumizi halisi kuzidi bajeti zilizoidhinishwa. Kaguzi pia zilibaini makusanyo ya mapato ambayo yalikuwa nje ya bajeti ambayo yalitumika bila idhini za mamlaka ambapo ni kinyume na kanuni za fedha. Tofauti ya matumizi halisi na bajeti zilizoonekana katika baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma zilifikia kiasi cha Sh.3,708,904,890 kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo hapo chini:-

## Jedwali 11: Matumizi yaliyozidi Kiasi cha Bajeti

	Jina la Shirika	Kiasi (Sh)	Maelezo
1.	Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)	176,292,855	Matumizi yaliyozidi kiasi ambacho kilipitishwa kwenye bajeti.
2.	Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)	94,918,500	Mapato yaliyopatikana nje ya bajeti na kutumiwa bila kujumuishwa kwenye bajeti ya Baraza.
3.	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi (CRB)	44,039,000	Matumizi ambayo yalizidi bajeti.
4.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza (MWAUWASA)	192,813,243	Raslimali zilizonunuliwa nje ya bajeti iliyoidhinishwa.
5.	Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)	2,908,912,902	Mapato yaliyopatikana zaidi ya yaliyoidhinishwa kwenye bajeti na yakatumiwa bila kuidhinishwa na Bodi ambayo yanamhusisha Waziri wa Mali asili na Utalii.
6.	Bodi ya Biashara za Nje (BET)	9,553,390	Matumizi yaliyopo juu ya bajeti.
7.	Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC)	282,375,000	Matumizi yaliyozidi bajeti.
Total		3,708,904,890	

### (ii) Kutokuwepo kwa Udhhibiti wa Bajeti Katika Vitabu vya Hesabu

Katika Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ilionekana kuwa malipo hutoka katika bajeti tofauti na yanayoripotiwa katika kifungu kingine cha bajeti. Jumla ya Sh.41,824,050 ziliidhinishwa kutoka vifungu tofauti vya bajeti na zikaripotiwa kwenye vifungu vingine tofauti.

Tofauti hizo za Kuripoti zilikuwa katika Maeneo Yafuatayo:-

(a) Malipo ya posho ya kazi za ziada kwenye ufunguzi wa lango la Lodoare na Waziri wa Mali Asili na Utalii jumla

ya Sh.4,700,000, zililipwa kutoka katika kifungu cha kazi za ziada na ikaripotiwa kwenye uchapishaji na udurufu.

- (b) Malipo ya masurufu na posho za kujikimu Sh.11,481,250 zilirekodiwa kwenye fungu la kulipa ya Kampuni ya Antelope Tours.
- (c) Tiketi za kusafiria kiasi cha Sh.4,378,400 ziliripotiwa kwenye kifungu cha misaada na michango.
- (d) Posho za vikao na posho za kujikimu Sh.6,395,000 ziliripotiwa katika kifungu cha hafla za kitaifa.
- (e) Posho za kujikimu jumla ya Sh.4,670,000 ziliripotiwa kwenye kifungu cha manunuzi ya matairi ya magari.

Matumizi yaliyotajwa yasingefanyika kwa sababu vifungu husika vilikuwa vimeshaishiwa fedha. Hivyo, ilitakiwa kuwepo kwa maidhinisho mapya ya kuvihamishia fedha vifungu hivyo kutoka kwa Bodi.

(iii) Kutopitiwa kwa Hesabu Zinazoingizwa Kwenye Vitabu vya Mfumo wa Hesabu za Kampuni  
Katika Shirika la Ugavi la Umeme la Tanzania, baadhi ya hesabu zinarekodiwa kwa makosa kitendo ambacho kinaweza kusababisha udanganyifu na makosa kupita bila kugundulika. Kiasi cha Sh.13,000,000 ziliripotiwa kimakosa kama Sh.1,300,000,000 kwenye kifungu cha matumizi ya vikao. Pia kiasi cha Sh. bilioni 11 kinachohusu malipo kupitia barua ya mkopo (letter of credit) lakini kimakosa zikarekodiwa kama zimepokelewa katika akaunti ya makusanyo ya shirika ya NBC. Pia TANESCO shilingi milioni 101 zilirekodiwa mara mbili katika akaunti ya Mitambo ya Shirika.

#### 5.2.5. Malipo Yanayotia Shaka

Ukaguzi wa mahesabu ya Mashirika na Taasisi za Umma kwa mwaka husika umebaini matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 3.958 ambayo yanatia shaka. Malipo hayo

yamefanyika kinyume na Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005 na ulipaji wa posho kwa wajumbe wa bodi. Haya yalionekana wakati wa ukaguzi wa Mashirika yaliyoainishwa katika jedwali lifuatalo:-

### Jedwali 12: Malipo Yanayotia Shaka

Na.	Jina La Shirika	Kiasi (Sh)	Maelezo
1.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza (MWAUWASA)	33,394,400	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Malipo yaliyolipwa kama mafao ya ukomo wa kazi kwa wajumbe wa bodi tofauti na Hati ya Makubaliano (MoU) kipengele cha 4.4 (b) Sh.23,194,400</li> <li>• Posho ya Simu kwa wajumbe wa bodi ya Wakurugenzi Sh.9,000,000 ambayo ni kinyume na Kifungu 4.4(d) Hati ya makubaliano (MoU)</li> <li>• Shilingi 1,200,000 zinazolipwa kila mwaka bila kuainishwa kwenye sheria za fedha.</li> <li>• Matumizi ya bodi ya wakurugenzi yanayotokana na kuongezeka kwa vikao vya bodi.</li> </ul>
		118,950,600	

2.	Kampuni ya kusimamia Raslimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO)	3,727,500,000	Jumla ya Shilingi 3,727,500,000 zililipwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) bila mkataba wa kisheria.
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma (MUWASA)	1,138,553	Mikopo iliyotolewa kwa wafanyakazi ambao si wafanyakazi tena, kwa sababu za kustaafu, utoro na vifo.
4.	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	6,350,000	Mishahara ya awali iliyotolewa bila kujaza fomu za maombi.
5.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano (TCRA)	40,500,000	Malipo ya simu za mikononi na posho za simu kwa wajumbe wa bodi, kwa viwango vilivyopitishwa vya dola za marekani 600 na posho ya simu dola 350 kwa Mwenyekiti wa Bodi, dola 300 kwa Makamu Mwenyekiti na dola 250 kwa wajumbe wengine wa bodi, hii ni kinyume na taratibu zilizokubalika za utawala bora.
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga (TUWASA)	30,326,412	Vifaa vya ujenzi vilivyounuliwa lakini haikuthibitika kama vilipokelewa eneo la ujenzi.
Jumla		3,958,159,965	

**5.2.6 Ucheleweshwaji wa Kulipa Madeni ya Wateja kwa Wakati**  
Usimamizi mzuri wa fedha na matumizi ni pamoja na kuhakikisha kulipa madeni ya wateja kwa wakati. Ukaguzi wa mwaka huu ulibaini kuwa, Mfuko wa Bima ya afya (NHIF) malipo ya wateja huchukua muda mrefu kulipwa kinyume na Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya ya mwaka 1999 sehemu ya 28 ambayo imeanisha kuwa wanaotoa huduma za afya kwa wateja walipwe ndani ya siku 60 baada ya kuwasilisha madai. Shilingi 1,599,000,000 zilikuwa hazijalipwa kwa zaidi ya siku 60 wakati tunakamilisha ukaguzi wa mwaka 2009/2010.

Pia iligundulika kuwa Bodi ya Mkonge ya Tanzania imeshindwa kulipa deni la jumla ya Sh.21,032,610 kwa kampuni ya LAL Gereji, deni ambalo halijalipwa kwa zaidi ya miaka mitatu.

Shirika la Ugavi la Umeme la Tanzania (TANESCO) halijaweza kulipa deni la Shilingi 20,817,000 la Serikali.

Kutolipwa kwa madeni kwa wakati kuna sababisha hali ngumu ya kifedha kwa watoa huduma na kunaweza kupelekea huduma mbovu au za chini ya kiwango kwa wateja. Pia kunaweza kusababisha kupotea au kushusha uaminifu wa kukopesheka kwenye Mashirika na Taasisi za Umma husika.

#### **5.2.7 Kutozingatia Sera ya Mikopo ya Magari**

Sera ni kanuni au miongozo zinazoongoza maamuzi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mashirika ya Umma yametengeneza sera mbalimbali ikiwepo ya mikopo ya Magari. Wakati mwingine sera zilizowekwa hazifuatwi ipasavyo. Ukaguzi uliofanyika katika mwaka huu ulibaini mapungufu hayo kwenye baadhi ya Mashirika ya Umma, kwa mfano katika Mfuko wa Kuwekeza Tanzania (UTT) na katika Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB). Mashirika hayo yalikiuka taratibu za sera zilizowekwa. Sera zao zinataka magari yaliyonunuliwa kwa mkopo yaandikishwe kwa jina la shirika na kadi za magari zihifadhiwe na shirika hadi mkopo

utakapomalizika lakini utaratibu huu haufuatwi. Mfuko wa Kuwekeza Tanzania walitoa mikopo ya magari matano lakini magari hayo yaliandikishwa majina ya watumishi waliokopa, pia kadi za magari zilitunzwa na wakopaji wenyewe kinyume na taratibu. Kati ya magari hayo, gari moja lilikatiwa bima ndogo tofauti na sera inavyosema kuwa magari yote ya mkopo yakatiwe bima kubwa (comprehensive). Benki ya Uwekezaji Tanzania ilitoa mkopo kwa mfanyakazi mmoja lakini kadi ya gari ilitunzwa na mfanyakazi na gari liliandikishwa kwa jina la mfanyakazi huyo kinyume na utaratibu. Hii inaonyesha jinsi Mashirika yanavyojiweka kwenye hatari ya kupoteza fedha kwa kutofuata sera ilizojiweka.

#### 5.2.8. Kutokuwepo Udhhibiti wa Matumizi ya Kemikali za Maabara

Tathimini ya udhibiti wa kupokea na kutoa vifaa na Kikemikali za maabara kutoka stoo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kuona kama taratibu zinafuatwa, ilibaini kuwa hakuna udhibiti kwenye matumizi ya kemikali pamoja na kuwa kiasi kinachotakiwa kwa matumizi huidhinishwa na wakuu wa idara.

Pia, ilionekana kuwa malipo yaliyofanyika kununulia kemikali katika mwaka huu yaliongezeka kufikia Shilingi bilioni 6.7 kutoka shilingi bilioni 2.3 za mwaka uliopita ikiwa ni ongezeko la asilimia 200. Hali hii inaonyesha kuwa ongezeko limetokana na kutokuwepo udhibiti mzuri wa Kemikali hizo. Kutokuwepo kwa udhibiti wa kemikali za maabara kutoka stoo za hospitali hupelekea Hospital ya Muhimbili kuingia gharama za ziada kununua kemikali ambazo mara nyingi zinatumiwa isivyopaswa.

#### 5.2.9 Kutokuwepo kwa Usuluhishi wa Mishahara Kutoka Hazina na ile ya Mashirika ya Umma

Fedha za mishahara ya watumishi wa Mashirika ya Umma kwa kawaida hutolewa na Hazina kufuatia orodha ya mishahara inayoandaliwa na kuwasilishwa na Shirika husika. Ukaguzi ulibaini kuwepo kwa tofauti kati ya mishahara



inayotoka Hazina na ile inayoandaliwa na baadhi ya Mashirika ya Umma. Katika Hospitali ya Muhimbili, Tume ya Ushindani wa Biashara (FCC) na Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo mishahara ilikuwa inalipwa tofauti na ile inayotoka Hazina. Hali hii inaweza kupelekea udanganyifu kwenye malipo ya mishahara ikiwa ni pamoja na kulipwa kwa mishahara hewa.

#### 5.2.10. Kutotumia Vitabu vya Magari

Usimamizi wa raslimali za Umma ni jukumu lililokabidhiwa kwa menejimenti za kila Shirika la Umma. Magari ni mojawapo ya raslimali muhimu katika Mashirika ya Umma inayotoa huduma muhimu ya usafiri. Hivyo, magari haya kama yakitumika bila usimamizi mzuri itapelekea kuwepo kwa matumizi makubwa ya fedha za Umma kwani gharama za mafuta na vipuri zitaongezeka. Hata hivyo, kuna njia zilizowekwa kudhibiti matumizi mabaya ya magari ya Umma ikiwemo vitabu vya kurekodi mafuta ya magari (log books) kama ilivyoainishwa katika sheria za fedha za mashirika ya Umma.

Ilibainika kwenye Shirika moja la Umma kuwa vitabu vya kurekodi matumizi ya mafuta ya magari havikuwepo kabisa na hakukuwepo na taarifa zozote za matumizi ya magari kwa mfano kama kila gari linatumia mafuta kiasi gani kwa kipindi fulani ili kurahisisha tathmini ya matumizi ya kila gari. Udhibiti wa gharama za mafuta ya magari umekuwa ni tatizo kubwa katika Mashirika ya Umma hapa nchini.

#### 5.2.11. Malipo ya Faini ya Sh.24,890,480 kwa Kucheleweshwa Michango ya Pensheni (PPF) ya Watumishi

Makato ya watumishi kwa ajili ya pensheni yanatakiwa kulipwa kwenye mifuko husika kama ilivyoainishwa kwenye sheria na ukiukwaji wake huwa husababisha adhabu ya faini. Katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi ilionekana katika Shirika la Usambazaji Maji la Dar es salaam (DAWASCO) lililipa jumla ya Shilingi 24,890,480 kama faini ya kucheleweshwa kulipa makato ya wafanyakazi ya PPF. Matumizi haya yanaoneka kuwa ni upotevu wa fedha za

umma, kwani ni gharama ambayo ingeweza kuepukika kama malipo ya Pensheni yangelipwa mapema na fedha hizo zingetumika kufanya shughuli nyingine za maendeleo ya shirika badala ya kulipa faini.

#### 5.2.12. Kutokuwepo kwa Udhibiti wa Vifaa Vilivyonunuliwa kwa Kutooanisha Akaunti za Wazabuni

Ukaguzi uliofanyika kuangalia malipo yaliyofanyika kwa wagavi katika mwaka husika kuna baadhi ya mapungufu yalibainika. Katika Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO) ilionekana kuna malipo yaliyolipwa kabla kwa bidhaa ambazo zilishapokelewa tayari lakini bado hazijaingizwa kwenye hesabu. Pia kuna malipo ya vipuli vilivyotakiwa kupelekwa katika kituo cha Umeme Mafia yaliyolipwa kwa Kampuni ya Wartisila Euro 237,411 tangu mwezi Mei 2009 lakini vipuri hivyo hadi kufikia Juni 2010 vilikuwa bado havijapokelewa.

Kwa upande mwingine TANESCO haifuatili akaunti za wateja zenye salio hasi kwa jumla ya Shilingi bilioni 2.4 ikionyesha kuwa mauzo mengi bado hayajarekodiwa kwenye akaunti za wateja. Pia Shirika halifanyi uoanishi wa idadi ya wateja waliopo kwenye mfumo wa (Hi-Affinity) na idadi halisi ya wateja waliopo kwenye ripoti za utendaji. Licha ya hayo, Shirika halioanishi mafuta yanayotumika kuendeshea mitambo na yale yanayorekodiwa katika vitabu vya hesabu ambapo tofauti ya shilingi 3.4 bilioni ilionekana.

## SURA YA SITA

### USIMAMIZI WA SHERIA ZA MANUNUZI NA MIKATABA

#### 6.0 Utangulizi

Tanzania imefanya mabadiliko makubwa ya sheria ya Manunuzi na kupelekea kuanzishwa kwa sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Ili kuhakikisha manunuzi yanafuata taratibu katika Tanzania, kifungu Na. 44 (2) cha sheria ya manunuzi kinamtaka mkaguzi wa Taasisi yeyote ya umma kuainisha katika ripoti yake ya mwaka kama taratibu zote za manunuzi zimefuatwa katika Taasisi husika.

Vile vile, kanuni ya 31 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Bidhaa, ujenzi, huduma zisizo za kiushauri na uuzaji wa mali za Umma kwa zabuni), inamtaka Mkaguzi wa Hesabu wa Taasisi ya Umma kuainisha katika ripoti yake ya mwaka kama manunuzi yaliyofanyika yalifuata taratibu za kuitisha zabuni na katika ushindani na ununuzi au uuzaji unatakiwa kuidhinishwa kwanza na bodi ya zabuni.

Kwa kuzingatia mamlaka niliyopewa katika vifungu vya sheria vilivyoainishwa hapo juu, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu imekagua taratibu za manunuzi kwa mashirika 122 katika ukaguzi wake wa kawaida wa mwaka wa fedha 2009/2010. Hivyo, sura hii inajumuisha matokeo na mapendekezo ya kaguzi zilizofanywa na Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi husika. Pia, Mamlaka ya Udhiliti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa manunuzi uliofanyika katika Mashirika 91 ambayo matokeo yake yamejumuishwa kwenye sura hii.

Pia sura hii, inatoa majumuisho ya taarifa za ukaguzi na utekelezaji wa mikataba iliyoonekana muhimu kutolewa taarifa katika mwaka husika. Ukaguzi wa mikataba ulifanyika sambamba na ukaguzi wa kawaida wa hesabu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Septemba, 2009, 31

Disemba, 2009 na 30 Juni 2010. Matokeo ya zoezi la ukaguzi wa mikataba iliyoingiwa na Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali yameainishwa sehemu ya pili ya sura hii.

#### 6.1 Usimamizi wa Manunuzi

Kulingana na Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004, neno manunuzi lina maana, kununua, kukodisha, au vinginevyo kupata bidhaa, ujenzi au huduma inayofanywa na taasisi kwa kutumia fedha za umma, kwa niaba ya Wizara au Idara ya Serikali au Shirika la Umma na ikijumuisha na kazi zote zinazohusiana na kupatikana kwa bidhaa au huduma ikiwa ni pamoja na kuainisha mahitaji, kuteua na kutangaza zabuni na kutoa mikataba. Yafuatayo ni mambo ambayo yalionekana kuwa na kasoro kwenye ukaguzi.

##### 6.1.1 Tofauti Kati ya Namba za Zabuni na Maelezo yake

Mpango wa manunuzi wa mwaka unatumika kama waraka wa awali unaotoa taarifa za zabuni. Ukaguzi umebaini kuwa namba za zabuni na maelezo ya ndani yanayohusu zabuni husika yalitofautiana na taarifa zilizochapishwa kwenye matangazo ya zabuni na zile zilizopo kwenye mkataba. Hali hiyo ilisababishwa na udhaifu katika kutunza kumbukumbu katika baadhi ya mashirika. Kwa mfano, katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha tulibaini zabuni Na. AE/029/2009-2010/14 kwa ajili ya kutengeneza kompyuta, lakini namba hiyo hiyo ilitumika kutangaza zabuni kwa ajili ya kununua huduma ya bima, wakati mkataba uliosainiwa ulihusu huduma ya kufanya usafi.

##### 6.1.2 Kitengo cha Manunuzi Kuteua Kamati ya Tathmini Badala ya Kamati hiyo Kuteuliwa na Mkuu wa Taasisi au Afisa Masuuli

Katika ukaguzi wa manunuzi, tulibaini kuwepo kwa teuzi za kamati za kutathmini zilizofanyika kinyume na taratibu. Imebainika kuwa, kamati hizo ziliteuliwa na kitengo cha manunuzi badala ya watendaji wakuu na Maafisa Masuuli wa baadhi ya mashirika kinyume na kifungu Na. 33(e) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kinachompa Mtendaji Mkuu mamlaka ya kuteua kamati ya tathmini.

- 6.1.3 Kutosambazwa kwa Mikataba Iliyotolewa kwa Wazabuni  
Katika ukaguzi imebainika kuwa baadhi ya Makatibu wa Bodi za Zabuni wa Mashirika ya Umma hawakupeleka mikataba kwa mamlaka husika kama vile PPRA, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na kitengo cha Ukaguzi Maalum cha Wizara ya Fedha kama inavyotakiwa na Kanuni Na. 96(2) ya Waraka wa Serikali Na. 97 wa mwaka 2005.
- 6.1.4 Zabuni Zilizoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi  
Ukaguzi uliofanyika katika Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CAMETRAC) umebaini kuwepo kwa zabuni iliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi badala ya Bodi ya Zabuni kinyume na sheria. Zabuni hiyo ilikuwa kwa ajili ya kumpata mshauri mwelekezi. Bodi ya Wakurugenzi katika kikao chake cha 78 kilichofanyika tarehe 6 Oktoba 2008 ilipitisha maombi ya uongozi ya kumpatia zabuni Wakala wa Ujenzi Tanzania (TBA) kama mshauri mkuu. Hivyo, mnamo tarehe 14 Oktoba 2008 bodi ya zabuni iliridhia maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi kwa kumpitisha mshauri huyo. Katika mazingira hayo, Bodi ya Zabuni haikufanya maamuzi yake kwa uhuru kwani maamuzi yao yaliingiliwa na Bodi ya Wakurugenzi.
- 6.1.5 Mapungufu katika Vitengo vya Manunuzi  
Sheria ya Manunuzi ya Umma inataka kila Shirika la Umma kuanzisha Kitengo cha Manunuzi. Hata hivyo ilibainika kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma hayana vitengo vya manunuzi, na mengine yameanzisha vitengo hivyo kama kamati badala ya idara zinazojitegemea. Hali hiyo ilijitokeza katika mashirika ya CBT, COASCO, KUWASA, MTUWASA, NCAA, SIDO na NEMC. Pia katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara, kitengo cha ununuzi kinasimamiwa na Mhasibu badala ya kusimamiwa na Mtaalamu wa ugavi. Kitendo hiki ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Manunuzi za Mwaka, 2004.

#### 6.1.6 Wakurugenzi wa Mashirika Kukaimisha Madaraka kwa Wajumbe wa Bodi za Zabuni

Imebainika kuwa baadhi ya Wenyeviti wa Bodi za Zabuni wakati wanakaimu nafasi za Wakurugenzi Wakuu walihusika moja kwa moja kwenye vikao vya Bodi za Zabuni na kufanya maamuzi ya kupitisha zabuni, kuteua kamati ya tathmini na kutoa zabuni kinyume na Kanuni ya 33 (3) ya tangazo la Serikali Na. 97 na Kanuni 87 (3) ya tangazo la Serikali Na.98, ambazo zinakataza kukaimisha kazi ya mkuu wa taasisi kwa wajumbe wa Bodi za Zabuni au Kitengo cha Manunuzi. Hali hiyo ilijitokeza katika mashirika ya DUWASA, NSSF na TCRA.

#### 6.1.7 Kutokuwepo Kamati ya Kupokea Bidhaa

Kanuni ya 127 ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 inataka Afisa Masuuli kuteua kamati ya uangalizi na upokeaji wa bidhaa pindi zinaponunuliwa, ambayo inawajibika kukagua, kuhesabu na kukubali bidhaa kama ilivyoainishwa kwenye makubalino ya mkataba. Imebainika kutoteuliwa kwa kamati husika kwa kipindi husika katika Mashirika ya MPRU, MTUWASA, na NCAA.

#### 6.1.8 Majukumu Yanayokinzana Katika Kutayarisha na Kutunza Mikataba

Katika Sheria ya Manunuzi ya Umma, makatibu wa zabuni wanajukumu la kutayarisha na kutunza mikataba. Hii inatakiwa kufanyika kama ilivyoainishwa kwenye kifungu cha 35 (k), (l) na (n) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004. Hata hivyo, katika Mashirika ya Umma, imebainika kuwa mikataba inatunzwa na Kitengo cha Sheria hivyo kupelekea mikataba kutopitishwa na Bodi ya Zabuni kama ilivyoainishwa kwenye Sheria. Vile vile, hali hivyo ilipelekea mikataba minane katika Shirika la Hifadhi ya Ngorongoro kutosainiwa wakati zabuni zilizotolewa zimeisha muda wake.

#### **6.1.9 Utunzaji Dhaifu wa Kumbukumbu za Manunuzi Katika Mashirika**

Baadhi ya mashirika yameonekana kuwa na kawaida ya kuwa na udhaifu mkubwa katika kutunza kumbukumbu za manunuzi unaosababishwa na ukosefu wa taaluma katika kutunza kumbukumbu, ukosefu wa nafasi katika ofisi za vitengo vya manunuzi na kupoteza nyaraka bila sababu za msingi. Madhara ya hali hiyo ni kuwa na manunuzi yasiyofuata Sheria, udokozi wa mali na kupotea kwa mali za umma.

#### **6.1.10 Udhaifu katika Uendeshaji wa Bodi za Zabuni**

Katika Mfuko wa Afya ya Jamii, Bodi ya Zabuni inaundwa na mameneja ambao sio wakuu wa idara. Sheria ya Manunuzi ya Umma inataka wajumbe wa bodi wawe wakuu wa idara ambao wanaweza kuripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mkuu. Kwa sababu ya udhaifu huo, Bodi ya Zabuni imeshindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo kama vile kutosimamia mpango wa mwaka wa manunuzi, kupitisha mahitaji ya manunuzi kutoka idara hitaji na kushindwa kutumia njia za ununuzi sahihi zilizoainishwa kwenye Sheria na pia kutumia njia zisizokuwa za ushindani katika kununua bidhaa na huduma.

#### **6.1.11 Kubadili Njia ya Kununua ili Kukwepa Vifungu vya Sheria**

Katika Mfuko wa Afya ya Jamii, utawala ulinunua kompyuta 50 na UPS zenye thamani ya shilingi milioni 79.90. Manunuzi hayo yalifanywa kwa njia ya ushindani wa wazi (Competitive Quotation) ambapo mzabuni aliyekuwa na bei ya chini alikuwa ni kampuni ya Computech ICS (T) Ltd iliyotoa bei ya chini kiasi cha shilingi milioni 100.33. Ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Zabuni zilibadili idadi ya bidhaa wakati wa kutoa zabuni hii ili thamani iwe chini ya kiwango kilichopitishwa kisheria cha shilingi milioni 80 kwa ushindani wa wazi. Kwa mtazamo huu, Bodi ya Zabuni ilitenda kinyume na Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004.

#### 6.1.12 Kutokuwepo kwa Uhuru wa Kamati ya Tathmini

Katika ukaguzi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania umebaini kuwa Kitengo cha Ununuzi kiliamuru Kamati ya Tathmini kurudia kutathmini zabuni kwa kuwa kamati iliwaacha wazabuni wawili ambao hawakutumiza vigezo katika mchakato wa awali. Kitengo cha manunuzi kilikuwa na mtazamo kuwa sababu zilizotumika kuwatoa wazabuni hao kwenye ushindani zilikuwa ndogo wakati Kamati ya Tathmini ikishikilia msimamo wake kuwa sababu zilikuwa za msingi. Baada ya misimamo hiyo, Kitengo cha Manunuzi kilifanya tathmini yake na kuwaingiza wazabuni waliokuwa wametolewa na kamati, hivyo, kufanya mmoja wa wazabuni kushinda na kupitishwa na Bodi ya Zabuni tarehe 27/11/09. Mapendekezo ya Kitengo cha Zabuni yalifanywa kinyume na Sheria inayotaka Bodi ya Zabuni kuidhinisha mapendekezo ya kamati ya tathmini na sio vinginevyo.

#### 6.1.13 Ufuatiliaji wa Kaguzi za Manunuzi Katika Mashirika 19 Uliofanywa na PPRA

Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004, inaipa uwezo Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA) kufanya ukaguzi wa manunuzi na kutoa taarifa baada ya ukaguzi. Katika mwaka huu wa ukaguzi, PPRA haikufanya ukaguzi mpya badala yake ilifuatilia mapungufu yalionekana katika Taasisi na Mashirika 25 yaliyokaguliwa katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 na 2008/2009 ili kuona kama mapungufu yaliyoonekana yalishapatiwa ufumbuzi na Mashirika husika. Matokeo ya ufuatiliaji yalionyesha uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi kwa kiwango kikubwa kwa wastani wa asilimia 50 kwa mwaka 2007/2008 na asilimia 55 kwa mwaka 2008/2009, wastani wa jumla ni asilimia 73 ambao ni juu ya wastani wa asilimia 69 uliokuwa umetarajiwa.

Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati (EWURA) ilipata asilimia 98 za uzingativu wakati Bodi ya Utalii ilipata asilimia 40 za uzingativu. Matokeo pia yalionyesha kuwa viashiria vya uzingativu 13 vilivyowekwa kupima uzingatiaji wa sheria, mashirika yalipata chini ya asilimia 50 katika viashiria vitano muhimu vya msingi vya uzingativu kati ya



viashiria 13 ambavyo ni kuanzishwa na uundwaji wa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PMU), uandaaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka, kutangaza mikataba iliyotolewa kwa mwaka, utunzaji wa kumbukumbu na uhakiki na udhibiti wa thamani. Kwa upande mwingine, mashirika yalionekana kufanya vizuri zaidi juu ya wastani katika viashiria 8 vilivyobaki vya uzingativu wa sheria ya manunuzi.

Nashauri kuwa Menejimenti za Mashirika ya Umma ziongeze jitihada za kuhakikisha kuwa sheria ya manunuzi inazingatiwa kikamilifu.

## 6.2 Usimamizi wa Mikataba

Kulingana na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004, mkataba wa manunuzi unamaanisha leseni, kibali au makubaliano ya aina yoyote yaliyoingiwa na taasisi za umma na wazabuni au mjenzi unaotaokana na mchakato wa ununuzi kwa ajili ya kununua bidhaa, ujenzi au kupata huduma. Mambo yafuatayo yalitokana na ukaguzi wa mikataba kwa kipindi husika.

### 6.2.1 Kuchelewa kwa Utekelezaji wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa

Mapitio ya nyaraka za mradi wa maboresho ya vitambulisho vya Taifa umebaini kuwa Baraza la Mawaziri liliidhinisha mpango wa kutekeleza mradi huu mwaka 2007, ambapo mradi ulipangwa kuanza mwezi Julai 2008 hadi Disemba 2009 kwa awamu mbili ambazo ni; kuchambua gharama za uendeleshaji wa Mamlaka ya Taifa ya Vitambulisho na kutambua gharama halisi za utekelezaji wa mradi.

Pia tulibaini kuwa Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Mambo ya Ndani iliidhinisha zabuni kwa ajili ya kazi hii tarehe 20 Septemba, 2008 baada ya hapo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilisaini mkataba na Gotham International Limited tarehe 13 Januari, 2010 kutoa huduma ya Ushauri kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa vitambulisho vya Taifa kwa kutumia teknolojia ya SMART CARD. Jumla ya gharama za

mkataba ni dola za kimarekani milioni 9 na muda wa mkataba ni miaka mitano (5) kuanzia tarehe 14 Januari, 2010.

Kulingana na kifungu cha 19.2(1) cha mkataba, kiasi cha dola za kimarekani milioni 2.7 sawa na shilingi milioni 3.6 zililipwa kwa kampuni ya Gotham International Limited baada ya mshauri kuandaa ripoti ya upembuzi wa mradi na waraka wa mapendekezo (RFP) ambapo makampuni 154 yaliwasilisha nyaraka za zabuni. Baada ya uchambuzi, wazabuni 54 waliteuliwa na baadae wazabuni 5 walichaguliwa. Kamati ya tathmini ya Zabuni iko kwenye mchakato wa kuchagua kampuni moja itakayoshinda kuwa mkandarasi wa kuchapisha Vitambulisho vya Taifa vinavyotarajiwa kuanza kutengenezwa kwa majaribio mwezi Machi, 2011.

Mshauri ameweza kuandaa na kuwasilisha mpango wa vitambulisho vya Taifa, ajira za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Sera na Mpango wa Mawasiliano. Hata hivyo, tumegundua kwamba, mradi umechukua muda wa mwaka mmoja tangu tarehe ambayo Bodi ya Zabuni ya Wizara itoe idhini na kusaini mkataba na hakuna sababu za msingi zilizotolewa.

Ucheleweshwaji huu una athari katika kufikia malengo ya shughuli za mradi. Tunashauri kwamba menejimenti iongeze juhudi kuongeza kasi ya mradi wa Vitambulisho vya Taifa kwa manufaa ya raia wa Tanzania.

#### 6.2.2 Udhaifu Katika Usimamizi wa Mikataba-NSSF

Shirika la Hifadhi ya Jamii NSSF lilianza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma awamu ya pili bila kusaini mkataba na Serikali. Pia ilibainika kuwa katika mkataba huo NSSF wanachukulia mradi huo kama mkopo kwa Serikali. Hata hivyo, mkataba wa awamu ya kwanza kifungu cha 2 (i) kinaonyesha kuwa mkataba huo ni wa kujenga, kumiliki na kuhamisha majengo. Kwa mpango huo NSSF itamiliki majengo hayo kwa miaka kumi wakati wakipokea kodi

kutoka Serikali. Tumebaini kuwa pamoja na makubaliano hayo, majengo ya awamu ya kwanza yalishakamilika na kuanza kutumika mwezi Septemba 2008. NSSF hawajaweza kupata kodi yoyote toka Serikalini. Hata hivyo, thamani halisi ya mikataba haijulikani kwani awamu ya pili ya ujenzi ilianza bila kuwa na mkataba, hivyo haki na wajibu wa pande zote mbili haikuweza kujulikana.

#### 6.2.3 Mkataba wa Manunuzi ya Mafuta

Katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma (DUWASA) kulifanyika manunuzi ya mafuta na vilainisho yenye thamani ya shilingi milioni 152.44 kutoka kwa mzabuni Nassoro Petrol Station bila kuwa na mkataba. Pia Kampuni hiyo haikuorodheshwa kwenye orodha ya wazabuni wa mwaka wa Mamlaka na Mzabuni huyu hakupatikana kwa njia za ushindani. Pia, DUWASA walinunua pikipiki kumi (10) kutoka kampuni ya Kishen Enterprises kwa gharama ya shilingi milioni 15 mwezi Oktoba 2009. Imebainika kuwa pikipiki mbili zimeharibika hivyo kuleta wasiwasi kama thamani ya fedha ilizingatiwa kwenye ununuzi huo. Vilevile, DUWASA waliingia mikataba yenye thamani ya shilingi milioni 75.52 na kampuni ya Plasco Limited kwa ajili ya kununua mabomba. Imebainika kufikia mwisho wa mwaka yaani tarehe 30 Juni 2010 mabomba yenye thamani ya shilingi milioni 11.09 ndiyo yaliyokuwa yamepokelewa kutoka kwa mzabuni, hivyo kupelekea DUWASA kununua mabomba ya kiasi cha shilingi milioni 131.77 kutoka kwa wazabuni wengine ambao hawakuwepo kwenye orodha ya wazabuni.

#### 6.2.4 Kusaini Mikataba Visivyo Halali

Katika shirika la Hifadhi Tengefu Baharini ilibainika kuwa mikataba yote ilisainiwa na mwenyekiti na katibu wa Bodi ya Zabuni kinyume na kifungu 33(h) cha Sheria ya manunuzi kinachotamka kuwa, kiongozi wa shirika ndiye mwenye dhamana ya kusaini mikataba yote kwa niaba ya Shirika.

#### 6.2.5 Udhaifu Katika Usimamizi wa Mikataba Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ilifanya manunuzi ya bidhaa na huduma vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.02 kutoka kwa wazabuni kumi na watatu bila ya kuwa na mikataba. Hali hiyo inaiweka mamlaka kwenye hatari ya kupoteza kesi kama ingetokea kutokuelewana kati yake na wazabuni. Vilevile, mikataba sita iliisha muda wake tarehe 31 Disemba 2009 bila kuhuishwa wakati wazabuni waliendelea kufanya kazi mpaka ilipofika mwisho wa mwaka wa fedha 2009/10 bila kuwa na mikataba. Pia, mkataba wa ununuzi wa jenereta mbili, tipa moja, boza la maji na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Nainokanoka haikutekelezwa kulingana na makubaliano ya mkataba.

#### 6.2.6 Usimamizi wa Mikataba Katika Shirika la Utangazaji Tanzania

Ukaguzi wa usimamizi wa mikataba katika Shirika la Utangazaji Tanzania umebaini kuwepo kwa mkataba ulioingiwa kati ya Shirika na Kampuni ya RRS-Global Communication mwezi Aprili 2008 kwa ajili kulipia huduma za Setilaiti. Ilibainika kwamba mkataba huu haukupitia kwenye utaratibu wa zabuni na zaidi mzabuni alifunga Setilaiti mwezi Septemba 2010 bila ridhaa ya TBC. Hivyo, TBC haikuwa angalifu katika kutathmini uwezo wa mzabuni kabla ya kupatiwa mkataba.

## SURA YA SABA

### USIMAMIZI WA RASLIMALI

#### 7.0 Utangulizi

Raslimali ni mali zinazomilikiwa na Taasisi au Shirika kwa ajili ya matumizi yake ya kila siku katika kuendesha shughuli zake. Raslimali zinajumuisha mali zinazoshikika na zisizoshikika ambazo taasisi inazimiliki. Raslimali zinajumuisha mali zisizohamishika, mitambo, vifaa mbalimbali, uwekezaji, fedha taslimu, madeni yanayodaiwa, akiba ya vifaa, mifumo ya ndani ya kompyuta, tovuti na malipo tangulizi.

Sura hii ni muhimu kwa sababu ya changamoto zinazoyakabili Mashirika ya Umma kwa kufuatilia na kusimamia raslimali. Pia pamoja na changamoto hizo, hapa ni mahali ambapo kuna uwezekano mkubwa wa wafanyakazi ambao sio waaminifu wanaoweza kufanya ubadhilifu wa mali za umma.

Kwa mwaka huu wa ukaguzi, tumeainisha masuala ambayo ni muhimu Serikali na Bunge liweze kuyatolea maelekezo ya namna nzuri ya kuyatekeleza.

#### 7.1 Kutokuwa na Umiliki Halali wa Mali

Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya Mashirika hayana umiliki halali wa mali zake, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa hati miliki.

Pia, Mashirika mengi yameonekana kutokuwa na umiliki halali wa magari na pikipiki. Kukosekana kwa hati miliki kunafanya mkaguzi ashindwe kuthibitisha umiliki wa mali hizo. Kwa mfano CDA haikuwa na umiliki wa viwanja ishirini na moja ambavyo haina hati miliki. Pia hali hiyo ilijitokeza katika kaguzi za mashirika ya NARCO, NEMC, na Bodi ya Korosho.

- 7.2 Uchakavu wa Majengo Katika Mashirika**  
Mashirika ili yaweze kuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi, majengo yake yanatakiwa kuwa kwenye hali nzuri. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa hali isiyoridhisha kwenye baadhi ya majengo yanayomilikiwa na Mashirika na Taasisi za Umma. Hali hiyo, ilidhihirika katika majengo mengi ya Bodi za Mazao na jengo la Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO). Inashauriwa kuwa mashirika na Serikali zitenge fedha mahususi ili kukarabati majengo chakavu ya Mashirika ya Umma.
- 7.3 COASCO Kutokuwa na Umiliki wa Jengo lake Mbeya**  
Katika ukaguzi wa Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), ilibainika kuwa uongozi haujapata hati za jengo lake lililopo eneo la Sabasaba ambapo ilibainika kuwa jengo hilo lilinunuliwa kutoka iliyokuwa Bodi ya Taifa ya Uzalishaji na Usambazaji wa Tumbaku ambapo kiwanja pia sio cha COASCO. Kukosekana kwa hati miliki imeleta shaka kuhusu umiliki halali wa kiwanja na jengo lililojumuishwa kwenye raslimali za Shirika.
- 7.4 Kutokuwepo kwa Bima kwa Ajili ya Raslimali**  
Katika usimamizi wa raslimali, mali zote za Mashirika ya Umma zinatakiwa kuwa na bima ili kujikinga dhidi ya majanga ya moto na athari zingine. Bima ni aina ya mfumo ambao hutumiwa kwa ajili ya kuinga mali za wahusika na majanga yasiyotarajiwa. Ilibainika kuwa katika mashirika mengi hayajaweza kuweka bima ya mali zao kama vile magari kwa sababu ya ufinyu wa ruzuku wanazopewa kutoka Serikalini.
- 7.5 Mifumo Hafifu ya Kutunza Kumbukumbu za Raslimali za Mashirika na Taasisi za Umma**  
Uhakiki wa daftari la mali zisizohamishika umebaini upungufu katika taarifa za msingi zinazotakiwa kuwepo kwenye daftari husika kama vile nambari ya mali, jina la muuzaji, tarehe ya kununuliwa n.k. Vilevile, baadhi ya mali zilizokuwa kwenye daftari ziliwekwa kwenye kundi moja hivyo haikuwa rahisi kutambua gharama halisi ya kila mali

zilizonunuliwa, hivyo kuwa vigumu kupata ulinganifu wa taarifa za kwenye daftari na hesabu.

#### **7.6 Mapungufu Kwenye Usimamizi wa Bidhaa Hodhi**

Kulingana na Aya Na. 6 (c) ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa Namba 2 (2009) bidhaa hodhi ni mali inayomilikiwa kwa ajili ya matumizi ya kuzalishia au kutumika kwa ajili ya kutoa huduma. Kwa ufafanuzi huo, ni wazi kuwa bidhaa hodhi ni mali muhimu ambazo zinahitaji utunzaji mzuri kama ilivyo fedha katika Mashirika ya Umma. Katika usimamizi wa mali hodhi, imebainika kuwa baadhi ya Mashirika, hayakufanya hesabu za mali katika stoo zao mwisho wa mwaka, pia baadhi ya mashirika yalihesabu bidhaa hodhi bila kuwepo kwa wakaguzi wa ndani, wakati mwingine mali hizo huhesabiwa bila kuwepo nyaraka za kutunzia kumbukumbu, kutofanyika kabisa kwa hesabu za mali hodhi na kutokuwa na thamani halisi za mali zote zilizopo bohari kwa ajili ya kuingizwa kwenye vitabu vya hesabu vya shirika husika.

#### **7.7 Madeni ya Muda Mrefu Yasiyolipika**

Uhakiki wa madeni katika Mashirika mbalimbali ya umma umebaini kuwepo kwa madeni ya muda mrefu ambayo hayajalipwa na wateja. Kwa mazingira haya, fedha za Mashirika husika zimeshikiliwa na wateja hivyo kuathiri Mashirika hayo. Hivyo, Mashirika ambayo yana madeni ya muda mrefu yako kwenye hatari ya kukosa fedha za kuendeshea shughuli zao za kila siku. Kwa mfano, Kampuni ya Magazeti Tanzania, ilikuwa na madeni kiasi cha shilingi . bilioni 2.0 kati ya mauzo ya mwaka yenye jumla ya shilingi bilioni 8.8 ambayo ni sawa na asilimia ishirini na tatu (23%) ya mauzo yote ya mwaka.

#### **7.8 Kukosa Hati Miliki ya Jengo la Kahawa**

Uhakiki wa umiliki wa jengo la Kahawa House linalomilikiwa na Bodi ya Kahawa Tanzania na kutumika kama makao makuu mjini Moshi, pia hutumiwa kama chanzo kikuu cha mapato kwa Bodi hiyo, tumekuta halina hati miliki. Upembuzi wa kina umebaini kuwa hati miliki hiyo

inashikiliwa na Benki ya Exim kama dhamana ya mkopo wa mashaka iliosainiwa tarehe 6 Machi 2003. Maelezo ya uongozi ni kwamba kesi ya kudai hati hiyo ipo mahakama ya ardhi. Inashauriwa kuwa bodi ihakikishe kuwa inakamilisha hatua hizo na kupata hati hiyo ya jengo hilo.

#### 7.9 Viwango vya Uchakavu Visivyokuwa Sahihi

Tafsiri na utekelezaji wa viwango vya uhasibu vya kimataifa katika uandaaji wa hesabu umebainika kuwa na mapungufu katika baadhi ya Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali. Manthalani, kiwango cha Uhasibu cha Kimataifa Namba 16 kinaeleza kuhusu namna ya kuweza kukadiria kiwango cha uchakavu kwa mitambo na mashine zinginezo. Upembuzi wa sera za kukadiria kiwango cha uchakavu katika mashirika umebaini kuwepo kwa mkanganyiko wa namna ya kukadiria viwango hivyo vya uchakavu. Aya ya 57 ya kiwango cha 16 inatoa mwongozo kuhusu namna ya kukadiria kiwango cha uchakavu wa mali za muda mrefu.

Kiwango kinaweka wazi kuwa muda wa matumizi wa raslimali unategemea manufaa yatakayopatikana kutokana na matumizi ya raslimali na yatategemea makadirio ya kitalaamu na pia maamuzi binafsi kwenye kutumia kiwango na kuzingatia uzoefu. Pia, aya ya 33 ya kiwango Namba 8 inataka kufanya makadirio ambayo ni ya uhakika. Ukaguzi ulibaini kuwa Mashirika mbalimbali ya umma yanatumia viwango tofauti tofauti, ambavyo vimeleta tofauti pia katika kuandaa hesabu.

Tunashauri Msajili wa Hazina wakishirikiana na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) kufanya utafiti kuhusu kiwango cha kutoza uchakavu ili kupendekeza makadirio viwango halisia katika Mashirika yote umma.

#### 7.10 Magari na Pikipiki Kutokuwa na Umiliki

Uhakiki wa mali zinazomilikiwa na mashirika umebaini kuwa baadhi ya mashirika yanamiliki mali zilizotolewa kama misaada kutoka kwa wafadhili au Serikalini. Uhakiki umebaini kuwa magari na pikipiki hizo hazikupata usajili wa namba za mashirika husika badala yake zilikuwa kwenye



usajili wa Miradi (DFP) na Serikali (ST). Hali hiyo imeyanyima mashirika haki ya kumiliki raslimali hizo pamoja na kuwa raslimali hizo zinatumiwa kwenye shughuli zao za uzalishaji. Tunashauri Serikali kuhamisha umiliki wa mali zote zilizopo kwenye miradi uwe kwenye mashirika hayo.

- 7.11 Usimamizi wa Uwekezaji katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii  
Mapitio ya uwekezaji katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umebaini kuwa mfuko uliwekeza hisa katika vitega uchumi vitano vyenye thamani ya shilingi bilioni 14.5 bila kuwepo na matarajio ya kupata gawio kwa siku za baadae. Upembuzi zaidi umebaini kuwa hakuna kampuni hata moja ambayo imetoa gawio kwa vipindi vyote toka Mfuko uwekeze. Tunashauri uongozi uchukue hatua za haraka kuhakikisha wanaondokana na uwekezaji kwenye kampuni zisizotoa gawio.
- 7.12 Uwekaji Kumbukumbu Sahihi wa Hesabu na Ardhi  
Kiwango cha mahesabu cha kimataifa namba 16 kinaelezea wazi kuwa ardhi na majengo ni mali tofauti na hivyo zinatakiwa zihesabiwe tofauti hata kama zimenunuliwa pamoja. Majengo yanahesabiwa kuwa na muda maalumu wa matumizi wakati raslimali hizo zinatumiwa na kuwa chakavu. Uhakiki wetu umebaini kuwa hesabu zilizoandaliwa hazikuzingatia umiliki wa ardhi kwani tumebaini kuwepo kwa ardhi na majengo ambayo kumbukumbu zao zimewekwa kwa pamoja kwenye mahesabu ya baadhi ya Mashirika ya Umma.
- 7.13 Uthamini wa Mali, Mashine na Mitambo  
Imekuwa ni sera za baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma kueleza kwenye maelezo ya hesabu kuwa mitambo na mali zingine ziwekewe kumbukumbu vitabuni kwa kutumia gharama halisi na kuzingatia uthamini ili kupata thamani ya kuingiza kwenye vitabu. Viwango vya Hesabu vya Kimataifa vinataka uthamini ufanyike kwenye mali kwa angalau kipindi cha miaka mitatu hadi mitano ili kuonyesha thamani halisi. Uhakiki uliofanywa katika baadhi ya Mashirika

umebaini kuwa uthamini wa mali haujafanyika kwa wakati kama inavyoelekezwa na viwango hivyo vya kiuhasibu vya kimataifa. Tunashauri uthamini wa mali ufanyike kwa wakati ili kupata thamani inayowiana na hali halisi.

## SURA YA NANE

### USIMAMIZI WA RASLIMALI WATU

#### 8.0 Utangulizi

Usimamizi wa raslimali watu ni kazi ya kitaasisi inayoshughulikia masuala yahasuyo watu kama vile malipo ya ajira, ajira, usimamizi wa utendaji kazi, maendeleo ya kitaasisi, usalama, hali njema, marupurupu ya kazi, hamasa ya kazi, mawasiliano, utawala, mafunzo na mambo mengine ya kiutumishi.

Matokeo ya kaguzi mbalimbali zilizofanyika mwaka yalibainisha kwamba baadhi ya Mashirika ya Umma yana mapungufu kadhaa kuhusiana na usimamizi bora wa raslimali watu. Mapungufu yaliyobainika ni kama yalivyoonyeshwa hapa chini;

- Majalada ya wafanyakazi hayakuwekewa taarifa mpya za taarifa za wafanyakazi.
- Wafanyakazi wengine, hasa wale wafanyao kazi kwa mikataba hawakuwa na mikataba ya kazi.
- Uajiri ulifanywa bila uwazi na bila kufuata masharti yaliyopo ya Utumishi wa Umma, kama vile kuajiri pasipo kutangaza nafasi ya kazi ikusudiwayo.
- Mashirika mengi yalikuwa na miundo/miongozo ya utumishi iliyopitwa na wakati
- Baadhi ya mashirika yalikuwa mpango maalumu wa mafunzo na maendeleo ya wafanyakazi.
- Kumekuwa na mapungufu mbalimbali katika tathmini za utendaji kazi wa wafanyakazi.
- Kumekuwa na upungufu wa wafanyakazi, hasa katika nafasi muhimu za kiutendaji.
- Ucheleweshwaji wa malipo ya mishahara hadi kusababisha malimbikizo ya mishahara na ulipaji wa mishahara chini ya kima cha chini cha mishahara.

- Ucheleweshwaji au kutowasilishwa kwa makato mbalimbali kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya kisheria toka kwa wafanyakazi.

Madhara ya mapungufu haya yanajumuisha kiwango kikubwa cha wafanyakazi kuacha kazi, kuwa na ari ndogo ya kufanya kazi na hatimaye kiwango kidogo cha matokeo ya kazi.

Mapungufu hayo ni kama inavyoonyeshwa katika aya zifuatazo hapa chini.

- 8.1 **Majalada ya Wafanyakazi Kutorekebishwa kwa Wakati**  
 Kila taasisi huajiri na kuhifadhi kumbukumbu za wafanyakazi wake. Wafanyakazi ni miongoni mwa raslimali muhimu na zenye thamani sana katika taasisi yeyote. Kama zilivyo raslimali nyingine, wafanyakazi ni raslimali ambazo lazima zitumike ipasavyo kufikia kiwango cha juu cha utendaji. Utunzaji mzuri wa kumbukumbu za wafanyakazi unaweza kuleta mchango mkubwa katika kufikia lengo hilo kwa kuhakikisha taarifa zinazopatikana zinaweza kusaidia kutoa maamuzi na kulinda haki za Mashirika ya Umma na wafanyakazi. Zaidi ya hayo, kwa sababu mifumo ya watumishi huunganishwa kwa ukaribu na mifumo ya mishahara, utunzaji wa kumbukumbu za wafanyakazi utaleta matokeo chanya katika usimamizi wa mifumo ya mishahara na bajeti nzima ya taasisi. Mfumo wa kumbukumbu za wafanyakazi lazima usimamiwe ipasavyo, aidha uwe katika mazingira ya utunzaji kumbukumbu kwa majalada au katika mazingira ya kutumia mfumo wa kompyuta.

Uchambuzi wa majalada ya wazi na ya siri kutoka Mashirika mbalimbali ya umma umebaini kuwa baadhi ya majalada ya wafanyakazi hayakuwekewa taarifa mpya zihusuzo mabadiliko yaliyojitokeza katika masharti ya ajira. Kwa mfano nyongeza mbalimbali za mishahara hazikuwa na uthibitisho wa viambatanishi husika kama vile barua za nyongeza za mishahara na barua za kupandishwa vyeo.

Mapungufu mengine yaliyogundulika kuhusiana na kumbukumbu za wafanyakazi ni kutokuwepo fomu za kiapo cha utunzaji siri, fomu za utambulisho, fomu za tathmini ya utendaji kazi, barua za ajira, barua za kukubali ajira au kupandishwa vyeo na fomu za kumbukumbu binafsi za mfanyakazi.

Kutoka sampuli ya Mashirika na Taasisi za Umma yaliyokaguliwa, Mashirika yafuatayo yamebainika kuwa na mapungufu mbalimbali yahasuyo uwekaji taarifa katika majalada ya wafanyakazi nayo ni: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), SUMATRA, Mfuko wa Uwekezaji Tanzania (UTT) na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

## 8.2 Miongozo ya Utumishi Iliyopitwa na Wakati

Ufuatiliaji wa miongozo ya ajira ya baadhi ya Mashirika ya Umma umebaini kuwa baadhi ya miongozo ya utumishi ya mashirika hayo ina mapungufu na imepitwa na wakati kwa kuwa baadhi haikujumuisha wafanyakazi wote, sifa, wajibu na majukumu ya viongozi waandamizi. Hali hiyo imegundulika katika Shirika la Viwango la Taifa ambapo, miongozo ya ajira ya shirika haukuendana na muundo wake wa kiuongozi. Baadhi ya nafasi zilizoonyeshwa kwenye muundo wa uongozi wa shirika hazikuonyeshwa kwenye miongozo ya ajira kwani sifa, wajibu na majukumu ya nafasi hizo hazikutafsiriwa katika mwongozo ya ajira. Upungufu huu unajenga hofu juu ya uwezekano wa utimizaji wa majukumu ya kazi na wajibu wa watumishi husika.

Uchambuzi zaidi katika Taasisi ya Utafiti wa Misititu Tanzania umebaini kwamba, mwongozo wa ajira ulitengenezwa tangu mwaka 2004, hata hivyo hapakuwa na mabadiliko yeyote yaliyofanywa ya kujumuisha mabadiliko ya hivi karibuni yahasuyo malipo ya ujira wa watumishi watafiti na utawala uliotolewa na Serikali na hivyo kuufanya mwongozo huo kupitwa na wakati na kutoendana na hali halisi ya mabadiliko katika usimamizi wa raslimali watu.

### 8.3 Mafunzo kwa Wafanyakazi

Haja ya kuboresha uzalishaji inakubalika ulimwenguni kote, hivyo uhitaji wa mafunzo bora na yenye tija ni suala la wazi na lazima. Uboreshaji huo umelazimika zaidi kutokana na maendeleo ya dunia ya kisasa kuwekeza katika mafunzo. Pia, Mashirika ya Umma yanafahamu umuhimu wa kuwapa mafunzo wafanyakazi na hivyo Mashirika na Taasisi za Umma yanawajibika kutoa mafunzo hayo katika ngazi zote. Wafanyakazi pia, wana wajibu wa kujiendeleza zaidi kimasomo ili kujiongezea elimu na ujuzi zaidi. Katika uchambuzi wetu juu ya mafunzo yatolewayo na Mashirika ya Umma imebainika kuwa mafunzo mengi yaliyofanywa hayakutanguliwa na mpango maalumu wa mafunzo na pale ambapo palikuwepo na mpango maalum wa mafunzo, mpango huo haukufuatwa ipasavyo.

Imebainika kwamba, baadhi ya Mashirika ya Umma hayatoi mafunzo kwa wafanyakazi wake na hivyo kusababisha utendaji kazi mbovu. Baadhi ya mifano kuthibisha hali hiyo ni matokeo ya uchambuzi wa mafunzo katika Mfuko wa Bima ya Afya uliofanywa mwaka huu wa ukaguzi ambapo baadhi ya mafunzo ambayo hayakuwekwa kwenye bajeti na mpango wa mafunzo, yalitolewa kwa baadhi ya wafanyakazi. Baadhi ya wafanyakazi walipatiwa mafunzo ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja na shughuli za kila siku za mfuko, wakati wafanyakazi wengine walihudhuria mafunzo zaidi ya mara moja huku wengine katika idara hiyo hawakuhudhuria mafunzo yeyote.

Pia uchambuzi wa Usimamizi wa Raslimali watu katika Bodi ya Kahawa Tanzania, ulibaini kuwa, bodi hiyo haina mpango wa mafunzo na ujengaji uwezo wa wafanyakazi, hali inayothibitishwa na kutokuwepo hata mfanyakazi mmoja aliyehudhuria mafunzo ya muda mfupi au mrefu.

Uchambuzi wa Usimamizi wa Raslimali watu katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga ulibaini kuwa hapakuwa na mpango mahsusni wa mafunzo ya muda mfupi

au mrefu kuonyesha ni mfanyakazi yupi na ni lini atatakiwa kuhudhuria mafunzo.

Mashirika mengine ya umma yaliyo na mapungufu juu ya utoaji wa mafunzo yanajumuisha Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara (MTUWASA) ambapo kulikuwa na ukosefu wa ratiba maalum ya mafunzo. Kwa upande mwingine, wafanyakazi na Shirika la Bima la Taifa hawakupatiwa mafunzo yoyote.

#### 8.4 Mapungufu Yaliyogundulika Katika Tathmini ya Utendaji Kazi wa Wafanyakazi

Tathmini ya utendaji kazi hupima ubora na kiasi cha utendaji kazi. Tathmini hufanywa siyo tu juu ya utendaji kazi wa wafanyakazi bali pia juu ya uwezekano wa kuwaendeleza. Malengo ya msingi ya tathmini hii, ni - kupima utendaji kazi uliopita, kutambua mahitaji ya mafunzo, kupanga na kukubaliana juu ya malengo na viwango vya kazi vijavyo, na kuwezesha utimizaji wa malengo hayo.

Uchambuzi wa mifumo ya upimaji utendaji kazi wa wafanyakazi, ulibaini udhaifu ambao unahitaji kufanyiwa kazi kwa ajili ya maendeleo ya Mashirika ya Umma husika. Kushindwa kufanya hivyo kunaweza kuleta ugumu wa kupima utendaji kazi wa mfanyakazi mmoja mmoja, kutathmini malipo stahili ya wafanyakazi, upandishwaji cheo, kushushwa cheo, nyongeza za mwaka, utimizaji na upangaji wa wafanyakazi. Zaidi ya hayo, wafanyakazi hawatoweza kupata mrejesho wa utendaji kazi wao na hivyo kushindwa kutambua maeneo yanayohitajika kuboreshwa.

Katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Moshi (MOUWASA), ukaguzi ulibaini kwamba fomu za tathmini za utendaji kazi katika mwaka huu wa ukaguzi na miaka ya nyuma hadi 2004 hazikuweza kuonekana katika majalada ya watumishi, ikionyesha kwamba tathmini hiyo haikufanyika kabisa. Udhaifu mwingine uliogundulika wakati wa

uchambuzi wa mfumo wa upimaji kazi wa TANAPA, ambapo kwa miaka mitatu wakaguzi walishauri uanzishwaji wa mfumo wa wazi wa tathmini ya utendaji kazi (OPRAS) lakini mpaka wakati wa kuandaa taarifa hii, menejimenti haikuweza kuanzisha mfumo huo. Zaidi ya hayo, hata mfumo wa siri wa tathmini wa utendaji kazi utumikao sasa haufanyiki ipasavyo kwa kuwa tathmini chache zilizofanyika kutumia mfumo wa siri wa tathmini. Ni sehemu A tu ya fomu ya tathmini ndiyo ilijazwa kiukamilifu na ofisa aliye chini ya utathmini huo wakati sehemu nyingine za fomu hiyo zikiwa zimejazwa kiupungufu au kutojazwa kabisa.

Udhaifu mwingine wa kiujumla uliogundulika ulikuwa ni ule wa Mashirika ya Umma kufanya tathmini ya utendaji wa kazi kwa wafanyakazi wa kada ya kawaida tu kwa kulinganisha utendaji kazi dhidi ya wajibu wa kazi zilizotolewa lakini hakuna tathmini yoyote iliyofanywa kwa watumishi wa ngazi ya menejimenti. Mashirika mengine ya umma yaliyoshindwa kufanya tathmini za utendaji kazi kwa mwaka yanajumuisha MTUWASA na Bodi ya Kahawa Tanzania ambapo tathmini ya utendaji kazi ilifanywa kwa mara ya mwisho mwaka 1997/1998.

#### 8.5 Upungufu wa Wafanyakazi

Uchambuzi wa mahitaji ya wafanyakazi wa Mashirika mbalimbali ya umma katika kipindi cha ukaguzi, ulibaini kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yana matatizo ya upungufu wa wafanyakazi katika nafasi muhimu za mashirika hayo. Mifano ya mashirika yenye matatizo hayo ni Mamlaka ya Ujenzi wa Mji Mkuu Dodoma (CDA) ambapo baadhi ya nafasi kama zilivyo katika mfumo wa kiuongozi wa shirika zilionekana kuwa wazi na baadhi zilikuwa zikishikiliwa kwa kukaimu kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu. Upungufu mwingine wa wafanyakazi ulionekana katika uchambuzi wa usimamizi wa raslimali katika Bodi ya Korosho Tanzania ambapo nafasi nyeti tisa (9) za kazi zilikuwa wazi.



Katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara, takribani nafasi nane (8) za mfumo wa kiuongozi wa mamlaka zilikuwa wazi. Katika mashirika mengine, kulionekana kuna upungufu lakini hapakuwa na tathmini ya mahitaji halisi ya wafanyakazi ya kutambua idadi ya wafanyakazi inayohitajika kwa kila fani, hii ni hali halisi iliyoonekana katika Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Mashirika mengine yaliyokumbwa na upungufu wa wafanyakazi ni Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi za Tiba Muhimbili (MUHAS) ambapo kati ya mahitaji 546 ya wafanyakazi walimu na wasio walimu, ni nafasi 404 tu ndizo zilikuwa zimejazwa na kuacha upungufu wa wafanyakazi 142. Kampuni ya Reli Asset ambayo ilikuwa na mfanyakazi mmoja tu katika kitengo cha manunuzi dhidi ya mahitaji ya wafanyakazi 6 na pia katika Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kanda ya Kigoma kulikuwa na ukosefu wa mhasibu.

Zaidi ya mapungufu hayo, mashirika mengi ya umma hayakuwa na mpango wa kurithishana madaraka.

#### 8.6 Ucheleweshaji wa Ulipaji wa Mishahara na Malipo ya Mishahara Chini ya Kima cha Chini

Katika uchambuzi wa Usimamizi wa raslimali watu juu ya suala la ulipaji mishahara, imefahamika kwamba baadhi ya Mashirika ya Umma hayatoi umuhimu wa kutosha juu ya haki ya wafanyakazi ya kulipwa mishahara. Imegundulika kuwa mwaka huu wa ukaguzi takribani wafanyakazi 7 wa zamani wa TAMKO - Kibaha hawakulipwa mishahara yao ya jumla ya shilingi milioni 2.6. Hivyo, wito unatolewa kwa mashirika ya umma kuhakikisha mishahara ya wafanyakazi inalipwa kwa wakati.

Upungufu mwingine uhusuo malipo ya mishahara ulibainika katika Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) ambapo malipo ya mishahara chini ya kima cha chini yalilipwa. Upungufu huu ulionekana Nyanza Glass Works Limited ambapo malipo ya mishahara ya mlinzi yalikuwa shilingi elfu 63 hali

mshahara wa kima cha chini cha mlinzi makao makuu ya ya shirika yakiwa shilingi laki 205.8.

Imegundulika pia kwamba katika Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), mishahara ya jumla ya shilingi milioni 77.3 ya wafanyakazi 8, ambao walipandishwa vyeo na menejimenti katika tarehe mbalimbali kuanzia Januari, 2006 hawajalipwa mishahara. Hata hivyo, mishahara yao ilibaki kama malimbikizo hadi wakati wa ukaguzi wa mwaka 2009/2010. Zaidi ya hayo, kiasi hicho hakikuingizwa kwenye vitabu vya hesabu za kituo kama madeni.

Ni ukweli kwamba, ucheleweshwaji wa malipo ya mishahara au ulipaji wa mishahara chini ya kima cha chini ni ukiukwaji wa sheria za kazi na mahusiano bora ya ajira.

- 8.7 Ajira za Kazi Kutofanywa kwa Uwazi**  
Uchambuzi wa Usimamizi wa raslimali watu katika mashirika mbalimbali ya umma, ulibaini kuwa kulikuwa na mashirika ambayo ajira za kazi zilifanywa pasipo kufuata taratibu za uwazi kama vile kutangaza nafasi zilizo wazi. Hali hii inawanyima haki watu wengine kushindana. Mfano mzuri ulibainika TANAPA ambapo menejimenti ilitangaza nafasi 19 za kazi kwa uwazi lakini kufikia mwisho mwa zoezi la uajiri wafanyakazi 32 zaidi walijajiriwa. Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa jumla ya wafanyakazi walioajiriwa na TANAPA katika mwaka huu wa ukaguzi bila nafasi zake kutangazwa zilifikia 181.
- 8.8 Ucheleweshwaji wa Uwasilishaji wa Michango ya Pensheni na Makato Mengine ya Kisheria**  
Uchambuzi wa masuala ya uhasibu na utoaji taarifa kuhusiana na uwasilishwaji wa michango ya pensheni kwenye mifuko ya hifadhi kama vile NSSF na PPF, ulibaini kuwa ucheleweshwaji wa kuwasilisha michango hiyo. Ucheleweshwaji huo ni ukiukwaji wa sheria na taratibu zilizopo kama vile sheria mbalimbali za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (NSSF Act, PPF Act etc) ambazo madhara yake ni uwezekano wa kuyaingiza mashirika husika katika hatari ya

kutozwa fidia au adhabu na hivyo kusababisha matumizi yasiyo ya lazima ambayo huleta matokea hasi kwenye bajeti na hatari ya kupoteza sifa njema katika jamii, ambapo shirika lingetegemewa kufuata sheria na taratibu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wa wafanyakazi, madhara makubwa kuhusiana na ucheleweshwaji wa michango ya pensheni ni ucheleweshwaji wa malipo ya uzeeni, kwani mifuko hulipa mafao ya kustaafu kulingana na michango ya mwanachama.

Mifano ya mashirika ya umma ambayo aidha yalishindwa au yalikosa ushahidi wa kuwasilisha michango hiyo ya pensheni na makato mengine ya kisheria ni Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma (DUWASA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA).



## SURA YA TISA

### UTAWALA BORA

#### 9.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea masuala ya utawala bora yaliyobainika kuwa muhimu kubainishwa katika taarifa hii kama yalivyoelezwa kwa kina katika taarifa za Mashirika na Taasisi za Umma husika kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Septemba, 2009, 31 Disemba, 2009 na 30 Juni 2010.

Utawala bora ni muunganiko wa mfumo na muundo wa kiutawala unaotekelezwa na Bodi za Wakurugenzi ili kutoa taarifa, maelekezo, kuongoza na kusimamia mali za shirika, mikakati na sera katika kufikia malengo ya shirika. Dhana kuu ya utawala bora ni kuhakikisha kuwa kuna uwajibikaji wa viongozi katika Shirika kwa kutumia njia ambazo zitaweza kupunguza au kuondoa tatizo la kukwamisha misingi mikuu ya utawala bora ikijumuisha Bodi ya Wakurugenzi, Kamati ya Ukaguzi, Uongozi wa Shirika, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na Wakaguzi wa Nje.

Katika ripoti iliyopita, tuliibua masuala na kutoa mapendekezo mbalimbali muhimu ili kuboresha mifumo ya utawala bora ambayo kama yangalitekelezwa kikamilifu yangelikuwa yamepelekea tija na ufanisi zaidi katika utendaji wa mashirika ya umma. Mapendekezo hayo ni pamoja na:-

- i. Masuala muhimu ya ufanisi wa Bodi za Wakurugenzi.
- ii. Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi wenye nyadhifa mbalimbali katika jamii hivyo kushindwa kutimiza wajibu wao wa kusimamia ipasavyo.
- iii. Utaratibu wa uteuzi wa Wakurugenzi Watendaji wa Mashirika ya Umma na Wenyeviti wa Bodi unaofanywa na mamlaka moja hivyo kupelekea mvutano wa kiutendaji.
- iv. Ucheleweshaji wa kuteua bodi za wakurugenzi pale muda wa bodi unapoisha.

- v. Kutotekeleza mapendekezo yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- vi. Kukosekana kwa mifumo ya uwajibikaji wa Bodi za Wakurugenzi.
- vii. Kukosekana kwa mwongozo wenye kuleta uwiano katika stahili za wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi katika Mashirika ya Umma.
- viii. Udhaifu mbalimbali wa kiutendaji katika baadhi ya Bodi za Mashirika
- ix. Utata katika muundo wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania.
- x. Suala la Wabunge kuwa Wajumbe wa Bodi mbalimbali kwenye Mashirika ya Umma.
- xi. Masuala ya uundaji wa kamati za ukaguzi.
- xii. Masuala ya utendaji katika vitengo vya ukaguzi wa ndani katika Mashirika ya Umma.

Hata hivyo, tumebaini kwa masikitiko makubwa kuwa sehemu kubwa ya mapendekezo yaliyotajwa hapo juu yamekuwa hayatekelezwi na Serikali na hivyo kupelekea hali ya kiutendaji katika Mashirika ya Umma kubaki kama ilivyokuwa awali na kupelekea kuendelea kuwepo na hoja za ukaguzi katika mwaka huu. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa Mashirika ya Umma yanasimamiwa na kuongozwa kikamilifu katika kutekeleza majukumu yake na hivyo kutimiza matarajio ya umma wa Watanzania.

#### 9.1 Ufanisi wa Bodi za Wakurugenzi

Bodi ya Wakurugenzi ni chombo cha wajumbe wa kuteuliwa ambacho kinasimamia shughuli za taasisi. Ingawaje chombo hiki kina majina mbalimbali, lakini kwa kifupi kinaweza kuitwa bodi.

Majukumu ya bodi yanaongozwa na mamlaka na wajibu unaowekwa kwake na Serikali. Masuala haya yanaelezwa kwa kina katika sheria za uanzishwaji wa mashirika. Sheria za uanzishaji wa mashirika pia zinaeleza kiwango cha Wajumbe wa Bodi, namna ya upatikanaji wao na namna ya kukutana kwao. Ingawaje bodi ni msingi wa uwepo wa

Mashirika ya Umma, katika nchi yetu zimeonekana kuwa na mapungufu yafuatayo:-

**9.1.1 Kukosekana kwa Miongozo ya Utendaji wa Bodi**

Bodi za Wakurugenzi katika Mashirika ya Umma ni chombo muhimu katika kuhakikisha kuwa utendaji wa Mashirika ya Umma unatimiza matarajio ya uanzishwaji wake. Ili kulifikia hili, kila Bodi ya Wakurugenzi inatakiwa kuwa na miongozo (charter) ya utendaji ambayo pamoja na mambo mengine itaelezea kwa kina majukumu ya bodi na namna ya kutekeleza majukumu hayo. Tumbaine kuwa mashirika mengi ya umma hayana miongozo ya utendaji kwa bodi zake za wakurugenzi na hivyo kuwafanya wajumbe wa bodi nyingi kutoelewa kwa kina nafasi zao na wajibu wao.

**9.1.2 Ushiriki wa Wajumbe wa Bodi na Wabunge katika Shughuli za Utendaji za Kila Siku za Mashirika ya Umma**

Katika ripoti zetu zilizotangulia, tumekuwa tukisisitiza suala la wabunge kutokuwa Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma. Hata hivyo, Serikali haijachukua hatua za dhati kutekeleza hili na madhara yameonekana dhahiri katika baadhi ya mashirika ambapo Wabunge na Wajumbe wa Bodi wengine wamekuwa wakishiriki katika shughuli za kiutendaji za mashirika kwa mwamvuli wa ujumbe wa bodi au Kamati za Kudumu za Bunge. Kwa utaratibu wa namna hii, ni wazi kuwa kanuni za utawala bora za kutenganisha madaraka kati ya Serikali na vyombo vya usimamizi (Bunge) inadhoofishwa. Ili tuweze kuwa na mashirika yanayosimamiwa kikamilifu na ambayo yatatoa matumaini kwa utendaji unaotarajiwa, muingiliano huu kati ya Serikali na Bunge kama ilivyobainika katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (TPDC) ni vema ukasitishwa.

**9.1.3. Uhuru wa Bodi za Wakurugenzi Katika Kusimamia Mashirika ya Umma**

Shirika la Umma ni Taasisi ambayo inaanzishwa kutimiza majukumu maalumu ya kisekta; na mara nyingi yakiendeshwa kibiashara kwa niaba ya Serikali. Mamlaka ya

kuongoza shughuli za taasisi hizi, imekasimiwa kwa Bodi za Wakurugenzi ambazo zinakuwa na jukumu la kusimamia menejimenti ya mashirika hayo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa ingawa Bodi za Wakurugenzi zina mamlaka ya kutunga sera na hata kuamua namna ya uwekezaji wa mitaji katika mashirika, yapo matukio yanayoonyesha kuingilia kwa Serikali katika maamuzi haya ikiwa ni pamoja na utoaji maelekezo ya kisera, uwekezaji na uingiaji mikataba mikubwa. Masuala kama haya siyo mazingira mazuri ya utendaji wa Mashirika ya Umma kwa sababu pale ambapo Serikali inaingilia mamlaka iliyoikasimu kwa Bodi ya Wakurugenzi, basi mfumo mzima wa uwajibikaji unakuwa dhaifu. Baadhi ya mashirika yaliyoonekana kuwa na muingiliano wa Serikali kwa kiasi kikubwa ni pamoja na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Shirika la Umeme (TANESCO), Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

#### 9.1.4 Udhaifu katika Utendaji wa Bodi za Wakurugenzi

Tumebaini kuwepo kwa udhaifu katika utendaji wa Bodi za Wakurugenzi katika kuyasimamia baadhi ya Mashirika ya Umma. Udhaifu iliobainika unatokana na baadhi ya wajumbe wa bodi kutofahamu vyema wajibu na mamlaka waliyonayo hasa katika kuimarisha kiwango cha uwajibikaji miongoni mwa menejimenti na watumishi wote wa Mashirika ya Umma.

Sehemu kubwa ya udhaifu uliobainika unatokana na masuala yafuatayo:-

- i. Kutokuwepo kwa Programu za Kujenga Uwezo wa wajumbe wa bodi: Mashirika mengi ya umma yamekuwa hayana utaratibu wa kuwa na mafunzo kwa wajumbe wanya wa bodi mara wanapoteuliwa ili kuwajengea uwezo kuhusiana na majukumu yao na pia kupata ufahamu wa taasisi husika pamoja na shughuli



inazozifanya kitu ambacho kingechangia kuboresha utendaji wao wa kazi.

- ii. Kutokuwepo kwa Hadidu za Rejea kwa Bodi Mpya: Imebainika kuwa, bodi nyingi za Mashirika ya Umma hazina hadidu za rejea zinazoelekeza ni nini na vipi bodi husika zinatarajiwa kutekeleza majukumu yao katika kuendeleza shirika husika. Upungufu huu unaonekana kuwa kikwazo kikubwa katika kuzifanya bodi ziwajibike kwa matokeo ya utendaji wa Shirika la Umma husika.
- iii. Vikao vya Bodi za Wakurugenzi: Ingawa Sheria nyingi za Mashirika ya Umma zinahitaji bodi kuwa na vikao angalau vinne (Kimoja kila robo mwaka) kukiwa na ongezeko pale itakapolazimu, tumebaini kuwa katika baadhi ya mashirika bodi zimekuwa zikifanya vikao vingi zaidi bila sababu za lazima kufanya hivyo kitu kinachoongeza gharama za uendeshaji wa shughuli za bodi. Kwa mfano, katika baadhi ya mashirika tumebaini wajumbe wa bodi wakipendekeza kuahirisha vikao ambavyo vimeishaanza hadi wakati mwingine kwa sababu ndogo sana ambazo zingeweza kupatiwa ufumbuzi na vikao kuendelea au kuahirisha baadhi ya ajenda kutokana na haraka ya mwenyekiti au baadhi ya wajumbe wenye nguvu vikaoni. Pia, hatukuweza kupata ushahidi wa kufanyika tathmini ya utendaji wa bodi kila mwaka unapoisha ili kuweza kuona utendaji wa nyuma, wa leo na wa kesho katika shirika. Mfano mzuri ni katika Mamlaka za Maji ikiwemo ya jiji la Mwanza na Baraza la Sanaa la Taifa.
- iv. Wajibu Katika Usimamizi wa Fedha na Utoaji Taarifa: Ukaguzi umebaini kuwa Bodi za Wakurugenzi bado hazijatekeleza kikamilifu wajibu wake wa usimamizi wa fedha na utoaji taarifa hali iliyopelekea baadhi ya mashirika kuchelewa kuandaa na kuwasilisha hesabu zake kwa ajili ya ukaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 Kifungu cha 31. Kutokana na kukosekana kwa uzingatiaji wa sheria hiyo,

kiasi cha mashirika 51 kati ya mashirika 166 sawa na asilimia 31.7 ndiyo yaliyoweza kuwasilisha hesabu zao kwa ajili ya kukaguliwa na taarifa zao kuripotiwa katika mwaka uliopita huku tatizo hili likiongeza mzigo wa kazi za ukaguzi zaidi katika mwaka unaofuata.

## 9.2 Kamati ya Ukaguzi

Kamati ya ukaguzi ni kamati ya Bodi ya Wakurugenzi ambayo shughuli yake kuu ni kuisaidia bodi katika kutekeleza jukumu lake la usimamizi wa uwajibikaji katika shirika hasa katika maeneo ya:-

- i. Ukamilifu wa hesabu za shirika na utaratibu mzima wa uwekaji kumbukumbu za mapato na matumizi pamoja na mfumo wa udhibiti katika shirika;
- ii. Utendaji kazi wa wakaguzi wa ndani;
- iii. Ushirikishaji wa wakaguzi wa nje katika kukagua hesabu za shirika,
- iv. Uzingativu wa matakwa ya kisheria pamoja na taratibu zilizowekwa; pamoja na
- v. Tathmini ya taratibu za menejimenti katika kubaini na kutatua hatari zilizopo katika shughuli za shirika.

Ingawaje kamati hii ina jukumu muhimu sana katika kuhakikisha kuwa ukaguzi wa ndani na wa nje unafanyika kama inavyotakiwa na hatari za kiutendaji zinabainishwa na kutatuliwa, kamati hii katika mashirika mengi ya umma imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinahitaji kutatuliwa ikiwa ni pamoja na:-

### 9.2.1 Muongozo wa Uundwaji wa Kamati ya Ukaguzi

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa hakuna muongozo wowote hapa nchini kwa Mashirika ya Umma kuhusu namna ya muundo na majukumu ya kamati ya ukaguzi. Kwa sababu hii, mashirika mengi ya umma yamekuwa yakihangaika kila moja likitafuta namna ya kuanzisha kamati hii na majukumu ambayo kamati hii itayatekeleza. Baadhi ya Mashirika ya Umma yameanzisha kamati hii kwa mujibu wa maelekezo ya misingi ya utawala bora duniani kote wakati ambapo mashirika mengine yamefuata mfumo ulioelekezwa

katika kanuni ya 31 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 ambazo zilitungwa mahususi kwa ajili ya Serikali Kuu.

#### 9.2.2 Miongozo ya Utendaji wa Kamati ya Ukaguzi

Miongozo (charter) ya utendaji wa Kamati ya Ukaguzi ni miongozo katika utendaji wa kamati yenye tija. Tumebaini kuwa, mashirika mengi ya umma hayajaandaa miongozo (Charter) ya utendaji ili kutoa mwongozo katika utendaji na majukumu ya kamati za ukaguzi.

#### 9.2.3 Kutokuwepo kwa Mtaalamu wa Fedha katika Kamati ya Ukaguzi

Kamati ya ukaguzi ina jukumu la kuhakikisha kuwa Bodi ya Wakurugenzi inapata uhakika kuhusu mifumo ya kusimamia athari za kiutendaji katika mashirika wanayoyasimamia, utawala na mfumo wa udhibiti wa ndani. Kwa hiyo, inahitajika mchanganyiko wa taaluma muhimu na uzoefu katika masuala mbalimbali. Kwa sababu ya umuhimu wa usimamizi wa fedha na taratibu za uandaaji wa hesabu kwa kila shirika, ni vyema angalau mjumbe mmoja wa kamati hii kuwa na utaalamu na uzoefu wa kutosha wa fedha ili kutekeleza majukumu yake. Kamati inatakiwa kubaini na kukubaliana na bodi juu ya taaluma nyingine zinazohitajika katika kamati hii. Mfano wa taasisi zenye kasoro hizi ni Shirika la Utangazaji Tanzania.

Ingawa taratibu zinahitaji kuwepo kwa mtaalamu wa fedha kama ilivyo hapo juu, tumebaini kuwepo kwa kamati za ukaguzi katika baadhi ya Mashirika ya Umma bila kuwa na mtaalamu wa masuala ya fedha ambapo ni kinyume na utaratibu unavyotaka.

#### 9.3 Ukaguzi wa Ndani

Ukaguzi wa ndani kimsingi unakusudiwa kutathmini na kupendekeza maboresho katika mfumo wa udhibiti wa ndani wa shirika. Mfumo wa udhibiti wa ndani ni utaratibu unaowekwa na bodi ya wakurugenzi wa taasisi, menejimenti na watumishi wengine kwa ajili ya kuwezesha kutoa uhakika kuhusu namna ya kufikia malengo ya shirika

kwa tija na uhakika katika uendeshaji, usahihi katika taarifa za fedha na uzingatiaji wa sheria na kanuni mbalimbali. Ni jukumu la menejimenti kuhakikisha kuwa kunakuwepo mfumo madhubuti wa kulinda rasimali za taasisi na kuisaidia taasisi katika kufikia malengo yake. Ukaguzi wa ndani umebainika kuwa na mapungufu yafuatayo:-

### 9.3.1 Watumishi wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na Mfumo wa Kutoa Ripoti

Wakaguzi wa ndani wa nyakati hizi wanatakiwa kuipatia kamati ya ukaguzi uhakika kuhusu misingi na taratibu za utawala bora katika shirika ikiwa ni pamoja na kutekeleza mahitaji mbalimbali ya menejimenti na wadau wengine. Wakaguzi wa ndani wanatakiwa kuwa na uelewa wa juu katika masuala ya mfumo ya udhibiti katika shirika ili kuhakikisha kuwa mfumo na taratibu za kiutendaji ni madhubuti. Ili kufikia kiwango hiki kikubwa cha matarajio, vitengo vya ukaguzi wa ndani, havina budi kuwa na watumishi wa kutosha na wenye mchanganyiko wa taaluma.

Hata hivyo, tulibaini kuwa vitengo vya ukaguzi wa ndani katika baadhi ya mashirika ya umma vimeanzishwa bila kuwa na mkakati mahsusi wa watumishi ambao ungetokana na tathmini ya hatari zilizopo za kiutendaji. Kwa kiasi kikubwa, taasisi zimeanzisha vitengo hivi ikiwa ni hatua ya kutekeleza mapendekezo ya wakaguzi jambo ambalo linaondoa maana ya kuwa na vitengo hivi.

Kwa upande wa taratibu za utoaji ripoti za wakaguzi wa ndani, mwongozo unahitajika kutoa utaratibu wa namna vitengo hivi vinavyotakiwa kuripori matokeo ya kazi zao. Imebainika kuwa, katika baadhi ya mashirika vitengo hivi vinaripoti kiutawala na kimajukumu kwa mkuu wa shirika wakati katika mashirika mengine vitengo hivi vimebainika kuripoti kiutawala kwa mkuu wa shirika na kimajukumu kwenye kamati ya ukaguzi na zingine kwa bodi ya wakurugenzi. Mifano ya taasisi yenye mienendo hii isiyo na usawa ni pamoja na Bodi ya Korosho Tanzania, Mamlaka ya

Maji Musoma (MUWSA), Kampuni ya Ranchi ya Taifa (NARCO) na Shirika la Bima la Taifa (NIC).

### 9.3.2 Utayarishaji wa Miongozo ya Ukaguzi wa Ndani Pamoja na Mawanda Finyu ya Ukaguzi

Wakaguzi wa ndani wamebainika kushindwa kuandaa kitabu cha miongozo ya ukaguzi (internal audit manual) pamoja na mpango kazi wa kila mwaka miongozo ambayo ingeongoza shughuli zao za kila siku katika mashirika. Ni muhimu sana kwa vitengo hivi vya ukaguzi wa ndani vielekezwe na kamati husika za ukaguzi kuwa na miongozo husika na kuhakikisha kuwa kila mwaka vitengo vinaandaa mpango kazi wa mwaka na kuidhinishwa na kamati ya ukaguzi.

Tulibaini pia, kiwango cha kazi ya wakaguzi wa ndani kimekuwa na mawanda finyu na pia ripoti wanazotayarisha zimekuwa hazitoshelezi mahitaji ya kamati za ukaguzi. Katika baadhi ya Mashirika ya Umma, wakaguzi wa ndani hawakuweza kuandaa ripoti za kila robo mwaka kama inavyotakiwa na miongozo mbalimbali na pale ambapo ripoti ziliandaliwa katika baadhi ya mashirika, mawanda yake yalionekana kuwa finyu na kutozingatia hatari za kiutendaji zilizopo katika shirika husika kitu ambacho hakikuisaidia menejimenti na kamati ya ukaguzi katika kufanya maamuzi mbalimbali. Baadhi ya mashirika yaliyoonekana kuwa na udhaifu ni pamoja na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma (MUWSA).

### 9.3.3 Ushiriki wa Wakaguzi wa Ndani katika Kuhakiki Malipo (Examination)

Tumebaini kuwa vitengo vya ukaguzi wa ndani katika baadhi ya Mashirika ya Umma vinashiriki katika mchakato wa kuhakiki nyaraka za malipo kabla ya malipo kufanyika. Wakaguzi wa ndani pia wamekuwa wakihakiki mishahara kabla ya malipo kwenye baadhi ya mashirika.

Kanuni za utawala bora zinahitaji kuwa wakaguzi wa ndani wasihusike na uhakiki wa malipo na utekelezaji wa shughuli

zingine za kiutendaji isipokuwa katika kushauri ili baadaye wanapokuwa wakiutathmini mfumo unaotumika waweze kuwa na uhuru wa kutosha katika kuishauri menejimenti namna ya kuboresha mfumo wa ndani wa udhibiti. Mfano wa udhaifu huu umejitokeza katika Mfuko wa Bima ya Afya, na Chuo cha Ardhi (ARU).

#### 9.3.4 Bodi za Wakurugenzi Kuingilia Kazi za Menejimenti

Bodi za Wakurugenzi kuingilia kazi za menejimenti kunaathiri kazi zake za kiuangalizi katika kusimamia kazi za menejimenti. Miongoni mwa kazi za Bodi za Wakurugenzi ni kutunga sera kuhusu masuala yote yanayohusu shirika, kuandaa mipango, kutengeneza mifumo ya utumishi na kuhakikisha shirika linakuwa imara kifedha. Kuingilia shughuli za kiutendaji kwenye mashirika kunapunguza hamasa kwa menejimenti katika utendaji wa kazi na wajibu kulingana na malengo yaliyowekwa. Mgongano huo unaweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya shirika. Hii imeonekana kwenye shirika moja la umma wakati wa ukaguzi uliofanyika kwa mwaka huu ambapo maonyesho 19 ya utalii ya kimataifa yalifanyika na kuhudhuriwa na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi badala ya menejimenti ya shirika. Pia ilibainika kuwa kamati ya Bodi ya Utendaji ilipendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi wanatakiwa kuhudhuria maonyesho ya utalii kwa niaba ya Mamlaka kinyume na vifungu Na. 3 na 5 vya Waraka wa Ikulu Na.SHC/B.40/6/21 wa tarehe 28/03/1994, unaofafanua kwa undani jukumu la Bodi ya Wakurugenzi na mamlaka waliyopewa ya kuhakikisha kuwa Mashirika ya Umma yanafikia malengo yaliyokusudiwa. Hili linaonekana kama kukiuka waraka uliotolewa na uhuru wa menejimenti na Bodi na kuleta mwingiliano wa kimaslahi kwa pande zote.

Maonyesho yaliyohudhuriwa na Bodi yanajuimuisha ya Vakantieburst-Uholanzi, BFT Brussels, Tel Aviv - Israel, ATM - Dubai, Chicago, ITB Ujerumani n.k. Sababu zilizotolewa na Mamlaka kwa Bodi kuhusishwa kwenye maonyesho hayo ya utalii zilikuwa haziridhishi na kukubalika.

Kwa kufuata misingi ya Utawala Bora, masuala ya kiutendaji ya Shirika yapo chini ya menejimenti na sio Bodi. Kwa maoni yetu jukumu la bodi la kuwa mwangalizi wa mwenendo wa Shirika utakuwa umeathiriwa kwa kujiingiza kwenye shughuli za kiutendaji za Shirika. Bodi ikijiingiza kwenye shughuli za kiutendaji za Shirika, jukumu lake la kuwa mwangalizi na kutoa mapendekezo pale ambapo menejimenti imeshindwa kufikia malengo yake linakuwa limeathiriwa.

#### 9.3.5. Kutokufuata Sheria ya Serikali ya kulipa Ada za Wakurugenzi wa Bodi

Ada za wakurugenzi na gharama za bodi za wakurugenzi zimekuwa zikiongezeka kila mwaka katika mashirika mengi ya umma. Hali hii inaonyesha kutofuatwa kwa kanuni za utawala bora. Kazi mojawapo ya Bodi za Wakurugenzi katika taasisi ni kusimamia majukumu ya menejimenti ya kuongeza mapato na kupunguza matumizi. Kwa upande mwingine matumizi yamepanda kwenye baadhi ya mashirika kwa sababu ya ongezeko la gharama za bodi na ada za wakurugenzi ambazo hupangwa na wakurugenzi wenyewe. Hii imedhihirika katika ukaguzi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA). Katika mkutano wake wa bodi uliofanyika mwaka 2006, Bodi ya Wakurugenzi wa mamlaka iliamua kwamba ada za wakurugenzi zipangwe kwa njia mbili; njia ya kwanza - Wakurugenzi walipwe ada kwa kupungua (on a reducing basis) : Mwenyekiti na Makamu mwenyekiti walipwe shilingi milioni 1.75 kwa mwaka, wakati wakurugenzi wengine walipwe shilingi milioni 1.5 kwa mwaka; njia ya pili - Iwapo faida ya mamlaka kabla ya kodi ni sawa au zaidi ya bilioni moja, ada za wakurugenzi zitakuwa asilimia 4 ya hiyo bilioni moja au zaidi na itagawanywa kama ifuatavyo, asilimia kumi (10%) ya asilimia nne (4%) ya faida kwa mwenyekiti na wakurugenzi wengine watagawana asilimia tisini (90%) ya asilimia nne (4%). Baada ya majadiliano na menejimenti na bodi ya NCAA, hatukupatiwa idhini ya njia ya pili kutoka kwa Waziri mwenye dhamana wala maelekezo ya Serikali au Waraka wa Hazina wa kuridhia malipo hayo.

#### 9.3.6. Kutokufuata Waraka wa Msajili wa Hazina

Wizara ya Fedha ilitoa waraka wa Hazina Na.8 tarehe 29 Juni 2009 unao yataka Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kuchangia asilimia 10 ya mapato yote kabla ya matumizi yatokanayo na shughuli za uzalishaji kwenda Hazina. Baadhi ya Mashirika hayakufuata waraka huu kwa mfano Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro (NCCA) ambayo haikutoa mchango wake kwa Hazina wa kiasi cha shilingi bilioni 3.721. Pia, kutofuata matakwa ya waraka ilionekana katika Mamlaka ya Udhambi wa Mawasiliano (TCRA) ijapokuwa imeanishwa pia kwenye Kifungu Na.54 cha Sheria ya TCRA na Sura ya 172 R.E 2007 inayoainisha kutoa mchango wa asilimia 10 ya mapato kabla ya matumizi kwa Hazina. Hata hivyo, ilibainika kwenye Muhtasari wa kikao cha dharura cha Bodi kilichofanyika tarehe 8 Septemba 2009 kuwa Bodi iliamua kuwa michango kwa Hazina iwe ni asilimia 10 ya mapato baada ya matumizi badala ya mapato kabla ya matumizi, hii ni kinyume na mwongozo uliotolewa na serikali, na hakuna waraka wa kubadilisha maamuzi ya awali ya Hazina. Kitendo hiki cha bodi ni kudharau maagizo ya Serikali.

#### 9.4 Hitimisho

Kwa ujumla, licha ya matukio mbalimbali yaliyojitokeza katika Mashirika ya Umma yanayohusiana na kushindwa kwa mifumo ya utawala bora na kutotekeleza mapendekezo ya kitaalamu yanayotolewa na Ofisi yangu, sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kutekeleza mapendekezo yetu ili kuleta ufanisi katika utendaji wa Mashirika ya Umma. Kwa hali hii tunaishauri Serikali kutunga Sheria na Kanuni za Utawala Bora katika Mashirika ya Umma ambayo itachochea uzingativu wa kanuni hizo na hivyo kuweza kuboresha utawala bora katika Mashirika na Taasisi za Umma.



## SURA YA KUMI

### UTENDAJI WA MASHIRIKA YALIYOPO NA YALIYOBINAFSISHWA

#### 10.0 Utangulizi

Sura hii inatoa taarifa ya utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyopo na yale yaliyobinafsishwa. Mashirika yaliyopo ni yale ambayo Serikali inahusika moja kwa moja na utendaji wake wa kazi na yale ambayo haina mamlaka ya moja kwa moja na utendaji wake wa kazi. Kama inavyokumbukwa, mwanzoni mwa miaka ya tisini (1990s) Serikali iliamua kutojikusha na uendeshaji wa Mashirika ya Umma na kubinafsisha idadi kubwa ya mashirika hayo. Serikali iliamua kujikusha zaidi na jukumu la udhibiti, na kuacha shughuli za kibiashara mikononi mwa sekta binafsi. Uamuzi huu ulitokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na utendaji mbovu wa Mashirika ya Umma yaliyokuwa yanamilikiwa na Serikali. Hata hivyo, siyo Mashirika yote yalibinafsishwa, kwani baadhi yalitengwa kwa ajili ya kubinafsishwa lakini baadaye yakarejeshwa na kuruhusiwa kuendelea na biashara. Mashirika ya Umma yaliyobinafsishwa yanasimamiwa na Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC) na mengine yapo chini ya Msajili wa Hazina.

Hivyo, sura hii inaeleza mambo muhimu ambayo yameandikwa katika taarifa ya mwaka ya Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma na Msajili wa Hazina kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010.

Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambapo sehemu ya kwanza inazungumzia utendaji wa Mashirika ya Umma yaliyopo na sehemu ya pili inazungumzia utendaji wa Mashirika yaliyobinafsishwa.

#### 10.1 Utendaji Kazi wa Mashirika ya Umma

Uchambuzi uliofanyika katika kipindi cha mwaka huu ulibaini kuwa, baadhi ya Mashirika ya Umma hayajiendesha

kama inavyotarajiwa. Mambo yanayosababisha Mashirika ya Umma kutofanya vizuri katika nchi yetu ni pamoja na urasimu katika kutoa maelekezo ya kisera pamoja na kutopata ushauri wa kisheria kutoka Wizara husika, udhaifu katika sheria na mipaka ya udhibiti inayosimamia utendaji wa Mashirika ya Umma, uwezo wa usimamizi hafifu wa Ofisi ya Msajili wa Hazina, Wizara na Bodi za Wakurugenzi kushindwa kutimiza wajibu wao kama vyombo vya usimamizi, ukosefu wa tabia ya kijasiriamali, menejimenti zisizo na uwezo, kutokuwa na wataalum, kutojipanga vizuri, kutokuwa na miundo ya uongozi inayofaa, kuanzisha mifumo bila ya kuwa na malengo, mipango, bajeti pamoja na usimamizi wa fedha hafifu unaotokana na ukosefu wa wafanyakazi bora, kutokuwepo kwa uwazi na uwajibikaji, michakato na taratibu duni za manunuzi, usimamizi hafifu wa mali na mitaji midogo kwa baadhi ya Mashirika ya Umma.

Uendeshaji wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo katika kipindi cha mwaka 2010 ulipimwa kwa kuangalia utendaji wa kifedha, kwa kuzingatia madeni yaliyodhaminiwa na Serikali, mapato kwa Serikali yatokanayo na gawio, marejesho ya mikopo na mapato mengineyo. Bakaa ya mapato na pia uwezo wa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo kujiendesha zenyewe.

## 10.2 Uwekezaji wa Serikali

### 10.2.1 Uwekezaji Katika Kampuni za Ndani ya Nchi

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2010, Serikali ilikuwa inamiliki hisa na mitaji ya kiasi cha shilingi trilioni 7.7 katika mashirika na Taasisi nyinginezo za Serikali 196 ambazo hesabu zao zilikaguliwa na kuwakilishwa kwa Msajili wa Hazina. Kwa hiyo, jumla ya uwezaji ni trilioni 7.7 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010 ikiwa ni ongezeko la shilingi trilioni 1.6 ikilinganishwa na jumla ya uwekezaji wa shilingi trilioni 6.1 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2009. Ongezeko hili linatokana na Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kuwasilisha hesabu

zilizokaguliwa ambazo zinaonyesha thamani halisi ya umiliki, mtaji wa Serikali na mapato mengine.

#### 10.2.2 Uwekezaji Katika Kampuni za Nje ya Nchi

Kutokana na taarifa ya Msajili wa Hazina ya uwekezaji nje ya nchi, Serikali inamiliki mali ya thamani ya shilingi bilioni 113.6 katika taasisi za kigeni tisa (9) kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ukilinganisha na shilingi bilioni 140.5 za mwaka uliopita 2008/2009. Kiwango hiki kimepungua kutokana na kupungua kwa mauzo ya hisa katika baadhi ya Kampuni, vile vile kutokana na ongezeko la limbikizo la hasara katika Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA).

#### 10.3 Mapato ya Serikali

Mapato ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 yanayotokana na gawio, marejesho ya mikopo na vyanzo vinginevyo yalifikia shilingi bilioni 40.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 84.1 kwa mwaka 2008/2009. Mapato ya Serikali yamepungua kwa shilingi bilioni 43.5 ambayo ni sawa na asilimia 51.68. Upungufu wa mapato ya Serikali yanatokana na kupungua kwa vyanzo vinginevyo vya mapato na marejesho kutoka shilingi bilioni 46.0 kwa mwaka 2008/2009 mpaka shilingi bilioni 14.1 kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mapato yaliyopokelewa kwa mwaka 2009/2010 ni kutoka Kampuni ya Sigara Tanzania, Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma (CHC), Mamlaka ya Udhubiti wa Mawasiliano Tanzania, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania. Kwa mwaka huu, taasisi ambazo hazikuchangia mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali kutokana na athari za mtikisiko wa uchumi Duniani ni pamoja na Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Mamlaka ya Eneo la Hifadhi Ngorongoro (NCAA).

Kwa upande mwingine, gawio limepungua kutoka shilingi bilioni 31.3 kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009 mpaka kufikia shilingi bilioni 15.1 kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Upungufu huu umetokana na baadhi ya taasisi


ambazo hazikutoa gawio kwa Serikali kwa sababu ya kuwa na mipango ya miradi mikubwa ya uwekezaji na kukosekana kwa faida.

Kwa ujumla, mapato yaliyokusanywa kutokana na gawio, malipo ya mkopo, marejesho na mapato mengineyo ya mauzo ya hisa yalikuwa kama ifuatavyo:

### Jedwali 13: Mapato ya Serikali

Aina ya Mapato	2006/07 Kiasi Sh. "000,000"	2007/08 Kiasi Sh. "000,000"	2008/09 Kiasi Sh. "000,000"	2009/2010 Kiasi Sh. "000,000"
Gawio	13,389.8	57,147.6	31,323.3	15,127.5
Mtaji & Riba	12,664.7	11,503.6	6,795.1	11,465.6
Mapato mengineyo & Fedha zilizowasilihwa	0.33	8,300.0	46,001.9	14,056.6
Jumla	26,054.8	76,951.1	84,120.1	40,649.7

#### Kielelezo 4: Mapato ya Serikali



Kulikuwa na bakaa ya mapato ya shilingi bilioni 105.8 ambapo shilingi bilioni 9.56 ni bakaa ya mikopo ambazo zilipaswa kukusanywa. Sababu ya kuwapo kwa bakaa ni:-

- (i) Kuwepo kwa Mashirika ya Umma yaliyofilisika chini ya Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma. Mapato yanayotegemewa kukusanywa kutokana na malipo ya mikopo ya Mashirika haya huenda yakapatikana katika mchakato mzima wa ubinafsishaji.
- (ii) Mashirika ya Umma kama TANESCO na TRC kuwa na hali ngumu kifedha kiasi cha kushindwa kulipa madeni. Mashirika haya yapo katika mkakati/mpango wa maboresho.
- (iii) Bakaa ya mkopo wa Zanzibar katika fedha za kigeni zilizotolewa kama mkopo na bado mpaka sasa mkopo unadhaminiwa na Serikali zote mbili chini ya mpango wa Tume ya Mfuko wa Pamoja wa Fedha.

- (iv) Mgawo na mapato mengineyo ambayo yalipaswa kulipwa mwaka 2009/2010, mfano mauzo ya asilimia 1.8 ya hisa za Serikali kwa NMB ambayo yaligawiwa kwa wafanyakazi wa NMB, yatalipwa katika mwaka wa fedha 2010/11.

#### 10.4 Bakaa ya Deni la Serikali kwa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo

Deni ambalo Serikali inadai mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2010 limepungua na kufikia shilingi bilioni 456.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 478.0 za mwaka 2008/2009. Kupungua huku kwa kiasi kikubwa kunatokana na malipo yaliyofanywa na Mamlaka ya Bandari Tanzania, Kiwanda cha Saruji Tanzania na Mamlaka ya Udhhibiti wa Anga Tanzania kwa kuzingatia makubaliano ya jedwali la marejesho ya mikopo.

Jumla ya bakaa imeongezeka kutoka shilingi bilioni 93.5 kwa mwaka 2008/2009 mpaka shilingi bilioni 95.5 kwa mwaka 2009/2010 ambayo ni sawa na asilimia 2.23. Ongezeko linatokana na kubadilika kwa viwango vya ubadilishaji fedha mara kwa mara pamoja na madeni yasiyolipika.

Kiwango cha mkopo kilichokusanywa, mtaji na riba kimeongezeka kwa asilimia 68.74 kutoka shilingi bilioni 6.8 mwaka 2008/2009 mpaka shilingi bilioni 11.5 mwaka 2009/2010.

Katika kiasi cha deni cha shilingi bilioni 95.5 mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2010; shilingi bilioni 20.2 ni deni la Zanzibar. Shilingi bilioni 4.5 ni deni la TTCL baada ya kukamilika kwa mpango wa kubadilishana madeni ambao ulirekebishwa na kufikia shilingi bilioni 15.60. Shilingi bilioni 30.5 ni deni la TRC na deni la TANESCO ni shilingi bilioni 21. Taasisi hizi nne zinatoa jumla ya asilimia 66.4 ya bakaa yote iliyopaswa kulipwa kulingana na vipengele vya mkataba.

## 10.5 Dhamana za Serikali

Kwa mujibu wa Sheria ya mwaka 1974 (iliyorekebisha 2004) inayohusu mikopo, dhamana na ruzuku zilizotolewa na Serikali katika taarifa iliyotolewa na Msajili wa Hazina kwa Mashirika ya Umma na Taasisi nyinginezo ya tarehe 30 Juni, 2010 ilionyesha kuwa:

Jumla ya deni lililodhaminiwa na Serikali ni shilingi bilioni 451.927. Deni hili limegawanywa kwenye makundi yafuatayo:

- (a) Mashirika ambayo hayaendelei na uzalishaji na yapo chini ya mpango wa mufilisi ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Mkongwe Tanzania, State Motor Cooperation, SUKITA and General Tyre East Africa. Haya yote yana jumla ya shilingi bilioni 30.819 ambayo ni asilimia 6.82 ya dhamana yote.
- (b) Mashirika ambayo utaratibu wa malipo yake ulibadilishwa ni pamoja na Friendship Textile Mills ambalo lilikuwa na deni la shilingi bilioni 25.781 ambayo ni asilimia 5.7 ya dhamana zote.
- (c) Mashirika yenye uhaba wa fedha ikiwa ni pamoja na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ina dhamana za jumla ya shilingi bilioni 68.131, Shirika la Ndege Tanzania shilingi bilioni 29.522, Kampuni ya Mbolea Tanzania shilingi bilioni 31.9 na Chama Kikuu cha Ushirika Mara shilingi bilioni 8.5. Zote zina jumla ya shilingi bilioni 138.057 ambazo ni sawa na asilimia 30.55 ya dhamana zote.
- (d) Mashirika ambayo malipo yake yanafuata taratibu za malipo zilizowekwa ikiwa ni pamoja na mkopo wa pamoja kwa TANESCO shilingi bilioni 256.5, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam- Kitivo cha Biashara shilingi milioni 770 ambazo ni sawa na asilimia 56.93 ya dhamana zote.

10.6 Uamuzi wa Kutotoza Ada ya Maridhiano (Concesión fee)  
Menejimenti ya TANAPA iliamua kutoza ada ya maridhiano kwa kutumia kiwango maalum (Fixed rate). Hata hivyo, manejimenti ilimteua mtaalam Kampuni ya Ushauri ya PricewaterhouseCoopers (PWC) kufanya tathmini ya namna ya kuongeza kiwango cha juu cha ukusanyaji wa ada za maridhiano. Mshauri alikubaliana na pendekezo la TANAPA la kutoza kiwango maalum (fixed rate). Wizara ya Maliasili na Utalii ilipewa pendekezo la kutoza kiwango maalum kwa barua Na. HD.176/484/01 ya tarehe 20 Julai, 2007. Ndipo Wizara tarehe 15 Octoba, 2007 ilibadili maamuzi ya TANAPA na kuanzisha tozo la asilimia badala ya kiwango maalum kuanzia tarehe 1 Julai, 2008. Uamuzi huu umeathiri kwa kiasi kikubwa bajeti ya makusanyo ya TANAPA kwa kiasi cha shilingi bilioni 16.9 kwa mwaka wa fedha 2008/2009. Kama tozo la kiwango maalum lingetumika, TANAPA ingekusanya jumla ya shilingi bilioni 21.28 wakati tozo la asilimia limevuna shilingi bilioni 4.59 tu, hivyo kusababisha upungufu wa makusanyo ya shilingi bilioni 16.69. Tunashauri Wizara ibadili uamuzi wake wa kuiruhusu TANAPA kutoza ada ya maridhiano kwa kutumia kiwango maalum (fixed rate). Kama ilivyokuwa imependekezwa na wataalamu na kama menejimenti ya TANAPA ilivyokuwa imeamua na kuanza kutekeleza.

10.7 Sababu Zinazokwamisha Utendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imetimiza miaka 5 sasa tangu ilipoanza kazi mwaka 2005/2006. Bodi imekumbana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na changamoto za mambo ya sera na utendaji, kama ifuatavyo:

Changamoto za Sera;

Wanafunzi kutochangia gharama za elimu kwa sababu wanafunzi wa vyuo bado wanaishinikiza serikali yao igharamie asilimia mia moja ya gharama ya elimu yao.

Wadau wanadhani mkopo wa wanafunzi ni zawadi na wala si mkopo, Shilingi ya Tanzania imeendelea kushuka thamani



na kiwango kikubwa cha maombi ya mkopo zaidi ya bajeti halisi. Wanafunzi wasio na sifa nao wanahitaji mikopo, vyo vikiu vinapandisha ada, ugumu katika kutambua maelezo ya muombaji. Baadhi ya vyo vinasajili wanafunzi nje ya Mfumo wa pamoja wa usajili.

**Changamoto za Utendaji;** Kuchelewa kuwasilishwa kwa majina kutoka NACTE na TCU kwa ajili ya usajili, waombaji wa mkopo kusajiliwa katika vyo viwili tofauti, kutokuwa makini katika kujaza fomu za maombi ya mkopo, muombaji wa mkopo kuhama kutoka Chuo kimojawapo alichopangiwa na TCU, vyo kuchelewa kutoa taarifa za maendeleo ya wanafunzi, wakopeshwaji huchelewa kukiri kupokea mkopo hivyo, mabaki ya mikopo kuchelewa kurejeshwa Bodi ya Mikopo. Kuendelea kuchelewa kutanzua changamoto hizi, kunadhoofisha utendaji wa Bodi. Matokeo yake yanaweza kasababisha malalamiko dhidi ya Bodi, vurugu na maandamano ya wanafunzi yasiyo ya lazima.

#### **10.8 Utendaji Kazi wa Mashirika Baada ya Ubinafsishwaji**

Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma lilikabidhiwa na Serikali jukumu la kusimamia na kutathimini kazi za mashirika yote ya umma yaliyobinafsishwa; kwa mujibu wa Sheria Na. 16 ya mwaka 2007 ya Benki ya Taifa ya Biashara.

Mnamo mwaka 2010, Shirika lilipanga kufanya tathmini kwa Mashirika 80 yaliyobinafsishwa. Hata hivyo, mpaka kufikia tarehe 31 Disemba 2010, Shirika lilifanikiwa kutathmini mashirika 53. Mashirika 44 kati ya 53 yalikuwa yakifanya kazi. Lakini baadhi yao yalikuwa yakifanya kazi kwa hasara kutokana na mtaji mdogo wa wawekezaji hivyo hayachangii kwa kiwango cha kutosha katika pato la Taifa. Kwa upande mwingine, Mashirika tisa (9) yalikuwa bado yamefungwa kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji chini ya kiwango, uongozi dhaifu, mtaji mdogo, baadhi ya mitambo na mashine ya viwanda kuchakaa, mipango hafifu na ukosefu wa taarifa sahihi za uwekezaji hivyo kusababisha kuendelea kupata hasara mwaka hadi mwaka

na hatimaye kufungwa. Sababu nyingine ni kuwa na madeni makubwa, kushindwa kupata masoko, ukosefu wa umeme thabiti, kuchelewa kutimiza vipengele vya awali vya makubaliano ya manunuzi kama vile kukabidhiana hati za umiliki, gharama kubwa za uendeshaji kama vile umeme na mali ghafi. Gharama hizi zimesababisha bidhaa zinazozalishwa kuwa si za ushindani. Pia, kumekuwepo na migogoro ya wadau na mashitaka yasiyokwisha mahakamani.

#### 10.9. Mashirika yaliyotengwa kwa ajili ya Kubinafsishwa.

Ubinafsishaji wa Mashirika ya umma hapa nchini ulianza tangu mwaka 1993. Tume ya Rais ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma (PSRC) ilipewa mamlaka ya kusimamia na kuongoza shughuli zote za ubinafsishaji. Hata hivyo shughuli za tume zilisimama tarehe 31 Disemba 2007 baada ya kumaliza ubinafsishaji wa mashirika mengi ambayo yalikuwa yametengwa. Mashirika ya Umma 34 ambayo yalikuwa kwenye hatua za ubinafsishwaji yaliamishwa katika Shirika Hodhi la Mali za Makampuni Yaliyobinafsishwa kutoka Tume ya Rais ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma (PSRC) kuanzia tarehe 1 Januari 2008.

Katika tarehe hiyo 1 Januari 2008, Shirika Hodhi la Mali za Makampuni Yaliyobinafsishwa lilipewa majukumu ya kuendesha shughuli za kampuni ya SIMU 2000 (SIMU 2000 Ltd). Kazi ambazo zilikuwa hazijakamilishwa na Kampuni ya SIMU 2000 ilikuwa ni pamoja na kusimamia na kuuza rastimali ambazo hazikuwa muhimu za kampuni ya Mawasiliano ya Simu (TTCL), kuchukuwa madeni ya mafao ya wafanyakazi ambayo hayakulipwa na lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki na kusimamia maswala yote ya mashtaka ya kimahakama dhidi ya TTCL. Kabla ya hapo Shirika Hodhi la Mali Zilizobinafsishwa lilirithi shughuli zote za uliokuwa Mfuko wa Mikopo (LART) na Shirika la Ndege la Tanzania (ATHCO)

Hata hivyo hadi kufikia tarehe ya kuandika ripoti hii (25 Februari, 2010), mashirika 34 bado yalikuwa yametengwa

kwa ajili ya ubinafsishwaji. Ieleweke kwamba Mashirika yanayotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa, yanakuwa yamezuiwa kupanuka zaidi kwa sababu hayawezi kuandaa na kutekeleza mipango mikakati au kuwekeza. Pia wafanyakazi wa mashirika hayo wanakuwa hawana morali wa kufanya kazi au kutimiza wajibu wao kwa sababu ya kutokujua hatima ya ajira yao na ya mwajiri wao. Uchakavu wa mali na raslimali za mashirika yaliyotengwa unakuwa ni wa kiasi cha juu kutokana na kukosa fedha kwa ajili ya ukarabati au urudishwaji wa mali zilizoharibika unakuwa mgumu. Serikali inapaswa kuharakisha taratibu za ubinafsishwaji wa mashirika 34 yaliyotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa ili kuepuka uharibifu na uchakavu wa raslimali zinazomilikiwa na mashirika hayo au kutoyatenga na kuyaongezea mitaji ili yaanze kufanya kazi upya. Maelezo ya mashirika yaliyotengwa kwa kubinafsishwa yapo kwenye Kiambatishi Na.IV cha hii ripoti.

#### 10.10. Mitaji Midogo ya Mashirika na Taasisi za Umma

Mitaji midogo ni hali ambayo kampuni inakuwa haina fedha za kutosha kujiendesha kibiashara na kulipa madeni inayodaiwa. Tunaweza pia kusema ni pale ambapo kampuni inakuwa na mtaji hafifu wa kuendesha shuguli zake bila ya kupata msaada kutoka nje. Mashirika yenye mitaji midogo mara nyingi yanategemea mikopo ya muda mfupi kwa ajili ya kupata fedha ya kuendesha biashara. Mitaji midogo inaweza ikawa ni tatizo kubwa ambalo litapelekea biashara nyingi kushidwa kufanyika. Kuna Mashirika ya Umma ambayo huduma zake kwa jamii ni za muhimu sana lakini yanashindwa kutoa huduma kama yanavyotegemewa kutokana na kukosa mtaji wa kutosha. Tatizo hili limepelekea utendaji wa mashirika mengi kuwa chini ya kiwango.

Baadhi ya Mashirika yenye utendaji duni ambayo yanahitaji Serikali kuyanusuru kwa kuyaongezea mitaji ni kama yafuatayo: Shirika la Ugavi na Umeme Tanzania (TANESCO) ambalo halifanyi vizuri kwa sababu ya kukosa mtaji wa kutosha. Shirika hili halina vifaa vya kisasa vya kurahisisha usambazaji wa umeme. Pia shirika limeshindwa kuongeza

vyanzo vingine vya umeme hasa kipindi cha ukame hivyo kupelekea kuwepo kwa umeme wa mgawo nchini kwa kipindi kirefu. Mashirika mengine ni Shirika la Ndege Tanzania, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Shirika la Reli Tanzania, Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania.

Kuna haja kwa Serikali kuingilia kati na kutafuta suluhisho la kudumu kwa tatizo hili kwa kuongeza mitaji kwa mashirika ya umma ambayo hayafanyi vizuri kabisa.

#### 10.11. Mashirika Ambayo Umiliki na Usimamizi wake Unapaswa kuwa Chini ya Serikali

Hatua kubwa zimechukuliwa na Serikali kuweka huria uchumi wa Tanzania kwa kuvutia uwekezaji wa nje na wa ndani. Katika hatua hii, Tanzania ilifanya mageuzi makubwa katika mashirika yanayomilikiwa na Taifa mwanzoni mwa miaka ya 1990, hatua ambayo bado inaendelea.

Mpango huu mpaka sasa umeondoa umiliki wa mashirika ya umma 336 kutoka Serikalini. Kwa ujumla, ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 4 kwa mwaka. Ongezeko hili ni zuri zaidi ya ilivyokuwa miaka ishirini (20) iliyopita hata hivyo haitoshi kuboresha maisha ya watanzania wa kawaida. Imebainika kuwa, baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa yanafanya vizuri wakati mengine hayafanyi vizuri kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo, uongozi dhaifu, ukosefu wa mitaji na nyingine ni kutofuatwa makubaliano ya uuzaji wa mashirika hayo.

Hata hivyo, ubinafsishaji haukuzingatia mashirika nyeti ambayo yalitakiwa kuachwa chini ya usimamizi na umiliki wa Serikali kwa kuzingatia umuhimu na mchango wa mashirika hayo katika uchumi hali ambayo ilisababisha Serikali kurudisha umiliki wa baadhi ya mashirika. Mifano yake ikiwa ni Shirika la Ugavi na Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Shirika la Reli Tanzania (TRC), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA),

Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Kampuni ya Usambazaji Maji Safi Dar es salaam (DAWASCO) na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es salaam (DAWASA), Shirika la Madini Tanzania (STAMICO). Mashirika haya hayategemewi kuzalisha faida bali umuhimu wake unaitaka Serikali kuyapa ruzuku pale mahitaji yanapojitokeza.

Baadhi ya mashirika ya umma yanatakiwa kumilikiwa na Serikali kutokana na aina ya huduma inayotoa katika nchi. Kwa mfano, Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ni alama ya utambulisho wa Taifa nje ya nchi ambayo yaweza kuitangaza Tanzania na kukuza utalii. Vivyo hivyo, kikwazo chochote katika utendaji wa TANESCO kitasababisha: uzalishaji mdogo, mapato madogo ya kodi, kupotea kwa ajira, mfumuko wa bei na mengineyo. Kwa upande mwingine, usafiri ni tatizo lingine, hasa kwa wanafunzi. Kama Serikali, ingelipa uwezo Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) angalau kuweza kujiendesha kwa nusu ya kiwango cha waendesha mabasi binafsi, tatizo hili kwa wananchi wa kawaida lingeweza kupungua. Kuyaacha mashirika haya katika mikono ya wamiliki binafsi ni hatari kwa uhuru wetu na mchango katika uchumi wa nchi. Makampuni yanayomilikiwa na watu binafsi mara nyingi hulenga kupata faida na si kutoa huduma.

#### 10.12. Changamoto za Wakati wa Zoezi la Usimamizi na Tathmini

Shirika Hodhi la Raslimali za Serikali limekumbana na changamoto mbalimbali wakati wa zoezi la tathmini kama inavyobainishwa hapa chini:

- Baadhi ya wawekezaji hawakuwa tayari kutoa maelezo na taarifa sahihi kuwezesha zoezi la tathmini.
- Baadhi ya mikataba ya manunuzi haikuambatanishwa na mpango wa uwekezaji hivyo kusababisha ugumu katika kuweka vigezo vya kutathmini utendaji wa mwekezaji.
- Baadhi ya mipango ya uwekezaji haiko wazi hivyo kukosa vigezo vya utendaji vilivyokubaliwa awali ili kurahisisha upimaji wa utendaji.

- Kutokuwepo kwa mkataba wa mauzo wakati wa ubinafsishwaji kabla ya kuanzishwa kwa PSRC.
- Matatizo ya mawasiliano baina ya wawekezaji na mashirika kutokana na ukweli kwamba baadhi ya mashirika yalibadili biashara, majina, mahali pamoja na anuani za mawasiliano.

## SURA YA KUMI NA MOJA

### TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

#### 11.0 Utangulizi

Sera ya teknolojia ya habari ilianzishwa mwezi Machi mwaka 2003, ili kuchochea ukuaji wa teknolojia ya habari hapa nchini. Maamuzi haya yalifanyika kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknolojia ya habari duniani kote tangu mwisho wa karne ya ishirini ambapo maendeleo hayo yamepelekea kupata mabadiliko makubwa kwenye maeneo ya kompyuta, mawasiliano ya simu na utangazaji. Pia teknolojia hii imesababisha mabadiliko kwenye maeneo mengine kama vile kukua kwa uelewa na maendeleo katika rasimali watu. Kuongezeka kwa uwezo wa teknolojia kumwezesha na ukuaji wa utandawazi hasa kwenye eneo la kompyuta na matumizi ya intaneti.

Ukuaji huo, umeleta mabadiliko kwenye uendeshaji wa biashara, umwezesha kujifunza na kubadilishana mawazo, umwezesha kubadilishana taarifa ulimwenguni, umwezesha wananchi na jamii kiasi cha kuleta mabadiliko katika uongozi kwa ujumla, hivyo kusababisha kukua kwa uchumi uliotokana na urahisi wa kupeana taarifa. Maendeleo katika sekta ya habari na mawasiliano yamechangia kufikia malengo katika uwekezaji, ufundishaji wa teknolojia na ukuaji wa mauzo.

Jitihada hizi zimwezesha Serikali na Mashirika ya Umma kutatua matatizo yake kwa ufasaha zaidi. Hivyo, sura hii inatoa taarifa ya mapungufu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi ambayo yakirekebishwa yataongeza ufanisi katika utendaji wa Mashirika ya Umma kama ilivyoonekana katika ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2010.

**11.1 Kutokuwepo kwa Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu za Taratibu zote za Teknolojia ya Habari**

Kwa kawaida taratibu rasmi za utunzaji kumbukumbu ni muhimu kuwepo kwa kila mfumo mpya unaonunuliwa ili kuwa na maelezo na kubainisha aina ya mfumo, kuujaribu mfumo huo kabla ya kuutumia, kufundisha watumiaji na pia kuwa na maelezo ya mabadiliko na maboresho yaliyofanywa katika mfumo huo.

Ukaguzi ulibaini baadhi ya mashirika ya umma yamenunua mifumo ya teknolojia ya habari na kuingiza mabadiliko mapya bila ya kuwa na taratibu rasmi za utunzaji kumbukumbu. Hali hii, inaweza kusababisha matumizi hafifu na yasiyokidhi mfumo mpya ulionunuliwa na ingeweza kusababisha kupotea kwa miongozo ya kuzuia mabadiliko. Hali hii inaweza kutokea kutokana na sababu kwamba mifumo mipya inatumika bila ya kuwa na taratibu rasmi za utunzaji wa kumbukumbu. Upembuzi uliofanywa katika miongozo ya kuzuia mabadiliko ya uongozi ambayo hutumika kuhakikisha mabadiliko yote ya teknolojia ya habari yanaruhusiwa ipasavyo na kutekelezwa kwa usahihi ulibaini kwamba ruhusa hazikutolewa kwa baadhi ya mabadiliko. Hivyo kuna athari kubwa inayoweza kutokea itakayo athiri ubora, ruhusa, usahihi wa maingizo ya data, na kukamilika kwa data zinazotoka na athari ya matumizi ya teknolojia mpya katika shirika husika. Mfano wa mashirika yaliyokuwa na kasoro hiyo ni Kampuni ya simu Tanzania na Hifadhi za Taifa Tanzania.

**11.2 Kutokuwepo kwa Kamati za Utendaji na Mpango Mkakati wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

Mpango mkakati wa teknolojia ya habari ni nyaraka inayoandaliwa na shirika ili kuhakikisha kuwa malengo ya teknolojia ya habari yanawiana na mpango mkuu wa shirika. Ni vizuri kila shirika kuwa na kamati ya utendaji ya teknolojia ya habari itakayohakikisha kuwa, matumizi ya teknolojia yanakidhi malengo ya Shirika. Kamati hii inatakiwa kuwa na wawakilishi kutoka idara mbalimbali



ndani ya Shirika. Pia tumebaini kuwa, mashirika mengine hayana mpango mkakati wa teknolojia ya habari wala kamati ya utendaji. Katika upembuzi mwingine, tulibaini kuwepo kwa kitengo cha teknolojia ya habari kinachoshughulika na baadhi ya mambo kama matumizi ya mtandao, lakini usimamizi wa utunzaji wa kumbukumbu katika kompyuta haukupewa kipaumbele. Kutokuwa makini katika usimamizi wa kutunza kumbukumbu kunaweza kusababisha kutokea kwa mapungufu mbalimbali ambayo yanaweza yasigundulike kwa mfano kubadilishwa, kufutwa au kuongeza taarifa yeyote isivyotakiwa na matokeo yake inaweza ikawa ni kuharibu taarifa zilizohifadhiwa kwenye mfumo wa utunzaji kumbukumbu na mifumo mingine itakayotumika hapo baadaye. Mashirika yaliyokuwa na mapungufu haya ni kama Hifadhi za Taifa Tanzania, Shirika la Simu Tanzania na Chuo Kikuu cha Ardhi.

### 11.3 Sera ya Teknolojia ya Habari

Sera ya teknolojia ya habari ni nyaraka inayoelekeza juu ya muundo na utekelezaji wa teknolojia ya habari kwenye shirika. Kabla ya sera hii kuanza kutumika, inatakiwa kupitishwa na uongozi wa shirika husika na baadaye zitawanywe kwa wafanyakazi wote ili zitumike kama mwongozo wa matumizi ya teknolojia ya habari katika shirika.

Hata hivyo, ilibainika kwamba, baadhi ya mashirika hayana sera zinazohusu teknolojia ya habari na baadhi yana sera hiyo lakini haikupitishwa na uongozi husika na nakala zilizopo hazijatawanywa kwa watumiaji. Udhaifu huu unapelekea kutokuwepo na miongozo ya matumizi ya teknolojia ya habari. Baadhi ya Mashirika yaliyo na mapungufu haya ni Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Shirika la Simu Tanzania na Hifadhi za Taifa Tanzania.

### 11.4 Usalama katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Usalama wa mifumo ya mawasiliano ya mashirika ni wa muhimu sana kwa ajili ya kulinda kumbukumbu za shirika

husika. Upembuzi katika teknolojia ya habari na mawasiliano ulibaini kuwa vyumba maalumu vya kuhifadhi kumbukumbu haviko imara katika kuhifadhi, kulinda na kuepuka uharibifu unaoweza kusababishwa na binadamu kwani vyumba hivyo hufungwa kwa kufuli ambazo ni nyepesi na rahisi kuvunjwa. Vyumba hivyo vimetengwa katika mazingira ambayo ni rahisi kufikiwa hata na watu wasioruhusiwa, hivyo kufanya kumbukumbu kuwa kwenye hatari ya kuharibiwa au kuibiwa.

Kwa kuwa mtandao wa kompyuta unaweza kufikiwa na mtu yeyote toka popote duniani, kuna hatari ya kuingiliwa na watu waharibifu na virusi haribifu. Mifumo ya kiulinzi kwa ajili ya kuzuia hatari hizo ni muhimu sana ili kulinda taarifa za ofisi. Kompyuta za Mashirika mbalimbali zimeunganishwa kwenye tovuti, watumiaji wanatumia mtandao kama kawaida, lakini hakuna hatua zozote za kiusalama zilizowekwa ili kuzuia hatari zinazoweza kujitokeza na kuharibu kumbukumbu za mashirika. Hali hii, ilibainika katika baadhi ya mashirika kama Chuo Kikuu cha Ardhi, Shirika la Simu Tanzania na Hifadhi za Taifa Tanzania.

#### 11.5 Ukosefu wa Mfumo wa Kompyuta wa Kutengeneza Hesabu

Katika ulimwengu wa sasa, kuna msisitizo mkubwa wa matumizi ya mfumo wa Kompyuta wa kuandaa hesabu kwa sababu unasaidia kutengeneza taarifa sahihi za hesabu na kwa wakati. Walakini mpaka sasa kuna mashirika na taasisi nyinginezo ambazo hazina mifumo ya kompyuta wa hesabu, na mashirika, mengine yanayo mifumo hiyo bali hayatumii mifumo hiyo kikamilifu na badala yake hutumia programu ya eksel kuandaa vitabu na taarifa za hesabu. Baadhi ya mashirika yanayohusika ni Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji Mwanza, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Dodoma, Mamlaka ya Kuendeleza Mji wa Dodoma, Ubungo Plaza, Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mji wa Musoma, Hospitali ya Taifa Muhimbili.

#### 11.6 Mpango wa Kudhibiti Maafa

Mpango wa kudhibiti maafa ni mkakati wa kuhakikisha kuwa biashara inaendelea bila kukwamishwa na janga lolote na linapotokea halisababishi kuharibika kwa kumbukumbu zote au hata sehemu ya mtandao. Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya mashirika si kwamba hayana mikakati ya kuepuka maafa yaliyotayari tu, bali hakuna hata mpango unaoweza kurejesha kumbukumbu endapo kutatokea upotevu au uharibifu. Kama Mashirika haya hayataweka mpango madhubuti wa kudhibiti maafa, kukitokea maafa yeyote, mashirika husika yatapoteza kumbukumbu muhimu ambazo zitapelekea hasara, kama vile kupoteza mapato, mikanganyiko katika kuendesha Mashirika, kupoteza ushindani na heshima ya shirika. Mashirika yaliyo husika ni pamoja na; Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Taasisi ya Takwimu ya Taifa, Hifadhi ya Taifa Tanzania, Mamlaka ya Taifa ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma na Baraza la Biashara la Taifa.

#### 11.7 Udhaifu Katika Miundombinu ya Mtandao wa Kompyuta

Mashirika ya Umma yanatumia mifumo mbalimbali inayoendeshwa kwenye kompyuta ili kutoa huduma ya kutunza kumbukumbu, barua pepe na tovuti. Pamoja na kwamba madhaifu haya yalikuwepo kwa mwaka uliopita, lakini bado mitandao inayotumika ambayo mifumo ya kompyuta imewekwa haiko kwenye hali nzuri, hali ambayo inahatarisha kukatika kwa mawasiliano kati ya watumiaji na mitambo ya kuhifadhi kumbukumbu. Kukatika kwa mawasiliano mara kwa mara kunakotokea kunaweza kukasababisha kupotea kwa kumbukumbu kati ya watumiaji hivyo kufanya usuluhisho kuwa mgumu ndani ya mfumo wa kompyuta. Tunashauri Mashirika ya Umma yaangalie uwezekano wa kuboresha mitandao yao ya kompyuta ambayo itawezesha kuhimili matakwa na mahitaji ya shughuli za Mashirika husika. Hii ni pamoja na kujumuisha kuweka mfumo thabiti utakaoweza kuimarisha utendaji kazi. Uwekaji wa miundombinu ya mtandao ambayo itarahisisha usimamizi wa karibu ni muhimu ili kurahisisha

kutatua matatizo ya mitandao katika maeneo ambapo hakuna kabisa au kuna wataalam wachache.

#### 11.8 Ukosefu wa Mafunzo ya Kutosha ya Kompyuta

Ni muhimu mno kwa watumiaji wa mfumo wa kompyuta kufundishwa namna ya matumizi ya mfumo huo. Makusudio makubwa ni kumfanya mtumiaji aupende na kuukubali mfumo huo. Tangu mwanzo mtumiaji anapaswa kupewa ujuzi wa mfumo utakaotumika. Pia, kama watumiaji hawatapewa elimu ya kutosha kunaweza kusababisha wasiupende mfumo wenyewe, pia wasiwe makini na mfumo huo. Kama mfumo haujakubalika tangu mwanzo watumiaji watahondwa kuutumia kwa ufasaha kama inavyotakiwa.

Hata hivyo kuna baadhi ya mashirika yamenunua mifumo mbalimbali ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kuitumia bila ya kutoa mafunzo kwa watumiaji. Mashirika mengine yametoa mafunzo yasiyotosheleza. Ni muhimu kwa kila muuzaji wa mtandao kuhakikisha anakabidhi mfumo kwa shirika husika baada ya kukamilisha taratibu za kuusimika mfumo huo na kisha kutoa hati ya makabidhiano ikiwa ni pamoja na kukamilisha taratibu zote. Hati ya makabidhiano ni uthibitisho kwamba matakwa ya mahitaji ya mkataba yalizingatiwa wakati wa mchakato wa kuusimika na kukabidhi mfumo huo. Katika upembuzi ilibainika kutokuwepo kwa mikataba wala maelekezo bayana ya kutumia baadhi ya mifumo iliyonunuliwa. Hali hii imepelekea kuwa na matatizo yasiyotatulika kwa watumiaji.

Kama hapatakuwa na mikataba iliyosainiwa, muuzaji hatalazimika kuuza mfumo husika kulingana na matakwa ya maelezo bainifu. Pia pasipokuwa na maelezo bainifu Shirika linaweza kununua mfumo usiokidhi mahitaji yake. Mashirika husika katika suala hili ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Mfuko wa kuwekeza Tanzania, TTCL na TPC.

- 11.9 Mfumo wa Usimamizi wa Bandari na Uangalizi wa Mizigo  
Mfumo wa usimamizi wa bandari ni mfumo wa mtandao uliobuniwa ili kusaidia uwakala wa kutoa na kusafirisha mizigo. Pia mfumo huu husaidia wafanyakazi wa Bandari kufahamu kwa ufasaha ni mizigo gani iliyopakuliwa na kubebwa katika meli zinazoingia na kutoka.

Wakati mfumo wa jumla wa uangalizi wa mizigo ni mfumo uliobuniwa kufuatilia na kutambua mizigo tangu meli inapotia nanga, mizigo inapopakuliwa na kuhifadhiwa, ukokotoaji wa tozo na ankara hufanyika kwa mujibu wa kitabu cha mamlaka ya bandari Tanzania cha tozo za bandarini kilichoanza kutumika tarehe 01/08/1999. Ukaguzi ulibaini kuwa mfumo huu kwa ujumla haufanyi kazi kikamilifu na kwa sehemu hutumia mfumo wa kompyuta na sehemu hutumia mfumo wa kawaida (manual). Hii ni kwa sababu sera ya magari haitoi maelezo ya kina ya nini kinachopaswa kufanyika, hivyo, inapotokea mfumo haufanyi kazi kabisa taarifa zinazotolewa baada ya hapo zinakuwa siyo za kuaminika.



**SURA YA KUMI NA MBILI**  
**MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU**

**12.0 Utangulizi**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza akafanya ukaguzi maalum au kwa kuombwa na mtu yeyote anayehusika, taasisi, mashirika ya umma, wizara, idara, wakala, mamlaka za serikali za mitaa na mamlaka yeyote kufanya ukaguzi wowote maalum. Kutokana na jukumu hilo la kisheria, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanya ukaguzi maalum katika Shirika la Maendeleo la Taifa kuhusiana na baadhi ya malipo baada ya kupata barua kutoka Bodi ya Wakurugenzi ya NDC yenye kumbukumbu namba CMD//AUDIT ya tarehe 19 Aprili, 2010 ikiomba kufanyika kwa ukaguzi maalum juu ya malipo mahsusni yaliyofanywa na menejimenti.

Kutokana na matokeo ya ukaguzi huo maalum, mapungufu yafuatayo yalibainika:

**12.1 Mapungufu Katika Hati za Mabadiliko Kwenye Mkataba wa Uthamini, Utambuzi na Uhakiki wa Mali za NDC**

Uchambuzi wa uhalali wa malipo ya shilingi milioni 82 yaliyofanywa kwa Kampuni ya M/s Trace Associates Limited ambayo ilipewa kazi na NDC kufanya uthamini, utambuzi na uhakiki wa mali za shirika kupitia mkataba wa tarehe 15 Mei, 2009 umegundua yafuatayo:

Hundi za malipo ya awamu mbili za kwanza zililipwa kwa mtoa huduma kwa kuzingatia masharti ya mkataba. Pamoja na kwamba malipo hayo yalifanywa kwa kuzingatia mkataba, uthamini huo ulileta mabadiliko ya bei (variations order) ambayo yalikuwa na mapungufu kama inavyoelezwa hapa chini.

Hapakuwa na hati rasmi za mabadiliko zilizotolewa kuelezea umuhimu wa kazi ya ziada kwa kiasi au kwa kupanda kwa bei ili kuthibitisha malipo ya ziada ya shilingi milioni 24. Nyaraka pekee iliyowasilishwa na menejimenti

ilikuwa ni barua yenye kumbukumbu Na.TRACE/NDC/Vol1/957 ya tarehe 13 Julai, 2009 kutoka Kampuni ya M/s Trace Associates Limited ikionyesha kuwa kulikuwa na makadirio ya chini ya kiwango cha kazi.

Hapakuwa na ushahidi kama mabadiliko hayo yaliidhinishwa na Bodi ya zabuni ya NDC na kupewa kibali na mwajiri. Huu ni ukiukwaji wa Kanuni ya Manunuzi ya Umma Na. 44 ya 2005 ambayo inataka mabadiliko yeyote kwenye thamani ya manunuzi au mikataba ya mauzo kupitiwa na kuidhinishwa na Bodi husika ya zabuni. Zaidi ya mapungufu hayo hapo juu, hapakuwa na mkataba mpya ulioandaliwa na kusainiwa kuthibitisha nyongeza hiyo.

#### 12.1.2 Mapungufu Yaliyotokana na Mkataba wa Kuweka Milango Migumu ya Mbao Themanini na Nane (88)

Uchambuzi wa malipo ya shilingi milioni 75.7 zilizolipwa kwa Kampuni ya M/s Classic Home Care kusambaza milango themanini na nane (88) ya mbao kwa ajili ya jengo la NDC ulibaini mambo yafuatayo:

Kwanza, kiasi kilichokubaliwa kwenye mkataba kwa ajili ya uagizaji wa milango kilifikia shilingi milioni 44.6 ikijumuisha kodi. Mpango wa malipo ya fedha zilizokubaliwa ulikuwa asilimia hamsini (50%) wakati wa kusaini mkataba, asilimia thelathini (30%) wakati wa kupokea milango na asilimia ishirini (20%) wakati wa kumaliza kazi. Hata hivyo, malipo yapatayo shilingi milioni 45.7 yalilipwa kwa M/s Classic Home Care Ltd, hivyo kusababisha malipo ya shilingi milioni 1.056 zaidi ya bei ya mkataba bila ya uthibitisho wowote.

Ilibainika pia kuwa, katibu wa bodi ya zabuni alitoa barua ya tuzo ya zabuni yenye kumbukumbu Na. S/NDC/6 ya tarehe 28 Septemba 2009 ikimuarifu mkandarasi kuleta na kufunga milango sitini na nane (68) ya mbao kwa mkataba wa gharama ya ziada ya shilingi milioni 49.931 kinyume na kifungu 33 (f) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004 ambayo inahitaji Afisa Mtendaji Mkuu kutoa maamuzi ya



tuzo ya zabuni. Hatukuweza kutambua vigezo vya ufikiwaji wa gharama hiyo ya mkataba kwa kuwa barua haikuonyesha dhahiri kiwango cha kazi itakayofanyika katika misingi ya kiasi cha vifaa vilivyotumika na gharama zake.

Baada ya maulizo juu ya uwepo wa nyongeza kwenye mkataba, imethibitika kuwa hapakuwa na nyongeza kwenye mkataba bali ilidhaniwa tu kwamba uletaji wa milango sitini na nane (68) ya ziada ilikuwa ni nyongeza ya mkataba uliokuwepo.

Zaidi ya hayo, mkataba wa kwanza wa kuleta na kufunga milango themanini na nane (88) uligharimu shilingi milioni 44.6 (sawa na Sh 507,400 kwa mlango mmoja), wakati awamu ya pili ya milango sitini na nane (68) ambayo ilidhaniwa kuwa ingeletwa kwa kuzingatia bei iliyopo iligharimu shilingi milioni 49.8 (i.e Tsh.734,290 kwa mlango mmoja). Kuna ushahidi kuwa mkataba wa pili mbali na kuwa uliingiwa kimakosa, ulikuwa na bei ya juu kwa shilingi milioni 15.428 (i.e. Tsh.734,290 - 507,400 mara milango 68). Zaidi ya hayo, bei ya mlango mmoja imeonekana kuwa kubwa kuliko bei ya soko na hivyo hapakuwa na zabuni shindanishi na hivyo hakukuwa na thamani ya fedha katika manunuzi haya.

#### 12.1.3 Hundi za Mzabuni Zililipwa Taslimu

Tulibaini kuwa hundi za kulipwa mtoa huduma hazikufungwa badala yake ziliandikwa kama hundi ambayo iko wazi ya kulipa fedha taslimu na hatimaye fedha kupokelewa kupitia kaunta ya benki na afisa mwandamizi wa NDC tarehe 3 Septemba 2009 badala ya kupitia akaunti ya benki ya mtoa huduma.

Hundi ya kwanza Na. 806118 ya kiasi cha shilingi milioni 12 ilihusu malipo ya ada ya kitaalam ya kusaidia upatikanaji wa hati miliki kwa NDC ya jengo lililoko Msasani Peninsular. Hundi hiyo ilikuwa ya kumlipa mtoa huduma lakini ililipwa kwa fedha taslimu. Tulibaini pia kuwa, hundi hiyo iliondolewa kwa makusudi kutoka kwenye kitabu cha fedha

na hivyo kutorekodiwa kwenye kitabu cha kutolea hundi na kuonyesha aliyeichukua.

Zaid ya hayo, ilibainika kuwa, mtoa huduma mnamo tarehe 26 Februari 2010 alilipwa shilingi milioni 2.5 kupitia hundi Na.929150 kwa mkataba uleule. Hali hii inaonyesha kuwa hundi ya hapo juu ya shilingi milioni 12 ililipwa kwa udanganyifu na hivyo kutoweza kutambua kwa uhakika wa huduma iliyotolewa kwa shirika kutokana na malipo hayo ya Sh.12,000,000. Tuna shaka kama kulikuwa na thamani ya fedha katika matumizi hayo.

Hundi ya pili Na.80613 ya shilingi milioni 23 iliyotakiwa kulipwa kwa Kampuni ya M/s Trace Associates kuhusiana na zoezi la kuthamini mali, lakini kwa makusudi haikufungwa na hivyo ikalipwa kwa fedha taslimu bila ya kuingizwa kwenye akaunti ya mtoa huduma. Hundi hii pia iliondolewa kutoka kwenye kitabu cha fedha na kitabu cha kuchukulia hundi kwa madhumuni ya kupoteza ushahidi.

Kutokana na matokeo ya ukaguzi huu maalum hapo juu, kuna wasiwasi juu ya usahihi wa malipo yaliyofanyika na tuliishauri Bodi ya Wakurugenzi kuchukua hatua muafaka juu ya tuhuma hizi za matumizi mabaya ya fedha za umma.

## SURA YA KUMI NA TATU

### HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 13.0 Utangulizi

Sura hii inahusu hitimisho na mapendekezo kwa mambo muhimu yaliyobainika katika ukaguzi ambayo yanahitaji kuangaliwa na Serikali na Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti husika za Mashirika na Taasisi za Umma. Mapendekezo haya yanatolewa kulingana na mamlaka niliyopewa chini ya kifungu Na. 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya mwaka 2008 kwa madhumuni ya kuzuia na kupunguza matumizi ya fedha za umma yasiyokuwa na tija, kuongeza ukusanyaji wa mapato ya umma na kuzuia hasara zinazotokana na uzembe, wizi, udanganyifu, na kugushi fedha na matumizi mabaya ya rasimali za umma kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

Baada ya kumaliza ukaguzi wa hesabu za mashirika ya umma yapatayo 122 ambayo hesabu zake zilipitishwa na Bodi za Wakurugenzi kwa miaka ya fedha inayoishia tarehe 30 Septemba, 2009, 31 Disemba 2009 na 30 June 2010 kwa pamoja kwa kutumia mamlaka niliyopewa kikatiba, napenda kutoa mapendekezo ya ujumla katika kila sura yatokanayo na ukaguzi wa mashirika na taasisi zinginezo za umma kwa kipindi husika kama ifuatavyo:-

#### 13.1 Hati za Ukaguzi

Hadi kufikia tarehe 25 Februari 2011, nimeweza kukagua hesabu za mashirika 122 ikiwa ni asilimia 71.7 ya hesabu za mashirika 170 yanayotakiwa kuwasilisha hesabu zao kwangu kwa ukaguzi. Kati ya mashirika ambayo kaguzi zake zilikamilika, mashirika 92 yalipata hati safi ikiwa ni asilimia 75.4, wakati mashirika 12 yamepata hati safi yenye masuala ya msisitizo ikiwa ni asilimia 9.8, na pia mashirika 10 yamepata hati isiyoridhisha ikiwa ni asilimia 8.2 ya mashirika. Katika ukaguzi huu mashirika ya umma 7 ikiwa ni sawa na asilimia 5.8 yalipata hati isiyoridhisha yenye masuala ya msisitizo. Kwa upande mwingine, shirika moja 1

ikiwa ni sawa na asilimia 0.8 lilipata hati chafu (disclaimer) kwani nilishindwa kutoa maoni na hakuna shirika lililopata hati mbaya (adverse). Undani na mchanganuo wa maelezo ya hati za ukaguzi yameainishwa kwenye kiambatisho II cha taarifa hii.

### 13.2 Mapendekezo ya Miaka iliyopita ambayo Hayajatekelezwa

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa majibu yake kwa taarifa zangu za miaka iliyopita kuhusu mapendekezo niliyoyatoa kwa Serikali. Kwa ujumla majibu yaliyotolewa hayakushughulikiwa kikamilifu na hayakukidhi mapendekezo yote niliyoyatoa. Jitihada zaidi na umakini vinahitajika katika kutoa majibu kikamilifu au maelezo ya namna ambavyo Serikali imejipanga kutekeleza mapendekezo hayo.

Mapendekezo mengi bado hayajatekelezwa na machache yako kwenye hatua ya utekelezaji. Ninashauri jitihada za ziada zichukuliwe na Serikali, Bunge, Bodi za wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma kuhakikisha kuwa mapendekezo yote yaliyotolewa kwenye taarifa zilizopita yanatekelezwa kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa Mashirika na Taasisi zetu za Umma.

### 13.3 Masuala Muhimu ambayo Hayakutolewa Taarifa kwenye Ripoti ya Mwaka Uliotangulia

Kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kinahitaji kwamba kila Shirika la Umma lazima liwasilishe hesabu kwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha wa hesabu husika. Tumepata uzoefu wa kutofuatwa kwa kiasi kikubwa kwa kifungu hiki cha Sheria kwa baadhi ya Mashirika ya Umma na kusababisha kaguzi kufanyika kwenye mwaka mwingine wa mwaka wa hasabu na kusababisha Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kushindwa kuyatolea taarifa kwenye mwaka husika. Hiki ni kikwazo kikubwa ambacho kama hakitafanyiwa kazi

kitarudisha nyuma dhana ya uwajibikaji tuliyoanza kuijenga miongoni mwa Mashirika ya Umma.

#### Mapendekezo

Nashauri Msajili wa Hazina kama mhifadhi mkuu wa kusimamia uwekezaji wa umma kuendelea kukazia katika jambo hili na kuyaamuru mashirika yawasilishe hasabu zao kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

### 13.4 Usimamizi wa Mapato na Matumizi

#### Usimamizi wa Mapato

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kuangalia mapato katika mashirika ya umma kulibainika kuwepo kwa mapungufu katika usimamizi wa mapato. Mashirika mbalimbali yalionekana kutokuwa na ufanisi katika ukusanyaji wa madeni ya muda mrefu kiasi cha shilingi bilioni 52.2. Utoaji ankara zisizokuwa sahihi kwa wateja, uvujaji wa kiwango kikubwa cha maji katika mamlaka za maji na kupotea kwa umeme uliozalishwa na TANESCO vimepelekea kupoteza mapato. Pia, kumekuwepo na ucheleweshwaji wa fedha za bajeti kutoka Hazina na kutoka katika wizara mama za mashirika. Ucheleweshaji huu, hukwamisha shughuli za mashirika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Dosari nyingine ni zile za kutokuonyesha na kuingiza vitabuni mapato katika vitabu vya hesabu kama viwango vya kihasibu vinavyoainisha na kutokuoanisha mapato kwenye vitabu vya hesabu na taarifa au mifumo mingine inayorekodi taarifa za mapato imeonekana kuwa na mapungufu kwenye mashirika mengi hali ambayo inaweza kupelekea kuwepo kwa udanganyifu na kupotea kwa mapato. Pia Mashirika mengine yaliingiza vitabuni faida na hasara tofauti ya sarafu bila kuwepo viambatanisho vinavyo onyesha usahihi wake.

#### Mapendekezo

Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wa Mashirika ya Umma wahakikishe kwamba, mikakati madhubuti ya

kukusanya madeni ya nyuma inakuwepo. Mamlaka za Maji ziimarisha miundombinu ya maji. Pia mamlaka za maji na TANESCO ziboreshe mifumo ya kuandika ankara kwa wateja iwe ya kisasa na mita za kurekodi vipimo iwe sahihi ili kuongeza mapato na kukidhi matakwana ya EWURA. TANESCO pia iwe na mikakati ya kuepuka upotevu wa umeme. Ili kuwepo utendaji mzuri wa kazi katika Mashirika. Fedha za bajeti zitolewe mapema na Hazina na Wizara mama, mapato yaonyeshwe kiusahihi kwa kufuata viwango vya hesabu na uoanishi wa mapato kutoka vitabu vya hesabu na mifumo mingine ya ripoti ili kuzuia udanganyifu. Shirika la viwango liboreshe mifumo ya kugundua nyaraka za kugushi za waagizaji magari yasiyokaguliwa ili faini kubwa zitozwe kukomesha uingizaji wa mali zilizo chini ya kiwango.

### 13.5 Usimamizi wa Matumizi

Uchunguzi wa usimamizi wa matumizi katika Mashirika ya Umma uligundua kuwepo kwa mapungufu kadhaa katika usimamizi wa matumizi, ambayo ni kama kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani katika matumizi, kutokuwa na viambatanishi muhimu vya matumizi, malipo kufanyika bila kuwepo hati za manunuzi (LPO) na bila kujaza fomu za kuagizia mali.

Pia mapungufu mengine ni kama kutorejeshwa kwa masurufu, kutokata mikopo ya mishahara inayotolewa kwenye mishahara ya miezi inayofuata, kutokuwepo kwa udhibiti wa bajeti kunakosababisha matumizi zaidi ya bajeti, ulipaji wa posho na matumizi mbalimbali kinyume na sheria za fedha, kutozingatia sheria na sera za ukopesaji magari. Mapungufu mengine ni kutodhibiti vifaa vitokavyo stoo na kutodhibiti utumiaji wa kemikali za maabara katika hospitali kunakopelekea kuongezeka kwa gharama za vifaa hivyo. Kwa upande mwingine kumekuwepo na kutokuoanisha Mishahara inayotoka Hazina na ile inayoandaliwa na Mashirika ya Umma. Pia kumeonekana kutokuwepo vitabu vya kutunza kumbukumbu za matumizi ya gari katika baadhi ya Mashirika ya Umma.

## Mapendekezo

Serikali, Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wanatakiwa kuhakikisha matumizi katika mashirika ya umma yanasimamiwa kwa umadhubuti ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za Umma. Masurufu yarejeshwe kwa wakati kama ilivyoainishwa kwenye sheria za fedha na masurufu mapya yasitolewe kabla ya kurejesha ya zamani, malipo yaambatanishwe na nyaraka zote muhimu na matumizi yote yaendane na bajeti.

Kuwepo na udhibiti wa matumizi ya vifaa vinavyotoka stoo na kemikali za maabara ili kupunguza kuongezeka kwa gharama na udanganyifu. Mikopo ya magari na mikopo mingine izingatie sera zilizowekwa kuepuka athari ya kupoteza fedha za umma, kuoanisha mishahara inayotolewa na Hazina kila wakati na yakiwepo mabadiliko taarifa iwasilishwe Hazina mapema.

### 13.6. Kuchelewa kwa Utekelezaji wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa

Baraza la Mawaziri liliidhinisha mpango wa kutekeleza mradi mwaka 2007, ambapo mradi ulipangwa kuanza mwezi Julai 2008 hadi Disemba 2009 kwa awamu mbili ambazo ni; kuchambua gharama za uendeleshaji wa Mamlaka ya taifa ya Vitambulisho na kutambua gharama halisi za utekelezaji wa mradi.

Pia, tulibaini kuwa Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Mambo ya ndani iliidhinisha zabuni kwa ajili ya kazi hii tarehe 20 Septemba, 2008 baada ya hapo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ilisaini mkataba na Gotham International Limited tarehe 13 Januari, 2010 kutoa huduma ya Ushauri wa menejimenti kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa vitambulisho vya Taifa kwa kutumia teknolojia ya SMART CARD. Jumla ya gharama za mkataba ni dola za kimarekani milioni 9 na muda wa mkataba ni miaka mitano (5) kuanzia tarehe 14 Januari, 2010.

Kulingana na kifungu cha 19.2(1) cha mkataba, kiasi cha dola za kimarekani milioni 2.7 sawa na shilingi bilioni. 3.6 za kitanzania zililipwa kwa kampuni ya Gotham International Limited baada ya mshauri kuandaa ripoti ya upembuzi wa mradi na waraka wa mapendekezo (RFP) ambapo makampuni 154 yaliwasilisha nyaraka za zabuni. Baada ya uchambuzi, wazabuni 54 waliteuliwa na baadaye wazabuni 5 walichaguliwa. Kamati ya tathmini ya Zabuni iko kwenye mchakato wa kuchagua kampuni moja itakayokuwa mkandarasi wa kuchapisha Vitambulisho vya Taifa vinavyotarajiwa kuanza kutengenezwa kwa majaribio mwezi Machi, 2011.

Mshauri ameweza kuandaa na kuwasilisha mpango wa vitambulisho vya Taifa, ajira za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Sera na Mpango wa Mawasiliano. Hata hivyo, tumebaini kwamba, mradi umechukua muda wa mwaka mmoja tangu tarehe ambayo Bodi ya Zabuni ya Wizara itoe idhini kwa ajili ya kazi ya ushauri na kusaini mkataba na hakuna sababu za msingi zilizotolewa.

Ucheleweshwaji huu una athari katika kufikia malengo ya shughuli za mradi. Tunashauri kwamba menejimenti iongeze juhudi na kuongeza kasi ya mradi wa Vitambulisho vya Taifa kwa manufaa ya raia wa Tanzania.

#### 13.7. Usimamizi wa Sheria ya Manunuzi na Mikataba

Kuanzishwa kwa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 zinatoa mwongozo wa kisheria kuhusu namna manunuzi yatakavyofanyika. Pamoja na kuwepo kwa Sheria, Mashirika ya Umma yameendelea kutozingatia kikamilifu sheria na kanuni katika kutekeleza shughuli zake. Hali hiyo imeonyesha kuwa hakuna elimu ya kutosha katika mashirika kuhusiana na Sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005. Hali hiyo inathibitishwa na mapungufu yaliyoainishwa kwenye taarifa hii.



Vilevile, ukaguzi wa mashirika ya umma umebaini kutokuwepo kwa uwazi na ufanisi katika kutekeleza shughuli za manunuzi ili kufikia lengo la thamani ya fedha na katika kusimamia mikataba.

#### Mapendekezo

Mamlaka ya Udhhibiti wa Manunuzi ya Umma iendelee na jitihada zake za kuyajengea uwezo Mashirika ya Umma na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi katika Mashirika ya Umma unaimarika.

Pia, Bodi ya Ugavi na Ununuzi iweke mkazo katika kuendeleza uandaaji wa wataalam wa ununuzi, kutoa mafunzo na kuendeleza mitaala ili kufikia mahitaji ya soko nchini.

Bodi za Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wahakikishe kuwa sheria ya manunuzi ya mwaka 2004 na Kanuni zake za 2005 zinazingatiwa. Pia, wahakikishe kunakuwepo na mfumo maalumu wa kusimamia mikataba ili kuleta ufanisi.

#### 13.8. Usimamizi wa Raslimali

Tumebaini kuwa, baadhi ya mashirika ya umma bado yanafanya uwekezaji katika kampuni ambazo hazijiendeshi kwa faida. Aina hizi za uwekezaji zinaweza kutumika kama vyanzo vya ufujaji wa fedha za umma na hatimaye kusababisha hasara kwa fedha ambazo zingetumika katika kutekeleza miradi mingine ya maendeleo. Tatizo lingine kubwa lililobainika ni baadhi ya mashirika ya umma kukosa hati miliki za mali kama vile, ardhi na majengo. Vilevile, kuna tatizo la tafsiri na utekelezaji wa viwango vya kihasibu vya kimataifa kuhusu uchakavu wa mashine na mitambo. Mapungufu mengine yaliyoonekana ni kukosa bima kwa baadhi ya mali, kutokusanya na kutolipa madeni na kutosimamia vizuri bakaa za mwisho wa mwaka za mali kwenye bohari.

### Mapendekezo

Serikali, Bodi za Wakurugenzi, Maafisa Watendaji wa mashirika wahakikishe wanawekeza kwenye kampuni zinazofanya vizuri kiutendaji ili kuweza kupata faida kwenye uwekezaji. Pia, Bodi za Wakurugenzi za mashirika ya umma wahakikishe wanapata umiliki wa mali na mitambo. Vile vile, Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu wafanye utafiti utakaowezesha kutoa muongozo wa makadirio ya viwango vya uchakavu ambavyo vinaendana na hali halisi ya matumizi na muda wa maisha ya mitambo na mali zinazomilikiwa na mashirika.

### 13.9. Usimamizi wa Raslimali Watu

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni kwenye sura ya nane, uchambuzi wa usimamizi wa raslimali watu umegundua, miongoni mwa mambo mengine mapungufu yafuatayo; majalada ya watumishi kutorekebishwa kwa wakati, miongozo ya ajira iliyopitwa na wakati, udhaifu katika mafunzo ya wafanyakazi au kutokuwepo kwa mafunzo, udhaifu katika upimaji utendaji kazi, upungufu wa wafanyakazi, ucheleweshwaji wa malipo ya mishahara, ulipaji wa mishahara chini ya kima cha chini na ucheleweshwaji wa kuwasilisha michango ya pensheni ya wafanyakazi.

### Mapendekezo

Kuhusiana na upungufu wa wafanyakazi, hasa nafasi za kiuongozi, tunashauri kwamba nafasi zote zilizo wazi kama ilivyo katika chati za kiuongozi na zile zinazokaimiwa zijazwe. Pia, mashirika yahakikishe kuwepo kwa mpango mzuri wa kurithisha madaraka.

Menejimenti ya Mashirika ya Umma zichukue hatua zinazofaa kwa lengo la kupitia upya mishahara na marupurupu ya wafanyakazi ili yaendane na masharti ya ajira ya mamlaka husika pamoja na maelekezo ya Serikali kuhusu ulipaji wa mishahara. Mashirika ya umma lazima pia yahakikishe kuwa mishahara inalipwa kwa wakati.

Usimamizi mzuri katika suala la ulipaji mishahara utawapa motisha wafanyakazi kuendelea kufanya kazi kwa muda mrefu na hii itapunguza idadi ya wafanyakazi wanaoacha kazi na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Kwa upande wa tathmini ya utendaji kazi, ni lazima menejimenti kufanya juhudi ya kutosha kuwezesha mawasiliano bora, ya wazi mara kwa mara kati ya kiongozi wa kazi na mwajiriwa; kutengeneza mahusiano mazuri kati ya kiongozi wa kazi na mwajiriwa kuhusiana na wajibu na majukumu ya kazi ya mwajiriwa na malengo ya ufanisi yaliyowekwa kwa kipindi husika; kutambua na kutatua masuala ya kiufanisi na kuipatia menejimenti taarifa muhimu kwa ajili ya kusaidia maamuzi ya watumishi ambao huhitaji tathmini juu ya utendaji kazi wa kila mmoja wao. Njia nzuri ya kufikia lengo hili ni kutumia mfumo wa wazi wa upimaji utendaji kazi na kuhakikisha kwamba fomu za kupima utendaji kazi zinajazwa na kuhifadhiwa ipasavyo katika jalada la mwajiriwa husika ili kuweka mtiririko wa utendaji kazi wa mfanyakazi.

Kuhusiana na suala la utunzaji wa kumbukumbu za waajiriwa, inashauriwa kwamba Mashirika ya umma yahakikishe kuwa kumbukumbu za waajiriwa zinatunzwa vizuri pamoja na kumbukumbu zote zinazohusiana na mabadiliko ya masharti ya ajira na taarifa nyinginezo kama vile fomu za tathmini ya utendaji kazi na nyinginezo kwa ajili ya utambulisho wa mfanyakazi zinatunzwa vizuri.

### 13.10. Utawala Bora

#### I. Utekelezaji wa Mapendekezo ya CAG

Katika kutekeleza matakwa ya kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 kuhusu mamlaka ya CAG kutoa mapendekezo kwa Serikali, tumekuwa tukitoa mapendekezo mbalimbali ya kitaalamu juu ya namna ambavyo Serikali inaweza kuboresha utendaji katika mashirika ya umma. Hata hivyo, tumebaini kuwa yapo mapendekezo mengi ambayo hayajatekelezwa, kitu

ambacho kinapelekea kuwoko kwa mapungufu yale yale kila mwaka kama vile kuendelea kuwaona waheshimiwa Wabunge wakiwa wajumbe wa Bodi katika mashirika ya umma na masuala mengine kama yalivyoainishwa katika sura ya tatu na ya nne ya ripoti hii.

#### Mapendekezo

Tunapendekeza kuwa wakati sasa umefika kwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na vyombo vingine vinavyohusika kushughulikia suala hili kikamilifu.

### II. Kanuni za Mgawanyo wa Madaraka Katika Utendaji wa Mashirika ya Umma

Mgawanyo wa madaraka ni kanuni muhimu katika mfumo wa udhibiti wa ndani na utawala bora katika mashirika yetu ya umma kwa kuwa kunapunguza hatari ya kuwepo kwa makosa kutokana na ufuatiliaji mkubwa katika maamuzi mbalimbali. Kanuni hii inasaidia sana katika kupambana na ubadhirifu kwa kupambana na utawala mbaya kwa kuwa angalau watu wawili wanapitia kabla malipo au maamuzi kufanyika. Tumbaini kuwa kanuni hii ya mgawanyo wa madaraka katika uendesaji wa mashirika ya umma bado haizingatiwi ipasavyo kwani bado kuna muingiliano mkubwa katika shughuli za kiutendaji kwa wajumbe wa bodi, wabunge na Serikali kwa mtendaji kuhoji maamuzi aliyoyatoa awali. Kwa aina hii ya utawala wa mashirika ya umma, bila shaka ni vigumu kupata tija.

#### Mapendekezo

Tunapendekeza kuwa Serikali, Bunge na Mahakama walisitize na kulisimamia suala la mgawanyo wa madaraka na majukumu katika utendaji wa Serikali na taasisi zake. Pia, juhudi zaidi zinahitajika kuhakikisha kuwa kanuni za utawala bora katika mashirika zinaelekezwa hadi ngazi za chini za utendaji.

### III. Udhaifu Katika Utendaji wa Bodi za Wakurugenzi

Utendaji wa bodi za wakurugenzi katika mashirika ya umma una maana kubwa katika kuyaongoza mashirika. Mapungufu

yaliyoonekana katika bodi mbalimbali za wakurugenzi na taswira yake kwa jamii ni ishara tosha ya udhaifu uliopo katika utendaji wa bodi kama ulivyoonekana katika sura ya tisa.

#### Mapendekezo

Tunapendekeza kuwa Msajili wa Hazina alitazame suala hili kiundani dhidi ya malengo ya uanzishwaji wa mashirika na kuchukua hatua madhubuti itakapobidi na kutupatia nakala ya uamuzi huo kwa hatua za ufuatiliaji.

#### IV. Mgongano wa Kimaslahi kwa Wabunge kuwa Wajumbe Katika Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma

Kama ilivyopendekezwa katika ripoti zilizopita na kwa kuwa Bunge ni chombo cha juu cha uwakilishi wa watu chenye majukumu ya kuangalia utendaji wa Mashirika ya Umma kupitia POAC, na ili kuondoa migongano ya kimaslahi, wabunge hawapaswi kuwa wajumbe katika Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma ambazo wanazisimamia. Kwa mujibu wa kanuni bora za utendaji, utaratibu huu hautumiki katika nchi yoyote ambayo ni mwanachama wa mashirikisho kama vile EAC, SADCOPAC, SADC, AFROSAI-E au EU.

#### V. Utendaji wa Kamati za Ukaguzi na Wakaguzi wa Ndani

Sheria ya Sarbanes-Oxley inataka wajumbe wote wa kamati za ukaguzi wawe huru na angalau mjumbe mmoja awe na ufahamu wa masuala ya uhasibu na usimamizi wa fedha. Pia, inatakiwa kuwa kamati za ukaguzi ziwe na hati au idhini ambayo itatakiwa ipitiwe upya kila mwaka kuonyesha wigo, muundo na taratibu za kamati ya ukaguzi. Kamati hii ni mhimili wa msingi wa utendaji kazi bora wa wakaguzi wa ndani na uhakika wa mfumo wa udhibiti wa ndani kwa bodi. Tumebaini kuwa mashirika mengi ya umma hayakufanya vizuri kwenye uundaji wa mfumo hii ya kamati ya ukaguzi na vitengo vya ukaguzi wa ndani hivyo kusababisha kuendelea kutolewa kwa hoja za kikaguzi kama vile wigo finyu wa ukaguzi wa ndani, kushiriki kwa wakaguzi wa ndani katika ukaguzi wa hati za malipo kabla ya malipo,

upungufu wa wafanyakazi na ukosefu wa hati ya ukaguzi wa ndani na kamati za ukaguzi.

#### Mapendekezo

Inapendekezwa kwamba miundo ya ukaguzi wa ndani na ya kamati za ukaguzi iundwe ipasavyo kwa ajili tathmini ya udhitibi wa ndani wenye nguvu.

#### VI. Bodi za Wakurugenzi Kuingilia Kazi za Menejimenti

Bodi za wakurugenzi kuingilia kazi za menejimenti inaathiri kazi zake za kiuangalizi katika kusimamia kazi za menejimenti. Miongoni mwa kazi za Bodi za Wakurugenzi ni kutunga sera kuhusu masuala yote yanayoathiri shirika, kuweka mipango, kutengeneza mifumo ya utumishi na kuhakikisha shirika linakuwa imara kifedha. Migongano ya kimaslahi itapunguza hamasa kwa menejimenti katika utendaji wa kazi na wajibu kulingana na malengo yaliyowekwa. Mgongano huo unaweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya shirika.

#### Mapendekezo

Masuala ya kiutendaji ya shirika yanatakiwa kutekelezwa na menejimenti na Bodi ya Wakurugenzi inatakiwa kutathmini utendaji wa menejimenti katika kufikia mpango kazi wa mwaka na mpango mkakati wa shirika. Bodi za wakurugenzi zipewe mafunzo juu ya kazi na wajibu wao na lazima iwe na miongozo ya bodi ambayo itafafanua kazi, wajibu na jinsi ya kuunda bodi na kamati zake.

#### VII. Kutofuatwa kwa Kanuni za Serikali Kuhusu Ada za Wakurugenzi

Katika kanuni za utawala bora, ada za wakurugenzi zinapangwa na wanahisa ambapo kwa mashirika ya umma, ni Msajili wa Hazina au Waziri anayesimamia shughuli husika. Zaidi ya hayo, ada za wakurugenzi hazitegemewi kutokana na kigezo cha ufanisi kwa sababu inaweza kusababisha kusukwa kwa taarifa za hesabu. Kudhibiti ada za wakurugenzi na matumizi mengine makubwa yatapunguza kwa kiasi kikubwa matumizi yanayoongezeka

ya Mashirika ya Umma. Bodi za Wakurugenzi zinatakiwa kufanya kazi ya kiushauri ya kuongeza mapato ya shirika, kuongeza ufanisi na kupunguza matumizi na si vinginevyo.

#### Mapendekezo

Tunashauri kwamba, mamlaka husika zifuate maelekezo na kanuni zitolewazo na Serikali. Mamlaka husika iombe maelekezo ya Serikali kuhusu maamuzi yanayohusu gawiwo la faida kwa kuwa Serikali ndiye mwanahisa pekee na ana haki ya kutoa maamuzi kupitia Msajili wa Hazina au waziri. Serikali lazima itoe maelekezo mahususi jinsi ya kupanga posho za wakurugenzi wanaohudumia Mashirika ya Umma ili kuondoa mazoea ya wakurugenzi ya kujipangia posho zao bila idhini ya Msajili wa Hazina au Waziri.

#### VIII. Kutokufuata Waraka wa Msajili wa Hazina

Wizara ya Fedha ilitoa waraka wa Hazina Na.8 unaoyataka Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kuchangia asilimia 10 ya mapato yote kabla ya matumizi yatokanayo na shughuli za uzalishaji kwenda Hazina. Baadhi ya Mashirika hayakutekeleza matakwa ya waraka huu, hali hii ilionekana katika mashirika mawili na shirika moja kupitia kikao chake cha Bodi ya Wakurugenzi iliamuliwa kuwa mchango wa Hazina uwe asilimia 10 ya faida iliyopatikana na si mapato kabla ya matumizi, hii ni kinyume na waraka uliotolewa na serikali na hapakuwa na mabadiliko yeyote kuhusu waraka huu. Uamuzi kama huu wa Bodi ni kitendo cha kupinga uamuzi halali wa Serikali.

#### Mapendekezo

Mamlaka zote zinatakiwa kuhakikisha kuwa zinafuata maagizo yanayotolewa na Serikali na pia kutoa michango yao kwa Hazina kama waraka ulivyoelekeza. Pale ambapo Mamlaka haziwezi kufuata maagizo, basi zitoe taarifa kwa chombo husika ili kupata ruhusa za kufanya vinginevyo. Msajili wa Hazina anatakiwa kuonyesha kuwa, ndiye mmiliki wa Mashirika na aanzishe sera za kudumu za kuwa mmiliki. Zaidi ya hayo, Msajili ahakikishe utawala wa Mashirika ya Umma unakuwa wa uwazi na endelevu na wa ufanisi.

Inategemewa kuwa Msajili wa Hazina ataanzisha sera ya umiliki ambayo itaainisha malengo ya Msajili wa Hazina na majukumu ya utawala bora kwenye Mashirika ya Umma na namna ya utekelezaji wa sera.

#### 13.11. Mashirika Yaliyotengwa kwa Ajili ya Kubinafsishwa

Mashirika ya Umma 34 yaliyotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa na Serikali na yakachukuliwa kutoka Tume ya Rais ya Ubinafsishaji wa sekta za umma (PSRC) na kuwekwa chini ya Shirika Hodhi la Mali za Makampuni yaliyobinafsishwa (CHC), bado yapo chini ya ubinafsishwaji mpaka wakati huu wa kuandika ripoti hii. Hii ni ishara ya kutokuwepo ufanisi kwenye utendaji wa Shirika Hodhi la mali za makampuni yaliyobinafsishwa, Mashirika hayo yaliyochukuliwa yalikuwa kwenye hatua za kubinafsishwa tangu tarehe 1 Januari 2008. Itambulike kwamba Mashirika yanayotengwa kwa ajili ya kubinafsishwa, yanakuwa yameondolewa na upeo wa kupanuka zaidi kwa sababu hayawezi kutengeneza na kutekeleza mipango mikakati au kuruhusiwa kuwekeza. Pia wafanyakazi wa mashirika haya wanakuwa hawana motisha ya kufanya kazi au kutimiza wajibu wao kwa kujituma ikiwa ni sababu ya kutokuwa na uhakika wa kudumu katika kazi. Uchakavu wa mali na raslimali nyingine zinazomilikiwa na mashirika yaliyotengwa unakuwa ni wa hali ya juu kutokana na kwamba ukarabati au urudishwaji wa mali zilizoharibika unakuwa mgumu kutokana na ukosefu wa fedha.

#### Mapendekezo

Serikali inatakiwa kufikiria aidha kuharakisha ubinafsishwaji wa mashirika 34 yalitotengwa kwa ajili ya ubinafsishwaji yaliyotoka PSRC na kuchukuliwa na CHC ili kuepuka uharibifu na uchakavu wa raslimali zinazomilikiwa na mashirika yaliyotengwa au Serikali kutoyabinafsisha na kuyaongezea mitaji na yaanze kazi upya.



### 13.12. Kipimo cha Utendaji wa Mashirika na Hali Baada ya Ubinafsishaji

Uendeshwaji wa mashirika ya umma kwa mwaka unaohusika umepimwa kwa ubora wa hesabu zake hasahasa madeni ya muda mrefu yaliyodhaminiwa na serikali ambayo ilikuwa imebakia shilingi bilioni 451, makusanyo ya gawiwo na Msajili wa Hazina, ulipaji wa madeni na malipo mengine ambayo umepungua kwa shilingi bilioni 42.5 ikilinganishwa na mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 June, 2009, mikopo iliyosalia imepungua kwa shilingi bilion 21, uwekezaji wa Serikali na uwekezaji binafsi umepungua kwa shilingi milioni 27.

Baada ya ubinafsishaji uendeshaji wa mashirika ya umma unapimwa kwa kuangalia kiasi cha fedha kilichowekezwa na mwekezaji, matengenezo yaliofanyika kwenye majengo mitambo na mashine, kiasi cha kodi kilicholipwa serikalini na makampuni na nafasi za kazi zilizopatikana.

#### Mapendekezo

Mashirika yafanye ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha uendeshaji wa mashirika unaboreka na gharama za uendeshaji kupungua.

Ili kuboresha uendeshaji, mashirika ambayo mitambo na mashine zake hazifanyi kazi vizuri na kuhitajika kununua mitambo na mashine imara na za kisasa ili kuongeza uzalishaji badala ya kupoteza hela nyingi kwenye matengenezo. Pia, serikali kwa kupitia TANESCO ihakikishe upatikanaji wa umeme wa kutosha viwandani ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza uzalishaji.

Wawekezaji ambao bado wanadaiwa pesa za uwekezaji inabidi walipe madeni yao na faida iliyozalishwa kama mkataba wa kuuziana unavyosema.

Mikataba wa kuuziana irekebishwe kuelezea hatua za kuchukuliwa kufuatia kushindwa kwa mwekezaji kutekeleza

mpangilio wa kuwekeza na pia ili kulinda viwanda vya hapa nchini na bidhaa ambazo zipo na zinatoshesheleza mahitaji. Wawekezaji waambatanishe mipango yao mipya ya uwekezaji kwenye mikakati yao ya uendesaji na ya masoko kama vile kutangaza ili kuendana na ushindani wa biashara.

Mashirika yahakikishe hesabu zao zinatayarishwa na kukaguliwa kwa wakati. Mashirika ambayo hesabu zao ziko tayari kwa kukaguliwa, hesabu hizo zikaguliwe ili tuweze kupima utendaji wake.

Mashirika yatafute njia ya kuinua mitaji yao ili kuweza kutekeleza mikakati mbalimbali ya masoko kwa ajili ya kuongeza mapato.

Kuhusiana na masuala ya Ardhi yanayotokana na utekelezaji wa makubaliano wa manunuzi, ni muhimu kuweka mapendekezo ya kulipa fidia, ili kutatua tatizo hili la muda mrefu.

Uongozi wa mashirika utafute mitaji kutoka kwenye mabanki ili kupanua biashara na kutumia mali ya kampuni kama dhamana.

Maamuzi ya hivi karibuni yaliyofanywa na TANAPA ya kutoza viingilio vya utalii kwa asilimia ya mapato yaliokusanywa yabadilishwe na kurudia mfumo wa zamani wa kutoza viingilio kwa kiwango maalum (fixed rate).

Serikali itafute namna ya kutatua changamoto zinazoikabili bodi ya mikopo ya elimu ya juu kwa sababu kadiri suluhisho la changamoto hizi zinavyochelewa, zinasababisha udhaifu katika utendaji wa bodi na hivyo kusababisha manunguniko na pengine migomo ya wanafunzi.

### 13.13. Mashirika Ambayo Umiliki na Usimamizi wake Unapaswa kuwa Chini ya Serikali

Baadhi ya mashirika ya umma yanatakiwa yawe chini ya umiliki wa Serikali kutokana na aina ya huduma yanazozitoa kwa taifa. Kwa mfano ATCL ni Shirika la Taifa na ni alama ya utambulisho wa taifa nje ya nchi ambalo linaweza kuitangaza Tanzania na kuinua utalii. Vivyo hivyo, kuzorota kwa utoaji umeme wa uhakika kwa TANESCO kumesababisha kushuka kwa kiwango cha uzalishaji, mapato kidogo ya kodi, kupungua kwa ajira, kuongezeka kwa bei za bidhaa na mengineyo. Kwa upande mwingine suala la usafiri ni tatizo hasa kwa wananchi, hasa wanafunzi. Kama Serikali ingeliwezesha Shirika la Usafiri Dar es salaam (UDA) kujiendesha hata kwa nusu ya uwezo wa wasafirishaji binafsi, tatizo hili kwa wananchi wa kawaida lingeweza kupungua kwa kiasi kikubwa. Kuyaacha Mashirika ya Umma kwenye mikono ya wamiliki binafsi kunaleta hatari kwa uhuru wetu na mchango kwa uchumi wa nchi. Makampuni yanayomilikiwa na watu binafsi yanakulenga zaidi kupata faida kuliko kutoa huduma kwa wananchi na maendeleo kwa nchi.

#### Mapendekezo

Serikali izingatie umiliki wa Mashirika yote muhimu ambayo hutoa huduma za msingi kwa umma. Zaidi ya hayo, menejimenti ya mashirika haya lazima zisimamiwe kuhakikisha utoaji wa huduma wa uhakika na kuaminika. Panapotokea matatizo ya kifedha, Serikali ihakikishe inatoa msaada unaohitajika na kwa wakati.

### 13.14. Mitaji Midogo Katika Mashirika ya Umma

Mitaji midogo katika Mashirika ya Umma, imekuwa ni tatizo sugu katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, ambayo ina idadi kubwa ya mashirika ambayo hayafanyi kazi kutokana na kukosa mtaji. Kuna haja kwa Serikali kuingilia kati tatizo hili linaloyakumba Mashirika ya Umma kwa kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha na kuiongeza mitaji kwenye Mashirika yanayohitaji mitaji ili kuhakikisha yanafanya kazi kwa ushindani na katika utoaji wa huduma kama ilivyotarajiwa.

### Mapendekezo

Serikali ina wajibu mkubwa wa kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha za kuongeza mitaji kwenye mashirika yanayohitaji ili kuhakikisha utendaji kazi mzuri wa mashirika na utoaji wa huduma bora na za bei nafuu kwa umma.

#### 13.15 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Teknolojia ya habari na mawasiliano ni muhimu sana na isiyoepukika kwa maendeleo ya nchi kutokana na umuhimu wa teknolojia hiyo. Mashirika ya umma mengi hayana kamati za utendaji za kushughulikia mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, wala mpango mkakati, wala mfumo unaotumika kutunza kumbukumbu za taratibu na michakato ya teknolojia ya habari, wala mfumo wa kompyuta wa kutengeneza hesabu itakaowezesha kuboresha uandishi wa taarifa za hesabu kwa ufasaha, ufanisi na usahihi. Wala hayana sera na miongozo madhubuti ya usimamizi mzuri wa matumizi ya kompyuta na intaneti. Mpango wa kujikinga dhidi ya majanga hauko madhubuti hivyo mashirika yapo hatarini kupoteza kumbukumbu na taarifa nyinginezo muhimu pale majanga yatakapotokea.

Mashirika ya umma hayafundishi watumishi wake namna ya kutumia mifumo hii kwa ufanisi. Mashirika mengine hayana hati ya makabidhiano baada ya mzabuni kumaliza taratibu zote za kusimika mfumo husika. Baadhi ya mikataba iliyosainiwa kati ya Mashirika na wagavi ni hatarishi kwa mashirika hususani pale inatokea migogoro yenye kuhitaji maamuzi ya kisheria. Vilevile, kwa upande wa wagavi mifumo ya teknolojia ya habari wanayo simika haina ulinzi madhubuti kuzuia mitandao ya mashirika ya umma isiathirike na virusi wala watu waharibifu.

### Mapendekezo

Menejimenti za mashirika ya umma zinapaswa kuhakikisha kuwa sera za teknolojia ya habari na mawasiliano

zinaandaliwa vizuri kabla ya kuzitumia. Sera zipate idhini ya menejimenti na kisha kusambazwa kwa watumiaji ndani ya shirika husika. Komyuta na mifumo yake inapaswa kutazamwa na kuboreshwa kila wakati, pia kuwepo na sera ya kujilinda dhidi ya virusi viharibifu. Menejimenti za mashirika ya umma zinapaswa kutumia kikamilifu mifumo ya komyuta kutengeneza taarifa za hesabu. Vile vile, mashirika yanapaswa kuwa na mipango na mikakati ya udhibiti dhidi ya majanga ili kulinda komyuta na mifumo yake pale majanga yanapotokea.

Menejimenti za mashirika ya umma ziandae mafunzo ya nguvu kwa watumiaji ili waweze kutumia mifumo hiyo kikamilifu, mikataba na wazabuni isainiwe. Mifumo ikabidhiwe kwa vithibitisho sahihi na hati za makabidhiano zitolewe baada ya kumaliza taratibu zote za makabidhiano.

Menejimenti ya TPA ihakikishe kuwa mfumo wake wa teknolojia ya habari na mawasiliano unatumika kikamilifu kupata taarifa zote zinazohitajika ndani ya TPA na kutoka TRA. Mashirika yatumie mifumo ambayo ni rahisi kutumika na itakayowasaidia wafanyakazi kuachana na kazi za kutotumia komyuta.

#### 13.16 Matokeo ya Ukaguzi Maalumu

Katika mwaka huu wa ukaguzi tulifanya ukaguzi maalum mmoja juu ya vitendo vya ubadhirifu katika Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC). Tulibaini kuwa hapakuwa na hati ya mabadiliko iliyotolewa kuelezea kazi ya nyongeza kwa kiasi au mabadiliko ya bei kuthibitisha malipo ya ziada ya shilingi milioni 24 kwa ajili ya kutambua na kuthibitisha mali za NDC kutoka kwa mzabuni. Zaidi ya hilo hundi zenye namba 806118 na 806113 za kiasi cha shilingi milioni 12 na shilingi milioni 23 zililipwa kwa fedha taslimu na afisa mwandamizi wa Shirika tarehe 26 Februari 2010.

Hata hivyo, tunapenda kutaarifu pia kuwa vitendo hivi vya ubadhirifu vilibainika na kuripotiwa na Menejimenti kwenye Bodi ya Wakurugenzi ambayo imeishachukua hatua zipasazo dhidi ya wafanyakazi waliohusika na ubadhirifu huu.



## Kiambatanisho I

### Orodha ya Makampuni Binafsi ya Ukaguzi Yaliyokagua Mashirika ya Umma

Na	Jina la Kampuni Binafsi ya Ukaguzi
1.	AA - Adolph Associates
2.	ABA Alliance
3.	AMAS Associates
4.	ATAM Consultancy
5.	ATEKAY Accountants and Auditors
6.	Baccon Certified Public Accountants
7.	Baker Tilly DGP & CO
8.	Citizen Certified Partners Consortium
9.	Co-operative Audit and Supervision Corp
10.	DCDM/BDO
11.	Delloite & Touche
12.	Ernst & Young
13.	Global Finance and Business Solution
14.	Globe Accountancy Services Association with Haron & Company
15.	Hassanali Rutakyamirwa & Company
16.	HLB Ashvir
17.	Horwath Tanzania
18.	INNOVEX Auditors
19.	Kavugha & Musambwa Auditors,
20.	KPMG
21.	Martec & Company
22.	MATSAB & Company
23.	MEKONSULT Auditors
24.	MGK Certified Public Accountants
25.	MM Micro Business Consultants
26.	MURL-AATEC Associates
27.	Nyange & Associates,
28.	OREFCO
29.	PAN Associates
30.	Paul Clem Associates
31.	PIMA ASSOCIATES
32.	PKF Tanzania
33.	PricewaterCoopersHouse
34.	Quintex Financial Services
35.	R&S Associates
36.	Reliable Consultants,
37.	RS & Partners

Na	Jina la Kampuni Binafsi ya Ukaguzi
38.	SBC Consultancy Services
39.	Shebrila & Co
40.	SMW Management Consultants
41.	TAC Associates
42.	TANSCOTT
43.	TMC Associates/TOP Consultants Consortium
44.	Trion & Company
45.	VA Business Assurance Services
46.	WISCON Associates
47.	Y.H Malundo & Co,



Hati Inayoridhisha

Na.	Shirika au Taasisi
1.	Benki ya Raslimali Tanzania
2.	Kampuni ya Ranch za Taifa (NARCO)
3.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha
4.	Bodi ya Mfuko wa Bima za Amana
5.	Chuo Cha Uhasibu Arusha
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Bukoba
7.	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)
8.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza
9.	Soko la Hisa Dar es salaam (DSE)
10.	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Usafiri Majini na Nchi Kavu (Sumatra CCC)
11.	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya
12.	Bodi ya Korosho Tanzania
13.	Baraza la Taifa Usimamizi wa Mazingira (NEMC)
14.	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF)
15.	Chuo cha Wanyama Pori (MWEKA)
16.	Bodi ya Chai Tanzania
17.	Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro
18.	Benki ya Posta Tanzania
19.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Babati
20.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro
21.	Baraza la Michezo la Taifa
22.	Benki Kuu ya Tanzania
23.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbeya
24.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji taka Moshi
25.	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania
26.	Bodi ya Usajili wa Wakandarasi
27.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)
28.	Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu
29.	Mfuko wa Pensheni ya Wafanyakazi za Serikali za Mitaa
30.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida
31.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Wasanifu Majenzi (AQRB)
32.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA)
33.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Soko la Mtaji (CMSA)
34.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga
35.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
36.	Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma (PPRA)
37.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha
38.	Chuo Kikuu cha Ardhi
39.	Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania
40.	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA)
41.	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)
42.	Kampuni ya Mbolea Tanzania
43.	Bodi ya Sukari Tanzania

44.	Marine Parks and Reserves Unit (MPRU)
45.	Mamlaka ya Majisafi na Maji Taka Musoma
46.	Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)
47.	Shirika la Viwango Tanzania (TBS)
48.	Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO)
49.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga
50.	Chuo cha Usafirishaji (NIT)
51.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Bima (TIRA)
52.	Hospitali ya Muhimbili
53.	Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini
54.	Kampuni ya Kusimamia Raslimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO)
55.	Shirika la Elimu Kibaha
56.	Chuo cha Technologia Dar es salaam
57.	Benki ya Twiga
58.	Mfuko wa Kuwekeza Tanzania (UTT)
59.	Bodi ya Katani Tanzania
60.	Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere
61.	Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha
62.	Kituo cha Uwekezaji Tanzania
63.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi
64.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma
65.	Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization (TEMDO)
66.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Masomo ya Biashara Moshi
67.	Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA)
68.	Chuo Kikuu cha Sokoine
69.	Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Kiuchumi (NEEC)
70.	Shirika la Tija la Taifa (NIP)
71.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma
72.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Iringa
73.	Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA)
74.	Mamlaka ya Elimu Tanzania
75.	Shirika la Nyumba Tanzania
76.	Mamlaka ya Udhhibiti wa Nishati na Maji (Ewura)
77.	Mamlaka ya Udhhibiti Mawasiliano Tanzania
78.	Mamlaka ya Ukanda wa Utekelezaji Tanzania
79.	Chuo cha Mabaharia Dar es salaam
80.	Shirika la Mafuta Tanzania
81.	Marine Service Company Ltd
82.	Bodi ya Biashara ya Nje (BET)
83.	Kituo cha Utafiti Teknolojia ya Kilimo Vijijini
84.	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)
85.	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)
86.	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa (GEPF )
87.	Tume ya Ushindani (FCC)
88.	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Nishati na Maji (Ewura CCC)
89.	Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Rufiji(RUBADA)
90.	Bodi ya Utalii Tanzania
91.	Chuo cha Technologia cha Arusha
92.	Ubungo Plaza Co Ltd.

### Hati Inayoridhisha yenye Masuala ya Msisitizo

Na.	Shirika/Taasisi
1.	Shirika Hodhi la Rastimali za Mashirika ya Umma
2.	Baraza la Sanaa la Taifa(NAC)
3.	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)
4.	Chuo Kikuu cha Mzumbe
5.	Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tabora.
7.	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)
8.	Shirika la Hifadhi Za Tanzania (TANAPA)
9.	Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa elimu ya juu.
10.	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)
11.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania
12.	Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa

### Hati Zenye Kasoro

Na.	Shirika/Taasisi
1.	Shirika la Magazeti Tanzania.
2.	Maktaba Kuu ya Taifa
3.	Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)
4.	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)
5.	Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania(TFNC)
6.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara.
7.	Taasisi ya Idara ya Madawa
8.	Chuo Kikuu cha Afya na Sayasi za Tiba Muhimbili (MUHAS)
9.	Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA).
10.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi

### Hati Zenye Kasoro Zenye Masuala ya Msisitizo

Na.	Shirika/Taasisi
1.	Shirika la Posta Tanzania.
2.	Bodi ya Kahawa Tanzania
3.	Kampuni ya Maji Safi na Maji Taka Dar es salaam(DAWASCO)
4.	Shirika la Bima la Taifa (NIC)
5.	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar-es-salaam(DAWASA)
6.	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
7.	Bodi ya Pamba Tanzania
	Mkaguzi kushindwa kutoa maoni
1.	Shirika la Masoko Kariakoo



### Kiambatanisho III

A	Taasisi za fedha, Mifuko ya Pensheni na Kampuni za Bima	Hesabu Zimepo kelewa	Ukaguzi Unaendelea	Kuhakiki Ubora wa Ripoti	Hesabu Zinasubiri Kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Ripoti Zilizokamilika
1.	Benki Kuu ya Tanzania (BOT)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
2	Mfuko wa Taifa wa Mafao ya Watumishi wa Serikali za Mitaa (GEPF).	Ndiyo	-		Ndiyo	-
3	Insurance Deposit Fund	Ndiyo	-		-	Ndiyo
4	Local Authority Provident Fund	Ndiyo	-		-	Ndiyo
5	Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)	Ndiyo			-	Ndiyo
6	Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma. (PPF)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
7	Mfuko wa Mafao ya Wafanyakazi wa Umma (PSPF)	Ndiyo	Ndiyo		-	-
8	Benki ya Rasimali Tanzania (TIB)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
9	Benki ya Posta Tanzania	Ndiyo	-		-	Ndiyo
10	Benki ya Twiga	Ndiyo	-		-	Ndiyo
11	Mfuko wa Kuwekeza Tanzania (UTT)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
12	Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya	Ndiyo	-		-	Ndiyo
13	Shirika la bima la Taifa	Ndiyo	-		-	Ndiyo
14	Soko la Hisa Dar es salaam (DSE)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
15	Mamlaka ya Udhhibiti wa Hisa na Mitaji (CMSA)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
16	Mamlaka ya Usajili wa Bima Tanzania (TIRA)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
B	Taasisi za Uzalishaji	Hesabu Zimepo-	Ukaguzi Unae-	Kuhakiki Ubora wa	Hesabu Zinasubiri	Ripoti Zilizokami-

		kelewa	ndelea	Ripoti	Kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	lika
1	Taasisi ya Taifa ya Sukari	Ndiyo		Ndiyo	-	-
2	Mamlakaa ya Hifadhi ya Ngorongoro	Ndiyo	-		-	Ndiyo
3	Shirika la Maendeleo la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
4	Shirika la Madini Tanzania (STAMICO)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
5	Kampuni ya Mbolea Tanzania.	Ndiyo	-			Ndiyo
6	Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization (TEMDO)	Ndiyo	-			Ndiyo
7	Shirika la Mafuta Tanzania (TPDC)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
8	Kampuni ya Ranch za Taifa (NARCO)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
9	Shirika la Magazeti Tanzania.	Ndiyo	-		-	Ndiyo
10	Shirika la Nyumba Tanzania	Ndiyo	-		Ndiyo	-
11	Ubungo Plaza Co. Ltd	Ndiyo	-		Ndiyo	-
12	NHC/PPF IPS Building	Ndiyo		Ndiyo	-	-
13	Shirika la posta Tanzania	Ndiyo	-		Ndiyo	-
14	Shirika la Tija la Taifa (NIP)	Ndiyo	-		Ndiyo	-
15	Shirika la Kutengeneza Magari (NYUMBU)	Ndiyo				
16	Taasisi ya Idara ya Madawa	Ndiyo	-			Ndiyo
17	Kampuni ya Kutengeneza Matairi	Hapana	-		-	-
18	Kampuni ya Maendeleo ya Kiwanja cha Ndege Kilimanjaro	Hapana	-		-	-

C	Bodi za Udhhibiti, Mabaraza, Kamisheni, na Mamlaka	Hesabu Zimepokelewa	Ukaguzi Unae-ndelea	Kuhakiki bora wa Ripoti	Hesabu Zinasubiri Kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Ripoti Zilizokamilika
1.	Bodi ya Usajili wa Wabunifu na Wasanifu majenzi (AQRB)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
2.	Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
3.	Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi (NLPC)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
4.	Shirika la Nguvu za Atomic	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-
5.	Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
6.	Tume ya Ushindani (FCC)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-
7.	Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC)	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-
8.	Baraza la Kiswahili Tanzania	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
9.	Benjamin William Mkapa Foundation	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
10.	Bodi ya Biashara ya Nje (BET)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
11.	Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkuu Dodoma (CDA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
12.	Bodi ya Usajili ya Wakandarasi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
13.	Bodi ya Usajili ya Waandishi	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
14.	Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na maji (Ewura)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
15.	Bodi ya michezo ya kubahatisha Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
16.	Baraza la sanaa Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
17.	Bodi ya Taifa ya wahasibu na wakaguzi wa hesabu	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
18.	Bodi ya manunuzi	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-
19.	Bodi ya Mikopo ya	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-

	Wanafunzi wa elimu ya juu.					
20	Baraza la Ujenzi la Taifa. (NCC)	Ndiyo		Ndiyo	-	-
21	Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
22	Baraza la Taifa la uwezesaji wa kiuchumi (NEEC)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
23	Baraza la mitihani Tanzania (NECTA)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
24	Baraza la Michezo Tanzania	Ndiyo	-		-	Ndiyo
25	Baraza la Taifa la uwezekaji wa kiuchumi (NEEC)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
26	Bodi ya pareto Tanzania	Ndiyo		Ndiyo	-	-
27	Mamlaka ya maendeleo ya Bonde la Rufiji. (RUBADA)	Ndiyo				Ndiyo
28	Bodi ya sukari Tanzania	Ndiyo	-			Ndiyo
29	Bodi ya Tumbaku Tanzania	Ndiyo		Ndiyo	-	-
30	Bodi ya katani Tanzania	Ndiyo	-	-		Ndiyo
31	Shirika la Viwango Tanzania. (TBS)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
32	Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
33	Bodi ya Korosho Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
34	Mamlaka ya Bandari Tanzania	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
35	Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu Na Majini (Sumatra)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
36	Mamlaka ya anga Tanzania (TCAA)	Ndiyo	-		Ndiyo	-
37	Bodi ya kahawa Tanzania	Ndiyo	-		-	Ndiyo
38	Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)	Ndiyo		Ndiyo	-	-
39	Mamlaka ya Kudhibiti manunuzi ya Umma (PPRA)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
40	Mamlaka ya udhibiti	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-



	Mawasiliano Tanzania. (TCRA)					
41	Bodi ya Pamba Tanzania	Ndiyo	-			Ndiyo
42	Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
43	Mamlaka ya Elimu Tanzania	Ndiyo	-	-		Ndiyo
44	Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania(TFNC)	Ndiyo	-		Ndiyo	-
45	Tanzania Marine Parks	Ndiyo	-		Ndiyo	-
46	Bodi ya Chai Tanzania	Ndiyo	-		-	Ndiyo
47	Bodi ya Utalii Tanzania	Ndiyo	-		Ndiyo	-
48	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege	Ndiyo	Ndiyo		-	-
49	Mamlaka ya Ukanda wa Uwekezaji Tanzania. (EPZA)	Ndiyo			Ndiyo	-
50	Shirika la Haki Miliki Tanzania. (COSOTA)	Ndiyo	Ndiyo		-	-
51	Shirika Hodhi la Raslimali za Mashirika ya Umma(CHC)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
52	Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
53	Kampuni ya Kusimamia Raslimali za Shirika la Reli Tanzania (RAHCO)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
54	Hifadhi za Taifa za Tanzania (TANAPA)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
55	Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)	Ndiyo	-		Ndiyo	-
56	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri Majini na Nchi Kavu. (SUMATRA CCC)	Ndiyo	-		-	Ndiyo

D	Vyuo vya Elimu ya juu, Tafiti, Mafunzo	Hesabu Zimepo kelewa	Ukaguzi Unae-ndelea	Kuhakiki Ubora wa Ripoti	Hesabu Zinasubiri kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Ripoti Zilizoka-milika
1.	Chuo Kikuu cha Ardhi	Ndiyo	-		-	Ndiyo
2.	Chuo Cha Elimu ya Biashara	Ndiyo	Ndiyo		-	-
3.	Chuo cha Technologia Dar es salaam	Ndiyo	-			Ndiyo
4.	Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam	Ndiyo	-		-	Ndiyo
5.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)	Ndiyo	Ndiyo		-	-
6.	Chuo cha Uhasibu Arusha	Ndiyo	-		-	Ndiyo
7.	Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya	Ndiyo	Ndiyo		-	-
8.	Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima	Ndiyo	-		-	Ndiyo
9.	Chuo cha Usimamizi wa Fedha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
10.	Chuo Cha Mipango na Vijijini	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
11.	Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
12.	Shirika la Elimu Kibaha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
13.	Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.	Ndiyo	-	-		Ndiyo
14.	Chuo Kikuu Cha Mkwawa	Ndiyo		Ndiyo	-	-
15.	CARMATEC	Ndiyo		-	Ndiyo	-
16.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Masomo ya Biashara Moshi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
17.	Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi ya Afya Muhimbili (MUCHS)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
18.	Chuo cha Wanyama Pori (MWEKA)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
19.	Chuo Kikuu cha Mzumbe	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo

20	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa	Ndiyo	Ndiyo			-
21	Chuo cha Usafirishaji (NIT)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
22	Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
23	Chuo Kikuu Cha Sokoine.	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
24	Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
25	Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
26	Arusha Technical College	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
27	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.	Ndiyo	Ndiyo		-	-
28	Chuo Kikuu cha Dodoma	Ndiyo		Ndiyo	-	-
29	Chuo cha Ufundi Stadi Tanzania (VETA)	Ndiyo			Ndiyo	-
30	Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania	Ndiyo	-		-	Ndiyo
31	Taasisi ya Utafiti na Uvuvi Tanzania (TAFIRI)	Ndiyo	Ndiyo		-	-
32	Taasisi ya Utafiti ya Wanyama Pori (TAWIRI)	Ndiyo		Ndiyo	-	-
33	Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Madawa (TPRI)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
34	Centre for Foreign Relation	Ndiyo		Ndiyo	-	-
35	Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO)	Ndiyo	Ndiyo		-	-
36	Shirika la Utangazaji Tanzania(TBC)	Ndiyo	-			Ndiyo

E	Mashirika ya Kutoa Huduma	Hesabu Zimepokelewa	Ukaguzi Unae-ndelea	Kuhakiki Ubora wa Ripoti	Hesabu Zinasubiri Kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi	Ripoti Zilizokamilika
1	Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TANESCO)	Ndiyo	-	-		Ndiyo
2	Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL)	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
3	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
4	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Bukoba	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
5	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Babati	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
6	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam (DAWASA)	Ndiyo		-	Ndiyo	-
7	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dar es Salaam	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
8	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
9	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Iringa	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
10	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kigoma	Ndiyo	-	-	Ndiyo	
11	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Lindi	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
12	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbeya	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
13	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Morogoro	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
14	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
15	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo

	Moshi					
16	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mtwara	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
17	Marine Services Company	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
18	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Musoma	Ndiyo	-	-	Ndiyo	-
19	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbinga	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
20	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Rukwa	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-
21	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida	Ndiyo		-	-	Ndiyo
22	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga	Ndiyo	-		-	Ndiyo
23	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea	Ndiyo	-	Ndiyo	-	-
24	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tabora	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
25	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tanga	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
26	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Tukuyu	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
27	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kyela	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
28	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Ngara	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
29	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Korogwe	Hapana	-	-	-	-
30	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mpanda	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
31	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Njombe	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
32	Shirika la Masoko ya Kariakoo	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
33	Maktaba Kuu ya	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo

	Taifa					
34	Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
35	Usafiri Dar-es-Salaam (UDA)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	-
36	Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.	Ndiyo	-	-	-	Ndiyo
37	Shirika la Ndege Tanzania (ATC)	Ndiyo	Ndiyo	-	-	
38	Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha	Ndiyo	-		-	Ndiyo
39	Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)	Ndiyo	-		-	Ndiyo
40	Kituo cha Uwekezaji Tanzania	Ndiyo	-		-	Ndiyo
41	Makumbusho ya Taifa	Ndiyo	Ndiyo		-	-
42	Baraza la Ushauri la Watumia Huduma wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura CCC)	Ndiyo			-	Ndiyo
43	Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Kahama	Ndiyo	Ndiyo		-	-

*Kiambatanisho IV*

Orodha ya Mashirika Ambayo Yametengwa kwa Ajili ya Kubinafsishwa.

1.	Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL)	Lipo kwenye mchakato wa kumtafuta mwekezaji.
2.	Aluminium Africa	Lipo kwenye mchakato wa kuuza asilimia 25 ya hisa za Serikali.
3.	BP Tanzania Ltd	Lipo kwenye mchakato wa kuuza asilimia 50 ya hisa za Serikali.
4.	Kiwanda cha Matairi Arusha (General Tyre EA Ltd)	Kipo kwenye mchakato wa kuudwa upya.
5.	Kiwanda cha Madawa Keko :	Kipo kwenye mchakato wa kuuza asilimia 40 ya hisa za serikali.
6.	Kampuni ya Matofali Kisarawe:	Ipo kwenye mchakato wa kuuza asilimia 30 ya hisa za serikali.
7.	Kampuni ya Huduma za Meli:	Ipo kwenye mkakati wa kuudwa upya.
8.	MECCO:	Ipo kwenye mchakato wa kuuza asilimia 25 ya hisa za Serikali.
9.	Mikumi Wildlife Lodge:	Inatakiwa kuuzwa kwa mwekezaji.
10.	Kiwanda cha vifaa vya Ngozi Morogoro :	Jengo la kiwanda linatakiwa kuuzwa.
11.	Shamba la Mahindi Namtumbo:	Linatakiwa kuuzwa kwa mwekezaji.
12.	Shamba la Journeys End ;	Linatakiwa kuuzwa kwa mwekezaji.
13.	Shamba la Foster ;	Linatakiwa kuuzwa kwa mwekezaji.

14.	Shamba la Harlington ;	Linatakiwa kuuzwa kwa mwekezaji.
15.	Shamba la Kanamodo	Linatakiwa kuuzwa kwa mwekezaji.
16.	Shirika la Bima la Taifa (NIC):	Lipo kwenye mchakato wa kuudwa upya..
17.	Tangold (Kiwanda cha Korogwe):	Kipo kwenye mchakato wa kuuzwa na rasilimali zake kwa mwekezaji.
18.	Benki ya Biashara(NBC Limited):	Ipo kwenye mchakato wa kuuza asilimia 30 ya hisa za serikali.
19.	New Africa Hotel:	Ipo kwenye mchakato wa kuuza asilimia 23 ya hisa za serikali.
20.	NMB:	Ipo kwenye mchakato wa kuuza asilimia 1.78 ya hisa za serikali.
21.	PEHCOL:	Kwenye mchakato wa kuuza maeneo ya Sumbawanga na Tabora
22.	UDA:	Lipo kwenye mchakato wa kuuza asilimia 51 ya hisa za serikali.
23.	Kampuni ya MajiSongwe:	Ipo kwenye mchakato wa uuzaji wa mali zake.
24.	Kiwanda cha TPL Mbeya :	kipo kwenye mchakato wa uuzaji wa mali zake
25.	TPL Kitaraka Holding Ground:	Eneo lote lipo kwenye mchakato wa kuuzwa kwa mwekezaji.



26.	TANSCAN:	Ipo kwenye mchakato wa kuuza hisa asilimia 49 za serikali.
27.	Shirika la Posta la Tanzania.	Lipo kwenye Mkakati wa kuudwa upya.
28.	TDFL:	Lipo kwenye mchakato wa uuzaji wa asilimia chache za serikali.
29.	Kiwanda cha Sukari TPC Moshi:	Mchakato wa uuzaji wa asilimia 25 za Serikali unaendelea.
30.	Mashamba ya Mkonge Kibaranga:	Lipo kwenye mchakato wa uundwaji upya na Mufilisi.
31.	Kiwanda cha Korosho	Ipo kwenye mchakato wa uuzaji wa wa Stoo ya Kilwa.
32.	Shirika La Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL)	Lipo kwenye mchakato wa kundwa upya.
33.	Machimbo ya Makaa ya Mawe Kiwira,	Serikali ichukue asilimia 70 ya hisa za Tanpower Resources Ltd.
34.	Mwanza RTC:	Ipo kwenye mchakato wa uuzaji wa stoo zilizobaki.